ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha kumi na Tatu - Tarehe 7 Juni, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika *(Zubeir Ali Maulid)* Alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio ya Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nadhani mtaona kwamba kwenye *order paper* yetu ya leo hatuna masuali na tumefanya hivyo makusudi kwa sababu, Waziri anayesoma hivi punde anayewasilisha hoja yake alipaswa aanze kuiwasilisha jana. Kwa hivyo katika kuokoa huo muda ambao tumeupoteza nimetoa maelekezo kwamba tusiwe na masuala leo ili kuweza kumruhusu Mheshimiwa sasa aweze kuiwasilisha hoja yake na ianze kuchangiwa, ili kuweza kupata wachangiaji wengi zaidi pamoja na ule muda ambao tumeuzidisha.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo hayo niungane nanyi kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kukutakieni funga njema. Ahsante.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 - Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kabla ya lolote kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutujaalia asubuhi hii ya leo pamoja na neema kem kem zilizotushukia kupata fursa hii, kuja kuweka kusudio la kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha na mimi nataka nichukue fursa ambayo wewe umeichukua kuwatakia Waheshimiwa wote wawakilishi wa Baraza hili la Wawakilishi tukufu kuingia katika mfungo huu wa Mwezi mtukufu wa

Ramadhani ikiwa leo hii ni siku yetu ya awali, na mimi niwatakie Ramadhani kareem, inshaallah.

Baada ya hayo sasa naomba kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Zanzibar, yenye kusudio la Makadirio ya Mapato na Matumizi katika baraza hili la wawakilishi kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi, kwa kutujaalia afya njema na kukutana hapa ili kujadili mambo muhimu ya maendeleo ya nchi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze ili tuweze kutekeleza kazi hii kwa hekima, busara na uadilifu, na atuwezeshe kufanikisha majukumu yetu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, kwa furaha kubwa naomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa tena na wananchi kuiongoza Zanzibar kwa awamu ya pili, katika Uchaguzi Mkuu wa Marudio uliofanyika Machi 20, 2016.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Balozi Seif Ali Iddi kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar. Kuteuliwa kwake ni ushahidi kwa uwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya Serikali na kutoa mchango wake katika kuwaletea wananchi maendeleo yao katika shughuli za kila siku.

Mhe. Spika, vile vile napenda kukupongeza kwa dhati wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Spika mpya wa Baraza la 9 la Wawakilishi, na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu akujaalie uwezo, hekima na busara katika kuliongoza vyema Baraza letu. Aidha, sina budi kuwashukuru wasaidizi wako wote Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza, Maofisa na Wafanyakazi wote wa Baraza kwa kazi nzuri ya kuliongoza Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba kuwapongeza wajumbe wa Baraza lako tukufu waliochaguliwa na wananchi pamoja na walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili kuweza kujadili na kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imeundwa na sekta kuu nne ambazo ni Sekta ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo zilizo chini ya taasisi 16 zikiwemo Idara tano, Kamisheni 2, Mabaraza 3, Mashirika 2, Vyuo 2 na Kampuni 1. Taasisi hizi ni kama zifuatazo:-

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Ofisi Kuu Pemba
4. Shirika la Utangazaji Zanzibar *(ZBC)*
5. Idara ya Habari Maelezo
6. Shirika la Magazeti ya Serikali
7. Chuo cha Uandishi wa Habari
8. Tume ya Utangazaji
9. Kampuni ya Usambazaji Maudhui *(ZMUX)*
10. Kamisheni ya Utalii
11. Chuo cha Maendeleo ya Utalii
12. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo
13. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
14. Baraza la Kiswahili *(BAKIZA)*
15. Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni *(BASSFU)*
16. Baraza la Taifa la Michezo *(BTMZ)*

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa niruhusu kutoa maelezo kuhusu Bajeti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2016/2017. Katika maelezo hayo nitatoa uchambuzi wa utekelezaji wa programu tulizoahidi kutekeleza katika mwaka wa fedha 2015/2016.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ilikadiria kupata shilingi 13,052,200,000/= kwa ajili ya kutekeleza programu kuu 5. Kwa kazi za kawaida ni shilingi 10,072,200,000/= na shilingi 2,980,000,000/= kwa kazi za maendeleo ikiwa shilingi 480,000,000/= ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa uwanja wa Mao Tse Tung na shilingi 2,500,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maabara ya Utalii. Aidha, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,984,282,000/= zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 1,594,000,000/= zinazokusanywa na kutumiwa na Taasisi husika.

Mhe. Spika, jumla ya Shilingi 5,411,980,250/= zilipatikana kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 54 ya shilingi 10,072,200,000/=. Aidha, Wizara ilikusanya shilingi 1,590,195,558/= sawa na asilimia 80 ya shilingi 1,984,282,000/= zilizoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 1,001,596,124/= sawa na asilimia 63 ya shilingi 1,594,000,000/= ambazo zimekusanywa na kutumiwa na Taasisi za Wizara *(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1 A hadi 1E).*

TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imefanikiwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

Programu ya Pamoja ya Kuimarisha na Kuendeleza Sekta ya Utalii

UTEKELEZAJI

Mhe. Spika, katika jitihada za kuimarisha na kukuza utalii nchini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzisha Programu ya Maabara ya Utalii katika juhudi za kujua na kuondo changamoto zinazoikabili Sekta ya Utalii ili kuendelea kuchangia pato la nchi na kuinua hali ya uchumi na kijamii sambamba na kuimarisha sekta zote zilizopo nchini. Lengo kuu la programu hii ni kuimarisha utalii wetu na kufikia utalii wa daraja la juu kama inavyoelezwa katika Sera ya Utalii na Mipango Mikuu ya Serikali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,500,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza Programu hii ili kutekeleza shughuli tofauti zinazotekelezwa na sekta tofauti za Serikali ambazo zimegawika katika maeneo makuu 6 nayo ni: Bidhaa za Utalii na Huduma (Shilingi 437,600,000/=), Kuimarisha harakati za Utangazaji wa Sekta ya Utalii (Shilingi 75,000,000/=), Kuongeza Ulinzi na Usalama kwa watalii na wawekezaji pamoja na mali zao (Shilingi 650,000,000/=), Kuimarisha Miundombinu ya Utalii (Shilingi 865,252,394/=), Kuimarisha Mazingira na faida za Utalii kwa jamii (Shilingi 252,147,606/=) na Kuimarisha Utawala katika Sekta ya Utalii (Shilingi 220,000,000/=).

Mhe. Spika, Programu ya Maabara ya Utalii imejumuisha miradi midogo midogo 35 ambayo inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu,

2014/2017. Kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 miradi ambayo imejumuisha shughuli mbali mbali ilitarajiwa kutekelezwa. Kutokana na nchi kukabiliwa na majukumu makubwa ya kitaifa ikiwemo Uchaguzi Mkuu wa 2015, programu hii ilishindikana kutekelezwa kama ilivyotararjiwa.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyengine iliweza kupitia Mpango Mkuu wa Maabara ya Utalii ili kupitia shughuli ambazo zishatekelezwa katika taasisi husika zipate kuondolewa katika mpango huo.

Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Mao tse Tung

Mhe. Spika, hatua za awali za kusafisha uwanja zimekamilika ikiwa ni matayarisho ya ujenzi wa Uwanja wa Mao tse Tung. Aidha, shughuli zilizotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kufikisha umeme katika eneo la kiwanja, kuweka miundombinu ya simu na kufikisha maji safi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mradi huu ulipangiwa jumla ya shilingi 480,000,000/= na hadi kufikia Machi 2016 mradi huu haujaingiziwa fedha.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ilipanga kutekeleza programu kuu 5 kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji.
2. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo.
3. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii.
4. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii.
5. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Programu ya 1: Maendeleo ya Habari na Utangazaji.

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa na jamii iliyoimarika katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia habari. Aidha, programu hii imepangiwa programu ndogo 2 nazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa vyombo vya Habari na Utangazaji.

Mhe. Spika, programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari inatekelezwa na Taasisi tofauti nazo ni, Shirika la Utangazaji Zanzibar *(ZBC)*, Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Chuo cha Uandishi wa Habari na Kampuni ya Usambazaji Maudhui *(ZMUX)*.

Mhe. Spika, huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ndogo ni urushaji wa vipindi kupitia Televisheni na Redio, utoaji wa taarifa, picha, makala, filamu na sinema, uchapishaji wa magazeti, utoaji wa mafunzo ya habari na mawasiliano na usambazaji wa maudhui ya utangazaji.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika kufanikisha huduma zake Shirika la Utangazaji limefanikiwa kuwapatia wananchi taarifa na matukio mbali mbali ya kijamii na Kiserikali ndani na nje ya nchi. Jumla ya vipindi 8,248 vimerushwa kupitia *ZBC TV* na 10,008 kupitia *ZBC* Redio vikiwemo taarifa za kujikinga na maradhi ya kipindupindu, uhaulishaji wa ardhí, kupinga vitendo vya rushwa na unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto na wanawake na jumla ya vipindi 10,080 vya nje vimerushwa kupitia *ZBC TV*. Pia Shirika limefanikiwa kurusha jumla ya matangazo 14,300 kupitia *ZBC TV* na Redio.

Mhe. Spika, matangazo ya moja kwa moja yamerushwa yakiwemo Mikutano ya Baraza la Wawakilishi, Vipindi vya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015 na Uchaguzi wa Marudio wa Machi 2016, Sherehe za miaka 52 ya Mapinduzi, Sherehe za Kuapishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Uzinduzi wa Baraza la 9 la Wawakilishi, Sherehe za kuwaapisha Mawaziri na Manaibu Waziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na makongamano mbali mbali ya kuhamasisha amani, utulivu na ustawi wa jamii wa nchi.

Mhe. Spika, katika kuinua kiwango cha uelewa wa wananchi, Idara ya Habari Maelezo imesambaza taarifa 1200 katika magazeti na *blogs*. Taarifa hizo zinahusu masuala ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 25, 2015 na Uchaguzi wa Marudio wa Machi 20, 2016 pamoja na shughuli nyengine za kiuchumi na kijamii. Aidha, vijiji 45 vya Unguja vimeweza kuoneshwa sinema kuhusu elimu ya Uchaguzi na elimu ya afya juu ya maradhi ya mripuko wa kipindupindu na malaria. Vile vile, umefanyika usambazaji wa picha za viongozi wa kitaifa 1500 na machapisho ya Baraza la Mawaziri 1200.

Mhe. Spika, Shirika la Magazeti ya Serikali limefanikiwa kusimamia uchapishaji wa Magazeti ya Serikali na kuyasambaza katika Mikoa ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa lengo la kuelimisha na kuhabarisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Jumla ya nakala 1,080,000 kwa gazeti la kila siku (Zanzibar Leo) na nakala 156,000 kwa gazeti la wiki la michezo (*Zaspoti*) zimechapishwa. Idadi ya matangazo yaliyochapishwa yamefikia 720.

Mhe. Spika, katika Chuo cha Uandishi wa Habari, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kwa mwaka wa masomo ya muda mrefu 2015/2016 imeongezeka kufikia wanafunzi 120 ikilinganishwa na wanafunzi 100 kwa mwaka 2014/2015, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kwa mafunzo ya muda mfupi ni 45, idadi ya wahitimu waliopatikana kwa mafunzo ya muda mrefu ni 107, idadi ya wahitimu waliopatikana kwa mafunzo ya muda mfupi ni 20 na idadi ya ziara za kimasomo zilizofanyika ni 2.

Aidha, Chuo kimefanikiwa kuajiri wakufunzi 3 katika fani za Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma pamoja na kuongeza fani 2 mpya za Uhusianao wa Kimataifa na Uhusiano wa Umma ili kuimarisha utoaji wa mafunzo ya Chuo. Jumla ya vitabu 100 vya fani tofauti za mawasiliano ya umma vimenunuliwa na kuingizwa katika maktaba ya Chuo ili kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa urahisi. Katika kubadilishana programu za mafunzo na taasisi nyengine za elimu, Chuo kimeweza kufanya mazungumzo ya awali na Chuo cha Uandishi wa Habari katika Chuo Kikuu cha Dar-es -Salaam *(UDSM).*

Mhe. Spika, Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX) imeongeza chaneli katika king'amuzi chake kutoka 21 hadi 30 ambazo hivi sasa zinaonekana vizuri. Aidha, katika kuimarisha huduma zake Kampuni imeweka vifaa katika vituo vyake vya kurushia matangazo vikiwemo *'microwave link', 'genneretor', 'trip connector'* (kidhibiti umeme) pamoja na *'play out series'.*

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 3,621,853,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 imefanikiwa kupata shilingi 2,121,152,520/= sawa na asilimia 59 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,178,000,000/= hadi kufikia Machi 2016 jumla ya shilingi 762,963,529/= zimekusanywa sawa na asilimia 65. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E)

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji inatekelezwa na Taasisi 2 ambazo ni, Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji.

Mhe. Spika, huduma zinazotolewa katika programu ndogo hii ni udhibiti na usimamizi wa shughuli za habari na utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji.

Mhe. Spika, katika kufanikisha huduma zake Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutoa vitambulisho 450 kwa waandishi wa habari mbali mbali wakiwemo walioshiriki Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015 na Uchaguzi wa

Marudio wa Machi, 2016. Tume ya Utangazaji imetoa miongozo 2 kwa vyombo vya Utangazaji nchini juu ya kuripoti habari za Uchaguzi na kuhusu sifa za ving'amuzi vinavyotakiwa kuingizwa nchini. Aidha, vituo 5 vya utangazaji vimepatiwa leseni vikiwemo 4 vya Redio na 1 cha Televisheni. Kwa upande wa Redio ni Bahari FM, Swahiba FM, TBC na Azam FM, na kituo cha Televisheni ni SUZA TV.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 220,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 imefanikiwa kupata shilingi 132,555,550/= sawa na asilimia 60 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 65,000,000/= hadi kufikia Machi 2016 jumla ya shilingi 17,550,000/= zimekusanywa sawa na asilimia 27 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).

Programu ya 2: Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utamaduni wa Zanzibar unawaendeleza vizuri wasanii kiuchumi na kupunguza umasikini pamoja na kuwa na rasilimali watu yenye ujuzi na ustadi wa kukuza utalii nchini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya zao na ajira kwa jamii. Programu hii ina programu ndogo 2 ambazo ni uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria pamoja na uendelezaji wa rasilimali watu katika utalii na ukuzaji wa michezo.

Mhe. Spika, programu ndogo ya uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria imeundwa na taasisi zifuatazo; Kamisheni ya Utalii na Michezo, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

Mhe. Spika, huduma zinazotolewa na programu ndogo hii ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, kurikodi kazi za sanaa kupitia studio ya filamu na muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili, uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria, uelimishaji na ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na urithi wa utamaduni.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Baraza la Sanaa na Sensa za Filamu na Utamaduni limeweza kuratibu jumla ya matamasha 7 ya utamaduni

yenye lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kupitia Utamaduni na kutengeneza ajira kwa jamii sambamba na kuitangaza nchi kiutalii. Matamasha hayo ni ya Utamaduni wa Mzanzibari, Sauti ya Busara, Tamasha la Filamu la nchi za Jahazi (ZIFF), Tamasha la Watu wa Mangapwani, Tamasha la Kiislamu (ZEIF), Tamasha la Muziki wa JAZZ, Tamasha la Mwaka Kogwa na Tamasha la Vyakula vya Kizanzibari. Aidha, vikundi vya sanaa vimepata fursa ya kushiriki matamasha nje ya Zanzibar kama vile Tamasha la Utamaduni nchini Oman, Ujerumani, Ufaransa, Israil, Kenya, Comoro na Japan ambapo mafanikio makubwa yamepatikana ya wasanii wetu kujifunza mbinu zinazotumiwa na wenzetu kuendeleza mila na silka zao pamoja na kukuza uhusiano na ushirikiano kati ya wasanii wa ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, Studio mpya ya Kurikodia Filamu na Muziki Rahaleo iliyofunguliwa rasmi tarehe 08/01/2016 na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein imetoa fursa kwa wasanii wetu kurikodi kazi zao za sanaa hapa visiwani bila ya usumbufu wowote, kutokana na mnasaba huu kazi za sanaa zimerikodiwa zikiwemo ngoma za asili, muziki wa kizazi kipya pamoja na filamu *(Zenj Movies)*, matangazo mafupi, taarab za kiasilia na za kisasa, kasida na kwaya vyote vinarekodiwa.

Mhe. Spika, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni pia limeweza kufanya vikao 11 kwa kukutana na Masheha katika Wilaya na vikao 5 vya kukutana na wasanii wa fani tofauti kwa lengo la kuelimisha juu ya mabadiliko ya Sheria mpya na utekelezaji wake. Aidha, katika kusimamia maadili ya kazi za sanaa, rasimu za michezo ya kuigiza 15, mashairi ya nyimbo mchanganyiko 7, filamu mchanganyiko 46, tenzi 7 zenye maudhui mbali mbali na michezo 4 ya jukwaani imekaguliwa.

Mhe. Spika, katika kukuza na kuendeleza Kiswahili, Baraza la Kiswahili la Zanzibar limefanya mashindano ya uandishi wa tamthilia, makongamano 3 yamefanyika ambayo ni kwa walimu wa skuli za sekondari katika kuadhimisha Siku ya Kiswahili. Lengo ni kuwasaidia walimu wa Kiswahili kufahamu mada zenye matatizo kwenye ufundishaji wa somo la Kiswahili, kongamano kwa wahariri na waandishi wa habari juu ya matumizi fasaha na sahihi ya Kiswahili na kongamano lililojumuisha wadau na wapenzi wa Kiswahili kutoka Zanzibar na Tanzania Bara. Aidha, Baraza limechapisha nakala 1000 za Jarida la Baraza la Kiswahili Zanzibar linaloitwa JAHAZI Toleo No. 1 lenye kutoa taaluma ya lugha na fasihi ya Kiswahili kwa lengo la kusambaza maarifa yanayohusu lugha na fasihi ya Kiswahili.

Mhe. Spika, katika kutoa taaluma juu ya matumizi sahihi na fasaha ya Kiswahili kupitia vyombo vya habari pamoja na kukitangaza Kiswahili kitaifa na kimataifa, Baraza la Kiswahili Zanzibar limerusha vipindi 12 ZBC Redio na vipindi 14 ZBC TV. Pia Baraza limeshiriki katika vikao 2 vya Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki vilivyofanyika Dar es Salaam na Zanzibar kwa lengo la kujadili mambo yanayohusu Kamisheni hiyo.

Mhe. Spika, katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Prof. Adrian, mtaalamu kutoka Chuo cha Virginia Marekani imefanya tafiti katika maeneo ya kihistoria ya Mvuleni, Pale, Fukuchani na Pwani ya Wadeburi. Aidha, kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo cha *Oxford* Uingereza na Australia zimefanyika kazi za uchambuzi wa vielelezo vya utafiti vilivyokusanywa katika maeneo ya Unguja Ukuu, Fukuchani, Kuumbi kwa upande wa Unguja na Ras Mkumbuu na Pango la Watoro kwa Pemba. Mheshimiwa naomba kuomba radhi kwa neno ambalo limejitokeza ni Chuo cha *Virgin* ya Marekani. Kazi ya utayarishaji muongozo wa kuyaendeleza maeneo ya Urithi wa Kihistoria na Utamaduni ili kuyaongezea vivutio vya utalii na kujenga ushawishi wa kutembelewa na wageni wengi imekamilika.

Mhe. Spika, katika kuyatangaza maeneo ya kihistoria na kuanzisha programu zitakazowasaidia wananchi kujenga muamko wa kuyajua, kuyatembelea na kuyalinda maeneo ya kihistoria. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale iliandaa vipindi 8 vilivyorikodiwa na kurushwa hewani kupitia ZBC Redio, TV na Zenj FM. Aidha, mikutano 5 imefanyika kwa viongozi wa vijiji vya Fukuchani, Pete-Machaga, Kuumbi na Bungi inayohusu umuhimu wa kuyatunza na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria.

Mhe. Spika, ziara za kuwatembeza katika maeneo ya kihistoria zimefanyika kwa watoto mayatima 35 kutoka Ustawi wa Jamii, viongozi 20 wa timu za mpira kutoka vilabu mbali mbali vya Ligi Kuu ya Zanzibar na watendaji 17 wa Utamaduni kutoka Unguja. Lengo la kufanya ziara hizo katika maeneo ya kihistoria ni kushajiisha jamii kushiriki katika utalii wa ndani na kuendeleza utalii kwa wote. Aidha, idadi ya watalii wa ndani imefikia 4,222 na watalii wa nje imefikia 7,746 waliotembelea maeneo mbali mbali ya kihistoria hadi kufikia mwezi Machi 2016.

Mhe. Spika, katika kuyaendeleza majengo ya Makumbusho ili yatoe huduma na elimu stahiki kwa jamii, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imekamilisha maonesho 3 ya sanaa za mikono za Kizanzibari yenye kuonesha umahiri na ufundi mkubwa wa kiasili unaotokana na wasanii wa Kizanzibari

pamoja na vifaa vya maonesho hayo. Aidha, katika kuunga mkono tamasha la utamaduni la Mzanzibari, Idara ilifanikisha maonesho ya ala za muziki na historia za wasanii wa Zanzibar kwa ufanisi mkubwa sana. Katika kuadhimisha siku ya Makumbusho duniani Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ilifanikisha maonesho juu ya magonjwa yasiopewa kipaumbele kama minyoo, matende na kichocho. Maonesho yote hayo yalifanyika katika Makumbusho ya Mnazi Mmoja kwa vipindi tofauti na kuhudhuriwa na wanafunzi wengi kutoka Skuli ya Benbela na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (UDSM) wanaosomea masomo ya Urithi ambao walikuweko kwa kazi za vitendo pamoja na wageni kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,585,349,000 /= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 imefanikiwa kupata shilingi 905,434,380/= sawa na asilimia 57 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 290,812,000 /= hadi kufikia Machi 2016 jumla ya shilingi 79,344,258 zimekusanywa sawa na asilimia 27 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E bado kinaendelea kuonesha taarifa kwa kirefu).

Mhe. Spika, programu ndogo ya uendelezaji wa utalii na ukuzaji wa michezo inatekelezwa na Taasisi zifuatazo:- Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo na Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ).

Mhe. Spika, huduma zinazotolewa katika programu ndogo hii ni utoaji wa mafunzo ya utalii, ukarimu na ujasiriamali, uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo kupitia Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ).

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika kufanikisha huduma zake Chuo Cha Maendeleo ya Utalii kimefanikiwa kudahili wanafunzi wapya 243 sawa na asilimia 95 kwa mafunzo ya muda mrefu wakiwemo Cheti 174, Stashahada 69 na mafunzo ya muda mfupi 53 sawa na asilimia 63.8. Kuimarisha shughuli za taaluma ikiwemo ubora wa mitihani, kuongeza vipindi vya mafunzo ya vitendo *(Practical session)*, kuchapisha na kutunuku vyeti vya wahitimu 181 kwa ngazi za Cheti na Stashahada.

Mhe. Spika, katika kuhamasisha wanafunzi wanaohitimu ili kuweza kujiajiri wenyewe, wanafunzi 7 wameweza kujiajiri, mwanafunzi 1 kafungua mkahawa

wake na wanafunzi 6 wamejipanga kuendesha mradi wa ICT. Aidha, ziara 18 za kimasomo zimefanyika hapa Unguja kwenye vivutio vya utalii na mahoteli ambapo wanafunzi wanaangalia vifaa vinavyotumika katika fani zao na ziara 1 imefanyika kwenye mbuga za wanyama Mikumi - Tanzania Bara.

Mhe. Spika, katika kuendeleza na kukuza shughuli za michezo kitaifa na kimataifa Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imeziwezesha timu za taifa kushiriki katika mashindano ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Kombe la Mapinduzi *(Mapinduzi Cup),* Mashindano ya Klabu Bingwa Barani Afrika, Kombe la Chalenji na Mashindano ya *'Base ball'* Tanzania Bara. Vile vile Kamisheni imeimarisha miundombinu ya Uwanja wa Amaan kwa kutengeneza miundombinu ya maji, paa la VIP, mfumo wa kurushia matokeo ya mechi mbali mbali *(Score board system)* kwa kubadilisha mfumo wa Kichina uliopo mwanzo na kuweka mfumo wa Kiingereza na kujenga uzio wa matofali kwa lengo la kudhibiti wahalifu na wanaoharibu miundombinu ya kiwanja. Pia Kamisheni imeweza kujenga kiwanja cha michezo mchanganyiko kilichopo katika Wilaya ya Wete ili kuongeza idadi ya viwanja vya michezo nchini.

Mhe. Spika, Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kusaidia vyama na vilabu kushiriki katika mashindano 10 ya kitaifa na kimataifa vikiwemo Chama cha *Squash,* Chama cha Baskeli, Chama cha Mpira wa Wavu, Chama cha '*Golf*' kushiriki mashindano ya Nyerere *Master* Dar- es- Salaam, Chama cha Mchezo wa Karata, Chama cha Mchezo wa Judo kushriki mashindano 10 ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Burundi. Katika mashindano hayo Timu ya Mchezo wa Judo imefanikiwa kupata vikombe 2, medali 2 za dhahabu, medali 2 za fedha na medali 3 za shaba. Pia Baraza limesaidia Timu ya Mpira wa Ufukweni *(Beach Soccer)* kushiriki mashindano ya kimataifa ya *'Malindi International Beach Soccer Tournament'* yaliyofanyika mwezi wa Disemba, 2015 Mombasa Kenya.

Mhe. Spika, katika kuendeleza michezo kwa watu wenye ulemavu, Baraza limewezesha Chama cha Michezo ya Watu wenye Ulemavu wa Akili kuendesha mafunzo ya makocha wa michezo hiyo. Aidha, viongozi na waamuzi wa Chama cha Mchezo wa Kuogelea wameshiriki mashindano ya taifa ya kuogelea pamoja na kushiriki kikao cha uteuzi wa timu ya taifa ya Tanzania. Pia Baraza limefanya upimaji wa viwanja vidogo vidogo vya michezo katika maeneo ya Maisara na Miembeni (Matumbaku).

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 889,720,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2016 imefanikiwa kupata shilingi 378,339,450/= sawa na

asilimia 43 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 454,000,000/= na hadi kufikia Machi 2016 jumla ya shilingi 255,962,595/= zimekusanywa sawa na asilimia 56 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E kinaweza kuonesha hali hiyo).

Programu ya 3: Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii

Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii kwa kuongeza ajira kwa jamii, idadi ya watalii na tathmini yao. Programu hii inayotekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili Zanzibar itambulike zaidi kuwa ni miongoni mwa vituo bora vya utalii duniani.

Mhe. Spika, huduma inayotarajiwa kutolewa ni kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika kuimarisha Sekta ya Utalii, hasa kwa kuzingatia ushindani mkubwa uliopo katika sekta hii, Serikali kupitia Programu Jumuishi ya Maendeleo ya Utalii (Maabara ya Utalii) inaendelea kufanya mapitio tovuti ya utalii ili iweze kusaidia zaidi kusambaza taarifa muhimu zinazohusu bidhaa za utalii zilizopo Zanzibar. Kupitia tovuti hiyo Kamisheni ya Utalii itawasiliana moja kwa moja na wageni wanaopenda kuja kutembea Zanzibar kwa njia za kisasa ikiwemo ukurasa wa *'facebook na twitter'*. Aidha, jumla ya nakala 7,000 za majarida ya utangazaji zilichapishwa kwa ajili ya kutoa taarifa sahihi za utalii kwa mujibu wa soko husika. Kwa kushirikiana na ofisi za balozi za Tanzania, Kamisheni ya Utalii inaendelea kusambaza majarida katika masoko mbali mbali yakiwemo masoko ya Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, India na China. Pia Kamisheni imefanikiwa kushiriki katika onesho la kimataifa la '*DERTIORISTIK'* liliofanyika nchini Ujerumani na onesho la kitalii la '*Swahili Expo*' lililofanyika mjini Dar-es-Salaam.

Mhe. Spika, kwa madhumuni ya kuongeza wigo wa masoko ya utalii, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na wadau wa utalii ilifanikisha safari mpya za ndege za utalii kutoka nchini Ukraine na Poland kuja Zanzibar. Mbali ya ndege hizo, Kamisheni ya Utalii imetilia mkazo zaidi katika kuyafikia masoko ya utalii ya China, India, Urusi na Israel bila kuathiri harakati zetu za kujitangaza katika masoko yetu ya zamani ikiwemo Italy, Ujerumani, Uingereza na Ufaransa. Takwimu zinaonesha kuwa wageni kutoka katika

masoko mapya ya Urusi, India, China na Israel imeongezeka kutoka 22,106 mwaka 2014 hadi kufikia 29,070 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 39.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii imeiwezesha ofisi ya utangazaji utalii iliyopo nchini India kufanya kazi za utangazaji kikamilifu kwa kuipatia vielelezo vya utangazaji na kulipa gharama za uendeshaji. Ofisi hii imetoa mchango mkubwa wa kuitangaza Zanzibar nchini India katika Mji wa Mumbai. Kupitia ofisi hii Zanzibar ilifanikiwa kuwashawishi waandaaji wa misafara ya watalii kutoka India kuja Zanzibar kujionea hali halisi ya bidhaa za Utalii na baadae kuijumuisha Zanzibar katika orodha za nchi watakazopeleka watalii. Aidha, ofisi hii iko katika matayarisho ya kuleta watu mashuhuri kutoka India wakiwemo waandaji wa filamu mashuhuri. Lengo ni kuyashajiisha makampuni ya filamu kutoka India kufanya shughuli zake hapa Zanzibar. Mbinu kama hizi zimekuwa zikitumika na nchi nyingi za visiwa na kusaidia sana kuongeza idadi ya wageni katika nchi husika.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 304,500,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2016 imefanikiwa kupata shilingi 36,784,800/= sawa na asilimia 12.

Programu ya 4: Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuwa na mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii inayotekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Mipango na Sera, yenye jukumu la kuratibu na kuendeleza utalii pamoja na kujenga uwezo na mazingira mazuri kwa kazi kwa wafanyakazi wa Kamisheni.

Mhe. Spika, huduma ambazo zinazotarajiwa kutolewa ni uratibu na uendelezaji wa utalii na kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi wa Kamisheni.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali wamefanya utafiti wa siku za ukaazi kwa wageni na matokeo yanaonesha kuwa wastani wa siku za ukaazi kwa mgeni zimeongezeka kutoka 7.7 mwaka 2014 hadi kufikia 8.5 mwaka 2015. Ni dhahiri kuwa mafanikio haya yanakwenda sambamba na ongezeko la matumizi ya mgeni kwa siku.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaielewa Sekta ya Utalii na wanashiriki kikamilifu katika shughuli za utalii, Kamisheni ya Utalii imeandaa na kurusha jumla ya vipindi 39 kupitia vyombo vya habari vya Redio na Televisheni vyenye lengo la kuelimisha wananchi juu ya fursa zilizopo katika Sekta ya Utalii ili waweze kunufaika na fursa hizo. Hivi sasa Kamisheni ipo katika hatua za mwisho za kutengeneza Mpango Mkakati wa Mawasiliano katika Sekta ya Utalii ambao utaweka mfumo imara wa mawasiliano baina ya wadau wa utalii. Tunaamini utekelezaji wa Mpango huu utasaidia sana wananchi kupata taarifa kuhusu Sekta ya Utalii katika maeneo yao.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii imetoa mafunzo kwa waongozaji wa watalii na vikundi vya kinamama vinavyojishughulisha na uzalishaji wa mazao ya baharini ambayo hutengeneza bidhaa na kuziuza kwa watalii. Kamisheni ya Utalii iliandaa ziara maalum kwa waandaaji wa misafara ya wageni katika vivutio vipya vya utalii vinavyoratibiwa na jumuiya ya kinamama katika kijiji cha Fumba na Bweleo kwa madhumuni ya kuzitafutia soko bidhaa hizo.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii ina jukumu la kusimamia ubora wa huduma katika Sekta ya Utalii. Kwa msingi huo jumla ya miradi 150 ilifanyiwa ukaguzi kwa madhumuni ya kuangalia ubora wa huduma zinazotolewa katika miradi kwa wageni wetu.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa mazingira ya kufanyia kazi yanaimarishwa ili kuongeza ufanisi katika kazi, Kamisheni ya Utalii imewalipia gharama za mafunzo wafanyakazi wake 5 ambao wanasoma katika vyuo vya ndani katika fani za Uhasibu, Utalii, Sheria na Utawala. Pia imeipatia ofisi vifaa vya kufanyia kazi pamoja na kulifanyia ukarabati jengo la Makao Makuu ya Kamisheni.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 921,400,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2016 imefanikiwa kupata shilingi 558,289,200/= sawa na asilimia 60.5 na kutakiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,656,951,000/= na hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya shilingi 1,538,802,646 zimekusanywa sawa na asilimia 93 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E kinaweza kikatumika).

Programu ya 5: Uendeshaji na Mipango Katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika wizara. Programu hii imeundwa na programu ndogo tatu, programu ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya wizara na kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, programu ndogo ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

Mhe. Spika, huduma zinazotolewa katika programu ndogo hii ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika kusimamia majukumu yake ya kiutendaji Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanya ziara za kikazi katika taasisi ziliopo chini ya Wizara za Pemba na Dar es Saalam kwa ajili ya kuelewa utendaji kazi na kuelewa changamoto ambazo zimejitokeza. Aidha, idara imeimarisha mashirikiano na wadau wa ndani na nje ya wizara kwa viongozi na watendaji kushiriki makongamano, mikutano na warsha tofauti nchini China na Comoro.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 28 katika ngazi na fani tofauti wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ikiwemo ngazi ya Shahada ya Pili wafanyakazi 6, Shahada ya Kwanza wafanyakazi 10, Stashahada wafanyakazi 9 na Cheti wafanyakazi 3 ambapo mafunzo hayo yana lengo la kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 2).

Mhe. Spika, idara katika kuimarisha mazingira mazuri ya kazi imeweza kuzipatia ofisi zake vitendea kazi na vifaa mbali mbali kwa ajili ya kufanya kazi kwa ufanisi vikiwemo kompyuta 5, skana 1, samani, vifaa vya kuandikia na vifaa vya usafi. Aidha, Kitengo cha Ukaguzi wa Fedha za Ndani kimetayarisha ripoti 2 za fedha na ukaguzi kwa lengo la kuhakiki matumizi sahihi ya fedha. Pia Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kimetayarisha Mpango wa

Utekelezaji wa Manunuzi wa mwaka pamoja na Mpango wa Matumizi ya Fedha.

Mhe. Spika, Vikao vya Kamati ya Uongozi wa Wizara vimefanyika kwa ajili ya kujadili nyaraka kuu za wizara zikiwemo Sera ya Utalii, Sera ya Michezo, na Waraka wa kuanzishwa *channel* ya *ZBC* 2.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,370,153,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2016 imefanikiwa kupata shilingi 793,490,800/= sawa na asilimia 58 (Tafadhali angalia kiambatanisho nambari 1D).

Mhe. Spika, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini mipango, sera, tafiti na miradi ya maendeleo ya wizara.

Mhe. Spika, huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera, tafiti, kuandaa na kuwasilisha bajeti ya Wizara na mipango na miradi ya maendeleo.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika kukamilisha Sera ya Michezo ya mwaka 2016 inayopendekezwa, **i**dara ipo katika hatua za kuwasilisha Rasimu ya Sera hiyo katika kikao cha Makatibu Wakuu kwa ajili ya kujadiliwa. Aidha, katika kuhakikisha kwamba baada ya kupitishwa sera hiyo inatekelezwa kikamilifu, idara imetayarisha Rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Ssra hiyo ambao kwa sasa unajadiliwa na wataalamu wa Wizara. Mkakati huo unatarajiwa kuwasilishwa kwa wadau wakuu wa utekelezaji wa Sera ya Michezo 2016 inayopendekezwa ili wapate kujadili na kutoa michango yao katika kujiandaa na utekelezaji.

Mhe. Spika, idara kupitia Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini imetembelea na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na wizara ikiwemo mradi wa kufanya matengenezo kiwanja cha michezo cha Mao tse Tung kilichopo Kikwajuni, mradi wa kutengeneza njia ya kukimbilia katika uwanja wa Gombani Pemba, mradi wa uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria uliopo eneo la Kuumbi na mradi wa ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari hapo Kilimani. Lengo ni kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Mhe. Spika, idara imeandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za wizara pamoja na miradi ya maendeleo ambayo inawasilishwa Tume ya Mipango katika Kitengo cha Miradi na Ufuatiliaji na Tathmini, Mpango kazi na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 120,305,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2016 imefanikiwa kupata shilingi 15,500,000/= sawa na asilimia 13 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D).

Mhe. Spika, programu ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera, tafiti na mipango mikuu ya wizara - Pemba, kuratibu miradi ya maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 7 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi tofauti ikiwemo Cheti 3, Stashahada 2 na Shahada 2 ambapo mafunzo hayo yana lengo la kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku.

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba imekagua na kutathmini maeneo ya kihistoria ili kujua hali halisi ya maeneo hayo ambapo 20 kati ya maeneo 48 yanahitaji matengenezo pamoja na kuwekea mbao za maelezo. Lengo la kufanya tathmini hiyo ni kuimarisha na kutangaza maeneo hayo ili yaweze kutumika kwa utalii wa ndani na nje pamoja na kukuza pato la nchi.

Mhe. Spika, katika kufanya Uwanja wa Gombani Pemba kuwa wa kisasa na wenye hadhi ya Kimataifa, Ofisi Kuu Pemba ipo katika harakati za kuweka raba (*tartan*) katika njia ya kukimbilia ya kiwanja hicho. Kazi iliyokamilika hadi sasa ni kuweka jamvi (*base*) ya kuwekea raba (*tartan*), kununua vifaa vikiwemo raba na lami pamoja na kumlipa Mshauri Mwelekezi anaefanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,038,920,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2016 imefanikiwa kupata shilingi 504,503,850/= sawa na asilimia 49 (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D).

MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2016/2017

Mhe. Spika, wizara imejipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya dijitali na ununuzi wa ving'amuzi;
ii. Kuimarisha Makumbusho ya Pete Unguja;
iii. Kukamilisha Sera ya Michezo na kujenga viwanja vitatu vya Michezo vya Wilaya na;
iv. Kutangaza Sekta ya Utalii ndani na nje ya nchi kwa kutumia njia za kisasa zenye tija.

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imepangiwa jumla ya shilingi 16,281,900,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 9,684,400,000/= kwa matumizi ya kawaida na shilingi 6,597,500,000/= kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, katika fedha za miradi ya maendeleo shilingi 600,000,000/= kwa Mradi wa Maabara ya Utalii, shilingi 400,000,000/= ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na shilingi 5,597,500,000 ni ruzuku kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ujenzi wa Uwanja wa Mao tse Tung (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F).

KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (*PROGRAMM BASED BUDGET - PBB*) KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 serikali ilifanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma. Mageuzi hayo ni kutoka mfumo wa bajeti unaotumia vifungu (*line item*) kwenda katika mfumo unaotumia programu (*PBB*). Mfumo huo unategemewa kuleta uwiano mzuri wa Mipango ya Taifa katika bajeti pamoja na kuweka uwazi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa jamii.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo itatumia jumla ya shilingi 16,281,900,000/= kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano ambazo ni:-

1. Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji (Shilingi 3,660,795,000/=).
2. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo (Shilingi 8,162,637,000/=).
3. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii (Shilingi 208,505,000/=).
4. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii (Shilingi 904, 395,000/=).
5. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Shilingi 3,345,568,000/=) (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1G, 1H na 1I).

Programu ya 1: Maendeleo ya Habari na Utangazaji (shilingi 3,660,795,000)

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa na jamii iliyoimarika katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia habari. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni wananchi kupata na kutumia habari zenye kiwango bora kabisa. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 3,660,795,000/= na imepangiwa kusimamia programu ndogo kuu mbili:-

- Upatikanaji na Usambazaji wa Habari (Shilingi 3,441,651,000/=) na;
- Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji (Shilingi 219,144,000/=).

Mhe. Spika, katika programu ndogo ya upatikanaji na usambazaji wa habari inatekelezwa na Taasisi tofauti nazo ni, Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*), Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Chuo cha Uandishi wa Habari na Kampuni ya Usambazaji Maudhui (*ZMUX*), jukumu la msingi katika Programu ndogo hii ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha jamii, kuratibu uchapishaji wa matangazo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kutoa mafunzo ya taaluma ya uandishi wa habari na mawasiliano. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni urushaji wa vipindi kupitia TV na Redio, utoaji wa taarifa picha, makala, filamu na sinema, utoaji wa magazeti, utoaji wa mafunzo ya habari na mawasiliano na usambazaji wa maudhui ya utangazaji.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi

3,441,651,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya Shilingi 1,535,000,000/=.

Mhe. Spika, programu ndogo ya pili ni usimamizi wa vyombo vya habari na utangazaji ambayo inatekelezwa na Taasisi zifuatazo: Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji Zanzibar na jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini ili kwenda sambamba na Sheria ya Habari na Utangazaji. Huduma ambayo inatarajiwa kutolewa ni udhibiti na usimamizi wa shughuli za habari na utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 219,144,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya shilingi 100,000,000/=.

Programu ya 2: Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo (shilingi 8,162,637,000).

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa utamaduni wa Zanzibar unawaendeleza wasanii kiuchumi na kupunguza umasikini pamoja na kuwa na rasilimali watu yenye ujuzi na ustadi wa kukuza utalii nchini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii yetu. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa, uhifadhi wa utamaduni, kukuza utalii kupitia rasilimali watu yenye ujuzi na ustadi na kutoa ajira kwa jamii kupitia michezo. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 8,162,637,000/= na itakuwa na programu ndogo 2.

- Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria (shilingi 1,508,943,000/=) na;

- Uendelezaji wa Rasilimali Watu katika Utalii na Ukuzaji wa Michezo (shilingi 6,653,694,000/=).

Mhe. Spika, programu ndogo ya uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:

Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili, na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kusimamia, kuratibu, kuimarisha, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za utamaduni Zanzibar.

Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, kurikodi kazi za sanaa kupitia studio ya filamu na muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi fasaha ya Kiswahili, uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria, uelimishaji na ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na urithi wa utamaduni.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naiomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,508,943,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya shilingi 392,268,000/=.

Mhe. Spika, programu ndogo ya uendelezaji wa utalii na ukuzaji wa michezo inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:

Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo na Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ). Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kutoa taaluma ya utalii itakayowezesha kuijenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa pamoja na kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa nchini. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni utoaji wa mafunzo ya utalii, ukarimu na ujasiriamali, uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo kupitia Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ).

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kufanya kazi zake katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 656,194,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 5,997,500,000/= kwa mradi wa maendeleo na makusanyo ya shilingi 530,000,000/=.

Programu ya 3: Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii (shilingi 208,505,000/=).

Mhe. Spika, programu hii inayotekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili kuleta tija kwa maslahi ya Taifa.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii kwa kuongeza ajira kwa jamii, idadi ya watalii na thamani yao. Aidha matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuifanya Zanzibar kuwa Kituo Bora cha Utalii chenye kukidhi mahitaji ya jamii na watalii. Huduma inayotarajiwa kutolewa ni kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 208,505,000/= kwa kazi za kawaida, na makusanyo ya shilingi 2,000,000,000/=.

Programu ya 4: Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii (shilingi 904, 395,000/=).

Mhe. Spika, programu hii inayotekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Mipango na Sera, yenye jukumu la kuratibu na uendelezaji wa utalii pamoja na kuwajenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi wa Kamisheni.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuwa na mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa será na mipango ya utalii. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuwepo kwa utalii endelevu na wenye kuhimili ushindani. Huduma ambazo zinazotarajiwa kutolewa ni uratibu na uendelezaji wa utalii na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 904, 395,000/= kwa kazi za kawaida.

Programu ya 5: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa mipango bora iliyosimamiwa na kutekelezwa na usimamizi na uendashaji wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 3,345,568,000/= na itasimamia programu ndogo 3.

- Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Shilingi 1,645,735,000/=);

- Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara (shilingi 736,505,000/=) na;

- Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba (Shilingi 963,328,000/=).

Mhe. Spika, programu ndogo ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo itatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za utawala, utumishi, maendeleo, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa Wizara.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,643,735,000/= kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika**,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya Wizara ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kuratibu, kufuatialia na kutathmini mipango, sera, tafiti na miradi ya maendeleo ya Wizara.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuandaa na kuwasilisha bajeti na kuratibu mipango na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 136,505,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 1,000,000,000/= kwa utekelezaji wa Programu ya Maabara ya Utalii na mradi wa ujenzi wa uwanja wa Mao Tse Tung.

Mhe. Spika, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Pemba. Programu ndogo hii ni kiunganishi katika kuhakikisha majukumu, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni kusimamia na kuratibu shughuli za utawala, uendeshaji na mipango mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu - Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera, tafiti na mipango mikuu ya Wizara - Pemba, kuratibu miradi ya maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 963, 328,000/= kwa kazi za kawaida.

SHUKRANI

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalumu ziwaendee Mhe. Naibu Waziri Chumu Kombo Khamis, Katibu Mkuu Nd. Omar Hassan Omar, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Amina Ameir Issa, Makatibu Watendaji, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Wakuu wengine wa Taasisi za Wizara na wasaidizi wao wote kwa kufanya kazi kwa juhudi, maarifa, uadilifu na umakini mkubwa. Kwa kweli wamekuwa wakinisaidia sana kutekeleza majukumu yangu. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zetu na kunishauri kwa hekima na busara.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru wafanyakazi, wanamichezo, wasanii, washirika wa utalii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za Wizara yangu.

Mhe. Spika, pia shukurani za pekee ziende kwa Vyombo vya Habari vya Serikali na Binafsi kwa kufanikisha kurusha vipindi mbali mbali vikiwemo vya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015 na wa Marudio wa Machi, 2016 na kuelimisha jamii kuhusu kujikinga na maradhi ya Kipindupindu.

Mhe. Spika, nitakuwa si mwema kama sikuishukuru Wizara ya Fedha na Mipango pamoja Tume ya Mipango kwa ushirikiano mkubwa waliotupa kwa mahitaji ya fedha na ushauri.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nizishukuru nchi mbali mbali na Mashirika kadhaa ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali ya Misri, Serikali ya Japan, Serikali ya Ujerumani, Serikali ya Oman, Shirika la UNESCO na Shirika la Utangazaji la Ujerumani (DW) mashirika hayo tuliyoshirikiana nayo katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mhe. Spika, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi hususan Waheshimiwa Mawaziri ambao wamepata uteuzi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kusikiliza kwa utulivu na umakini mkubwa wakati wa kutoa bajeti hii.

Mhe. Spika, naliomba sasa Baraza lako Tukufu kujadili kwa kina matumizi ya Wizara yangu ya jumla ya shilingi 16,281,900,000. Kati ya fedha hizo shilingi 9,684,400,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 6,597,500,000/= kwa kazi za maendeleo. Katika fedha za miradi ya maendeleo, Shilingi 5,997,500,000/= zitatumika kwa utekelezaji wa ujenzi wa uwanja wa Mao Tse Tung ambapo shilingi 5,597,500,000/= ni ruzuku kutoka Serikali ya Jamhuri ya watu wa China na shilingi 400,000,000/= ni mchango wa Serikali. Aidha, katika fedha za kazi za maendeleo shilingi 600,000,000/= ni kwa utekelezaji wa Programu ya Maabara ya Utalii. Pia naliomba Baraza lako liidhinishe makusanyo ya mapato ya shilingi 2,547,268,000/= kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na makusanyo ya shilingi 2,010,000,000/= ambazo hukusanywa na taasisi zilizoruhusiwa kutumia makusanyo hayo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za taasisi hizo. Mhe. Waziri wa Fedha kaa mkao wa kula.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sasa nawaomba wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie katika Ramadhani hii tukufu na katika kumi hili la rehema bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

VIAMBATISHO
KIAMBATISHO NAMBA 1 A
FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2015 HADI MACHI 2016 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA
TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2015/2016	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI -MACHI 2015/2016	ASILIMIA
1	Ofisi Kuu Pemba	Mishahara	433,900,000	321,207,850	74%
		Matumizi Mengineyo	749,001,000	183,296,000	24%
	JUMLA		**1,182,901,000**	**504,503,850**	**43%**
	Idara ya	Mishahara	-	-	

2	Mipango, Sera na Utafiti	Matumizi Mengineyo	120,305,000	15,500,000	13%
	JUMLA		**120,305,000**	**15,500,000**	**13%**
3	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Mishahara	756,000,000	620,275,800	82%
		Matumizi Mengineyo	614,153,000	173,215,000	28%
	JUMLA		**1,370,153,000**	**793,490,800**	**58%**
4	Idara ya Habari Maelezo	Mishahara	210,900,000	150,910,650	72%
		Matumizi Mengineyo	114,358,000	31,300,000	27%
	JUMLA		**325,258,000**	**182,210,650**	**56%**
5	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	Mishahara	589,000,000	414,619,080	70%
		Matumizi Mengineyo	460,601,000	99,472,000	22%
	JUMLA		**1,049,601,000**	**514,091,080**	**49%**
6	Idara ya Makumbusho na Mambo ya kale	Mishahara	431,900,000	306,043,300	71%
		Matumizi Mengineyo	234,282,000	37,500,000	16%
	JUMLA		**666,182,000**	**343,543,300**	**52%**
7	Kamisheni ya Utalii	Mishahara	594,300,000	428,203,700	72%
		Matumizi Mengineyo	631,600,000	170,000,000	27%
	JUMLA		**1,225,900,000**	**598,203,700**	**49%**
	JUMLA YA MISHAHARA		**3,016,000,000**	**2,241,260,380**	**74%**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO		**2,924,300,000**	**710,283,000**	**24%**
	JUMLA KUU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU		**5,940,300,000**	**2,951,543,380**	**50%**

TAASISI ZA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2015/2016	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI -MACHI 2015/2016	ASILIMIA
1	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mishahara	1,405,000,000	1,129,528,350	80%
		Matumizi Mengineyo	431,000,000	114,953,420	27%
	JUMLA		**1,836,000,000**	**1,244,481,770**	**68%**
2	Shirika la Magazeti ya Serikali	Mishahara	311,000,000	184,408,700	59%
		Matumizi Mengineyo	249,610,000	233,769,600	94%
	JUMLA		**560,610,000**	**418,178,300**	**75%**
3	Chuo cha Uandishi wa Habari	Mishahara	270,000,000	187,081,800	69%
		Matumizi Mengineyo	52,490,000	16,000,000	30%
	JUMLA		**322,490,000**	**203,081,800**	**63%**
4	Tume ya Utangazaji	Mishahara	165,000,000	118,555,550	72%
		Matumizi Mengineyo	55,000,000	14,000,000	25%
	JUMLA		**220,000,000**	**132,555,550**	**60%**
5	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	Mishahara	320,000,000	261,139,450	82%
		Matumizi Mengineyo	49,000,000	32,000,000	65%
	JUMLA		**369,000,000**	**293,139,450**	**79%**
6	Baraza la Kiswahili	Mishahara	-		
		Matumizi Mengineyo	40,800,000	10,800,000	26%
	JUMLA		**40,800,000**	**10,800,000**	**26%**

7	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	Mishahara	56,000,000		
		Matumizi Mengineyo	90,000,000	37,000,000	41%
	JUMLA		**146,000,000**	**37,000,000**	**25%**
8	Baraza la Michezo	Mishahara	-		
		Matumizi Mengineyo	90,000,000	48,000,000	53%
	JUMLA		**90,000,000**	**48,000,000**	**53%**
9	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	Mishahara	120,000,000		
		Matumizi Mengineyo	427,000,000	73,200,000	17%
	JUMLA		**547,000,000**	**73,200,000**	**13%**
	JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU		**2,647,000,000**	**1,880,713,850**	**71%**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA RUZUKU		**1,484,900,000**	**579,723,020**	**39%**
	JUMLA KUU YA RUZUKU		**4,131,900,000**	**2,460,436,870**	**60%**
	JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA		**5,663,000,000**	**4,121,974,230**	**73%**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA WIZARA		**4,409,200,000**	**1,290,006,020**	**29%**

	JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA) A		**10,072,200,000**	**5,411,980,250**	**54%**
MIRADI YA MAENDELEO					
1	Maabara ya Utalii		2,500,000,000	-	
2	Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung		480,000,000	-	
	JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO) B		**2,980,000,000**		
	JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)		**13,052,200,000**	**5,411,980,250**	**41%**

KIAMBATISHO NAMBA 1B
MAPATO YALITOKUSANYWA JULAI 2015 HADI MACHI 2016
MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

NO.	TAASISI	BAJETI	MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI MACHI 2015/16	ASILIMIA
1	Idara ya Habari Maelezo	38,000,000	17,330,000	46%
2	Tume ya Utangazaji	65,000,000	17,550,000	27%
3	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	230,000,000	73,239,758	32%

4	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	20,812,000	4,305,000	21%
5	Baraza la Kiswahili	40,000,000	1,799,500	4%
6	Kamisheni ya Utalii	1,656,951,000	1,538,806,646	93%
	JUMLA	**1,984,282,000**	**1,590,195,558**	**80%**

KIAMBATISHO NAMBA 1C
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA

NO.	TAASISI	BAJETI 2015/2016	MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI HADI MACHI 2016	ASILIMIA
1	Chuo cha Uandishi wa Habari	150,000,000	108,801,000	73%
2	Chuo cha Maendeleo ya Utaliii	454,000,000	255,962,595	56%
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	500,000,000	269,205,820	54%
4	Shirika la Utangazaji (ZBC)	350,000,000	310,530,709	89%
5	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	140,000,000	57,096,000	41%
	JUMLA	**1,594,000,000**	**1,001,596,124**	**63%**

KIAMBATISHO NAMBA 1D
FEDHA ILIYOPATIKA JULAI 2015 HADI MACHI 2016 KWA KILA PROGRAMU NDOGO
Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
1	Shirika la Utangazaji Zanzibar	1,836,000,000	1,244,481,770	68%
2	Idara ya Habari Maelezo	355,753,000	182,210,650	51%
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	560,610,000	418,178,300	75%
4	Chuo cha Uandishi wa Habari	322,490,000	203,081,800	63%
5	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	547,000,000	73,200,000	13%
	JUMLA	**3,621,853,000**	**2,121,152,520**	**59%**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utanagzaji

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Tume ya Utangazaji Zanzibar	220,000,000	132,555,550	60%
	JUMLA	**220,000,000**	**132,555,550**	**60%**

Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
1	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	735,000,000	514,091,080	70%
2	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	90,000,000	37,000,000	41%
3	Baraza la Kiswahili	40,800,000	10,800,000	26%
4	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	719,549,000	343,543,300	48%
	JUMLA	**1,585,349,000**	**905,434,380**	**57%**

Programu ndogo ya Uendelezaji wa Utalii na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
1	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	369,000,000	293,139,450	79%
2	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	430,720,000	37,200,000	9%
3	Baraza la Michezo	90,000,000	48,000,000	53%
	JUMLA	**889,720,000**	**378,339,450**	**43%**
1	Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung	480,000,000	-	0%
	JUMLA KUU	**1,369,720,000**	**378,339,450**	**28%**

Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Kamisheni ya Utalii	304,500,000	36,784,800	12%
	JUMLA	**304,500,000**	**36,784,800**	**12%**

Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Kamisheni ya Utalii	921,400,000	558,289,200	60%
	JUMLA	**921,400,000**	**558,289,200**	**60%**

Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Habari, Utamaduini, Utalii na Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
1	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,370,153,000	793,490,800	58%
	JUMLA	**1,370,153,000**	**793,490,800**	**58%**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	120,305,000	15,500,000	13%
	JUMLA	**120,305,000**	**15,500,000**	**13%**

	Mradi wa Maabara ya Utalii	2,500,000,000	-	0%
	JUMLA KUU	**2,620,305,000**	**15,500,000**	**1%**

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Ofisi Kuu Pemba	1,038,920,000	504,503,850	49%
	JUMLA	**1,038,920,000**	**504,503,850**	**49%**

KIAMBATISHO NAMBA 1E
FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2015 HADI MACHI 2016 KWA KILA PROGRAMU NDOGO
Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
1.	Shirika la Utangazaji Zanzibar	350,000,000	310,530,709	89%
2	Idara ya Habari Maelezo	38,000,000	17,330,000	46%
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	500,000,000	269,205,820	54%
4	Chuo cha Uandishi wa Habari	150,000,000	108,801,000	73%
5	Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX)	140,000,000	57,096,000	41%
	JUMLA	**1,178,000,000**	**762,963,529**	**65%**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Tume ya Utangazaji Zanzibar	65,000,000	17,550,000	27%
	JUMLA	**65,000,000**	**17,550,000**	**27%**

Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
1	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	20,812,000	4,305,000	21%
2	Baraza la Kiswahili	40,000,000	1,799,500	4%
3	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	230,000,000	73,239,758	32%
	JUMLA	**290,812,000**	**79,344,258**	**27%**

Programu ndogo ya Uendelezaji wa Utalii na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	454,000,000	255,962,595	56%
	JUMLA	**454,000,000**	**255,962,595**	**56%**

Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2015 HADI MACHI 2016	ASILIMIA
	Kamisheni ya Utalii	1656,951,000	1,538,806,646	93%
	JUMLA	**1656,951,000**	**1,538,806,646**	**93%**

KIAMBATISHO NAMBA 1F
BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017
TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2016/2017
1	Ofisi Kuu Pemba	Mishahara	428,539,000
		Matumizi Mengineyo	534,789,000
	JUMLA		**963,328,000**
2	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	136,505,000
	JUMLA		**136,505,000**
3	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Mishahara	1,050,682,000
		Matumizi Mengineyo	595,053,000
	JUMLA		**1,645,735,000**
4	Idara ya Habari Maelezo	Mishahara	208,219,000
		Matumizi Mengineyo	112,170,000
	JUMLA		**320,389,000**

5	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	Mishahara	618,519,000
		Matumizi Mengineyo	290,201,000
	JUMLA		**908,720,000**
6	Idara ya Makumbusho na Mambo ya kale	Mishahara	418,941,000
		Matumizi Mengineyo	219,282,000
	JUMLA		**638,223,000**
7	Kamisheni ya Utalii	Mishahara	576,100,000
		Matumizi Mengineyo	536,800,000
	JUMLA		**1,112,900,000**
	JUMLA YA MISHAHARA		**3,301,000,000**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO		**2,424,800,000**
	JUMLA KUU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU		**5,725,800,000**

TAASISI ZA RUZUKU

NO.	TAASISI	MAELEZO	BAJETI 2016/2017
1	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mishahara	1,463,327,000
		Matumizi Mengineyo	392,000,000
	JUMLA		**1,855,327,000**
2	Shirika la Magazeti ya Serikali	Mishahara	287,592,000
		Matumizi Mengineyo	238,000,000
	JUMLA		**525,592,000**

3	Chuo cha Uandishi wa Habari	Mishahara	278,343,000
		Matumizi Mengineyo	56,000,000
	JUMLA		**334,343,000**
4	Tume ya Utangazaji	Mishahara	163,144,000
		Matumizi Mengineyo	56,000,000
	JUMLA		**219,144,000**
5	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	Mishahara	366,194,000
		Matumizi Mengineyo	42,000,000
	JUMLA		**408,194,000**
6	Baraza la Kiswahili	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	42,000,000
	JUMLA		**42,000,000**
7	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	84,000,000
	JUMLA		**84,000,000**
8	Baraza la Michezo	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	84,000,000
	JUMLA		**84,000,000**
9	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	Mishahara	-
		Matumizi Mengineyo	406,000,000
	JUMLA		**406,000,000**

	JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU		**2,558,600,000**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA RUZUKU		**1,400,000,000**
	JUMLA KUU YA RUZUKU		**3,958,600,000**
	JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA		**5,859,600,000**
	JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA WIZARA		**3,824,800,000**
	JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA) A		**9,684,400,000**
MIRADI YA MAENDELEO			
1	Maabara ya Utalii		600,000,000
2	Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung SMZ		400,000,000
	Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung CHINA		5,597,500,000
	JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO) B		**6,597,500,000**
	JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)		**16,281,900,000**

KIAMBATISHO NAMBA 1G
BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KWA KILA PROGRAMU NDOGO
Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
1	Shirika la Utangazaji Zanzibar	1,855,327,000	500,000,000

2	Idara ya Habari Maelezo	320,389,000	55,000,000
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	525,592,000	550,000,000
4	Chuo cha Uandishi wa Habari	334,343,000	200,000,000
5	Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX)	406,000,000	230,000,000
	JUMLA	**3,441,651,000**	**1,535,000,000**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
	Tume ya Utangazaji Zanzibar	219,144,000	100,000,000
	JUMLA	**219,144,000**	**100,000,000**

Programu ndogo ya Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
1	Kamisheni ya Utamaduni	744,720,000	-
2	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	84,000,000	120,000,000
3	Baraza la Kiswahili	42,000,000	22,268,000
4	Idara ya Makumbusho	638,223,000	250,000,000
	JUMLA	**1,508,943,000**	**392,268,000**

Programu ndogo ya Uendelezaji wa Utalii na Ukuzaji wa Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
1	Chuo cha Maendeleo ya Utalii	408,194,000	530,000,000
2	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	164,000,000	-
3	Baraza la Michezo	84,000,000	-
4	Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung (CHINA)	5,597,500,000	-
5	Ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung (SMZ)	400,000,000	-
	JUMLA	**6,653,694,000**	**530,000,000**

Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
	Kamisheni ya Utalii	**208,505,000**	**-**
	JUMLA	**208,505,000**	**-**

Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
	Kamisheni ya Utalii	**904,395,000**	**2,000,000,000**
	JUMLA	**904,395,000**	**2,000,000,000**

Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,645,735,000	-
	JUMLA	**1,645,735,000**	-

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
1	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	136,505,000	-
2	Mradi wa Maabara ya Utalii Zanzibar	600,000,000	-
	JUMLA	**736,505,000**	- -

Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017 MATUMIZI	BAJETI 2016/2017 MAPATO
	Ofisi Kuu Pemba	963,328,000	-
	JUMLA	**963,328,000**	**-**

KIAMBATISHO NAMBA 1H
MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017
MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017
1	Idara ya Habari Maelezo	55,000,000
2	Tume ya Utangazaji	100,000,000
3.	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	250,000,000
4	Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni	120,000,000
5	Baraza la Kiswahili	22,268,000

	JUMLA NDOGO	**547,268,000**
	Kamisheni ya Utalii	2,000,000,000
	JUMLA NDOGO	**2,000,000,000**
	JUMLA	**2,547,268,000**

KIAMBATISHO NAMBA 1I
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA

NO.	TAASISI	BAJETI 2016/2017
1	Chuo cha Uandishi wa Habari	200,000,000
2	Chuo cha Maendeleo ya Utaliii	530,000,000
3	Shirika la Magazeti ya Serikali	550,000,000
4	Shirika la Utangazaji (ZBC)	500,000,000
5	Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)	230,000,000
	JUMLA	**2,010,000,000**

KIAMBATISHO NAMBA 2: WAFANYAKAZI WA WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO AMBAO WAMEKWENDA MASOMONI KWA MWAKA 2015/2016

NO.	JINA KAMILI.	JINSI	TAASISI	FANI	KIWANGO	MUDA	CHUO
1.	Nd.Dawa Kombo Makame.	Mke.	Uendeshaji na Utumishi.	Ugavi na Ununuzi.	Stashahada.	Miaka miwili.	ICPS.
2.	Nd. Mohammed Haji Bakari	Mme	Uendeshaji na Utumishi	Utunzaji Kumbukumbu	Stashahada.	Miaka miwili.	ICPS.

3.	Nd. Safia Ujudi Mchavu.	Mke.	Chuo cha Maendeleo ya Utalii.	Arts in Tourism and Society.	Shahada ya Pili.	Miaka miwili.	Chuo Kikuu Iringa.
4.	Nd. Fatma Moh'd Muhidin.	Mke.	Chuo cha Maendeleo ya Utalii.	Business Information Technology.	Shahada ya Kwanza.	Miaka mitatu.	Zanzibar University.
5.	Nd.Zaituni Mussa Ali.	Mke.	Chuo cha Maendeleo ya Utalii.	Tourism Mgt & Marketing.	Shahada ya Pili.	Mwaka	Chuo Kikuu cha Bourne mouth.
6.	Nd.Ilyasa Mzee Juma	Mke	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	Uongozi wa Rasilimali Watu	Cheti	Mwaka	Chuo cha Utawala wa Umma
7.	Nd. Ali Ussi Ally	Mme	Makumbusho na Mambo ya Kale	Heritage Management	Shahada ya Pili	Miaka miwili	Chuo Kikuu Dar-es-Salaam
8.	Nd. Mbaya Ali Abdalla.	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	Shahada ya Kwanza	Miaka mitatu	Chuo Kikuu Cha Mwalimu
9.	Nd. Asha Abass Khamis	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Tourism Management and Marketing	Shahada ya Kwanza	Miaka mitatu	SUZA
10.	Nd. Saida Mwinyi Hamza	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Katibu Muhutasi	Stashahada	Miaka miwili	IPA
11.	Nd. Salama Ahmada. Hija	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Teknolojia ya Habari na Biashara	Stashahada	Miaka miwili	IPA
12.	Nd. Fauzia Mzee Haji	Mke	Makumbusho na Mambo ya Kale	Teknolojia ya Habari Mawasiliano na Uhasibu	Stashahada	Miaka miwili	ZIToD

13.	Nd. Wanu Ali Makame	Mke	Shirika la Magazeti ya Serikali	Uchumi na Fedha	Shahada ya Pili	Miaka miwili	Zanzibar University
14.	Nd. Yussuf Ali Hassan	Mme	Shirika la Magazeti ya Serikali	Graphic Design and Web Development	Shahada ya Pili	Miaka miwili	India
15.	Nd. Kassim Khamis Jape	Mme	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Uhusiano wa Kimataifa	Shahada ya Pili	Miaka miwili	China
16.	Nd. Amina Omar Othman	Mke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Uandishi wa Habari	Stashahada	Miaka miwili	Royal College
17.	Nd. Juma Mbarouk	Mme	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Uandishi wa Habari	Stashahada	Miaka miwili	IJMZC
18.	Nd. Sada Said	Mke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Uandishi wa Habari	Shahada ya Kwanza	Mwaka	China
19.	Nd. Ali Haji Mwadini	Mme	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Uhusiano wa Kimataifa	Shahada ya Kwanza	Mwaka	China
20.	Nd. Nunu Mwalim Ngwali	Mke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Ugavi na Ununuzi	Stashahada	Mwaka	Chuo cha Fedha Chwaka
21.	Nd. Sheikha Seif Suleiman	Mke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Mawasiliano ya Umma na Uandishi wa Habari	Shahada ya Kwanza	Miaka miwili	Open University
22.	Nd. Salha Ameir Mwadini	Mke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Utunzaji Kumbukumbu	Cheti	Mwaka	Dar College

23.	Nd. Haji Khatib Haji	Mme	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Rasilimali Watu	Shahada ya Kwanza	Miaka miwili	College of Finance and Business
24.	Nd. Jitihada Abdalla Salim	Mke	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Uandishi wa Habari	Shahada ya Kwanza	Miaka mitatu	Open University
25.	Nd. Ramadhan Bakari Jabu	Mme	Shirika la Utangazaji (ZBC)	Accounting and Islamic Banking	Stashahada	Miaka miwili	ZIBRET
26.	Nd. Mohammed Walid Fikirini	Mme	Kamisheni ya Utalii	Tourism Mgt & Marketing.	Shahada ya Kwanza	Miaka mitatu	SUZA
27.	Nd. Fikirini Haiba Ali	Mme	Kamisheni ya Utalii	Cultural Anthropology & Tourism.	Shahada ya Kwanza	Miaka mitatu	Tumaini University Iringa
28.	Nd. Hamzia Khamis Khalfan	Mke	Ofisi Kuu Pemba	Rasimali Watu	Stashahada	Miaka miwili	ZABECS
29.	Nd. Mwajuma Hija Kipenda	Mke	Ofisi Kuu Pemba	Rasimali Watu	Stashahada	Miaka miwili	ZABECS
30.	Nd. Mauwa Khamis Juma	Mke	Ofisi Kuu Pemba	Rasimali Watu	Cheti	Mwaka	Utawala wa Umma (IPA)
31.	Nd. Haroub Ali Nassor	Mme	Ofisi Kuu Pemba	Teknolojia ya Habari	Cheti	Mwaka	Utawala wa Umma (IPA)
32.	Nd. Khalifa Rajab Hamad	Mme	Ofisi Kuu Pemba	Rasimali Watu	Cheti	Mwaka	Utawala wa Umma (IPA)

33.	Nd. Jamila Abdalla Salim	Mke	Ofisi Kuu Pemba	Uandishi wa Habari	Shahada ya Kwanza	Mia ka mita tu	Open University
34.	Nd. Suhaila Moh'd Iddi	Mke	Ofisi Kuu Pemba	Ugavi na Ununuzi	Shahada ya Kwanza	Mia ka Mita tu	Zanzibar University (Tunguu)

KIAMBATISHO NAMBA 3
KAZI ZA SANAA ZILIZOKAGULIWA NA BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI (BASSFU)

NO.	KAZI ZILIZOHAKIKIWA	ZILIZO KUBALI KA	ZILIZO KATAL IWA	ZILIZOSA WAZISHA	IDADI
1.	Rasimu za michezo mbali mbali 15	13	-	2	15
2.	Mashairi ya nyimbo mchanganyiko 7	6	1	-	7
3.	Filamu mchanganyiko 46	35	-	11	46
4.	Tenzi zenye maudhui mbali mbali 6	5	-	-	5
5.	Michezo ya jukwaani 4	3	-	1	4
JUMLA		**67**	**1**	**14**	**77**

KIAMBATISHO NAMBA: 4
MASHINDANO MBALI MBALI AMBAYO TIMU ZA ZANZIBAR ZILISHIRIKI MWAKA 2015/2016

S/NO.	CHAMA	MASHINDANO	PAHALA	MAELEZO
1.	Chama cha Netiboli	Mashindano ya ligi kuu ya Zanzibar	Zanzibar, November, 2015	Mshindi wa kwanza ni JKU na mshindi wa 2 ni timu ya mafunzo

2.		Mashindano ya Klabu Bingwa ya Tanzania	Zanzibar, November, 2015	Timu ya Uhamiaji ya T/Bara ilipata ushindi wa kwanza, JKT Mbweni Mshindi wa pili na JKU mshindi wa 3.
3.	Chama cha Mchezo wa Kuogelea	Mashindano ya Klabu Bingwa ya Muungano	Zanzibar, Machi, 2016	KMKM walipata ushindi wa 4 jumla kwa kupata medali 1 ya fedha na 3 za shaba.
4.	Chama cha Squash	Mashindano ya Zanzibar Cup, 2015	April, 2015	Mchezaji Saleh Juma alipata nafasi ya kwanza.
.		Mashindano ya Kombe la Muungano	Zanzibar, Mei, 2016	Mashindano yalifanyika lakini timu za nje ya Zanzibar hazikushiriki (tatizo la kiwanja).
5.	Chama cha JUDO	Mashindano ya 10 ya Afrika Mashariki	Burundi, Febuari, 2016	Timu ya Zanzibar ilipata ushindi wa 3 kwa kupata medali 2 za dhahabu, 1 fedha na 3 za shaba.
6.	Chama cha Riadha	Mashindano ya Afrika Mashariki na kati ya vijana chini ya umri wa miaka 18	Dar es salaam April, 2016	Timu ya Zanzibar imefanikiwa kupata ushindi wan ne jumla kwa kupata Medali 2 za dhahabu,

				Medali 1 ya Fedha na Medali 4 za Shaba.
7.	Chama cha Mpira wa Miguu	Mashindano ya Kombe la Challenge	Ethiopia, Novemba, 2016	Timu ya Zanzibar ilitolewa katika hatua ya robo fainali
		mashindano ya Kimataifa ya mpira wa ufukweni "Malindi International Beach Soccer Tournament"	Mombasa-Kenya Disemba, 2015	Timu ya Zanzibar ilifanikiwa kupata ushindi wa tatu.
8.	Chama cha Baskeli	Mashindano ya Taifa ya Baskeli mashindano ya kuchagua wachezaji kumi watakaoshiriki katika mashindano ya Taifa	Zanzibar, Novemba, 2014	Vilabu mbali mbali vilishiriki
9.	Chama cha mchezo wa Karata	Mashindano ya Klabu Bingwa ya mchezo wa Karata	Zanzibar, Septemba, 2015	Klabu ya Kichungwani Pemba ilipata ushindi wa kwanza na kuwa klabu bingwa kwa mchezo huo.
10.	Chama cha mchezo wa Golf	mashindano ya Nyerere "Nyerere Masters"	Dar es salaam, Novemba, 2015	Timu ya Zanzibar haikufanya vizuri katika mashindano hayo

11.	Chama cha mchezo wa Bao	Mashindano ya Klabu Bingwa ya mchezo wa Bao	Zanzibar, Septemba, 2015	Klabu ya Mwembe ladu ilipata ushindi wa kwanza na kuwa klabu bingwa kwa mchezo huo.

KIAMBATANISHO NAMBA: 5
MAFUNZO MBALI MBALI KWA VYAMA VYA MICHEZO

S.NO.	CHAMA	MAFUNZO	PAHALA	MAELEZO
1.	Chama cha mchezo wa Tennis	Mafunzo ya Utawala	Nairobi - Kenya, Januari,2016	Kiongozi 1 alishiriki
2.	Chama cha Mpira wa miguu	Mafunzo ya ukocha	Zanzibar, April, 2016	Jumla ya makocha 48 kutoka Unguja na 92 kutoka walishiriki mafunzo hayo.
3.	Chama cha mchezo kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa akili (SOZ)	Mafunzo ya Ukocha	Zanzibar, April, 2015	Jumla ya Makocha 22 wa Zanzibar walishiriki mafunzo hayo.
4.	Chama cha mchezo wa Judo	Mafunzo ya Sports massage	Zanzibar, Sept,205	Vyama mbali mbali vya michezo vilishiriki mafunzo hayo.
5.	Chama cha mpira wa wavu	Mafunzo ya ualimu wa michezo	Dar es salaa., April, 2016	Vijana 3 wameshiriki mafunzo hayo.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, kwa uwasilishaji wako mzuri sana siku ya mwanzo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, na mimi naungana na Waheshimiwa ambao wamekupongeza mpaka umefika kukaa na mimi nikupongeze vile vile.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hapo atakaefuatia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, lakini kabla sijamwita naomba nitoe tangazo moja tu la wageni ambao wamefika hapa mbele yetu. Wageni waliopo ni wageni wa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, Muwakilishi wa Wawakilishi, Jimbo la Chukwani, ni wasanii wa filamu za kizazi kipya, jumla yao ni sita wanaongozwa na Meneja wao Khamis Ali maarufu kama ni (*Good Father*). Ahsanteni sana, karibuni sana muone jinsi tunavyofanya shughuli hizi kwa niaba ya wananchi. Baada ya hapo sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaj na Habari ili kutoa maoni ya kamati. (*Makofi*)

Mhe. Maryam Thani Juma (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, ahsante sana kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) ambae ameweza kutufikisha hapa tukiwa wazima na hasa ikiwa leo ni siku ya mwanzo ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. *(Makofi)*

Pili napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Gando kwa kuweza kunichagua nikafika hapa na leo niko mbele ya Baraza hili kuwasilisha maoni ya kamati hii ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, kwa biaba ya Mwenyekiti wa Kamati hii napenda kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka 2016/2017 kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kuendelea kuturuzuku neema ya uhai na uzima na kutuwezesha kukutana kwa mara ya kwanza kwa Baraza hili la Tisa la Wawakilishi kwenye Mkutano huu wa Bajeti ambao ni mkutano wa mwanzo wa bajeti kwa Baraza hili la Tisa.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa niaba ya

kamati yangu kusoma maoni ya Kamati kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba pia kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa imani kubwa mliyopewa na Wajumbe wa chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi wa Zanzibar kuwa viongozi wa kuwaongoza. Ni imani ya kamati yangu na Wajumbe wote wa Baraza kwamba mutatimiza matarajio ya wajumbe waliowachagua kuwa viongozi wao ndani ya chombo hiki cha kutunga sheria.

Mhe. Spika, pongezi za kipekee kabisa naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Gando kwa imani yao kubwa waliyonionesha kwa kuniteua na kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mwakilishi wao ndani ya chombo hiki cha kutunga Sheria hapa Zanzibar. Ahadi yangu kwao ni kuwaambia kwamba tutafanya kazi kwa pamoja na mashirikiano ya hali ya juu kuhakikisha tunaleta maendeleo si kwa jimbo letu tu bali kwa nchi nzima.

Mhe. Spika, nitakuwa mchache wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa imani yao kwa kumchagua Mwenyekiti wa Kamati hii. Napenda kutumia fursa hii adhimu kuwaahidi kuwa tutafanya kazi kwa mashirikiano ya hali ya juu, na kamwe sitawaangusha!

Mhe. Spika, vile vile naomba pia kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano mazuri waliyotupatia wakati wa upitiaji wa bajeti ya wizara hii.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilipata fursa ya kulifikiria na kulifanyia uchambuzi fungu la makadirio ya bajeti ya wizara hii.

Mhe. Spika, kwa muktadha huo nachukua fursa hii kukuarifu kuwa kazi hiyo tuliifanya na leo hii tupo hapa kwa ajili ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, taarifa ya kazi tuliyoifanya kama Kanuni ya 94(9) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012 inavyoelekeza.

Mhe. Spika baada ya utangulizi huo napenda sasa kuwataja Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ili muweze kuwatambua kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Mwenyekiti
2. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Mjumbe
4. Mhe. Maryam Thani Juma - Mjumbe
5. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Mjumbe
6. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Mjumbe
7. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
8. Mhe. Mussa Foum Mussa - Mjumbe
9. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
10. Ndg. Latifa Saleh Suleiman - Katibu
11. Ndg. Makame Salim Ali - Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo napenda sasa nitoe Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama ifuatavyo:-

SEKTA YA HABARI

Mhe. Spika, vyombo vya habari vina umuhimu mkubwa katika kuhamasisha shughuli za maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa pamoja na kupanua uhuru na haki ya wananchi ya kupata taarifa mbali mbali zinazoihusu jamii yao na ulimwengu kwa ujumla.

Katika kufanikisha lengo hilo jema la serikali, wizara imejipangia Programu Maalum ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji. Progaramu hii ina lengo la kuhakikisha upatikanaji wa habari na usambazaji pamoja na usimamizi wa vyombo vya habari na utangazaji.

Mhe. Spika, licha ya kuwa upatikanaji wa habari ni haki ya msingi ya wananchi lakini bado kuna maeneo mengi katika nchi yetu hasa kisiwa cha Pemba hazipatikani huduma za habari kwa uhakika. Matangazo yamekuwa yanakatika mara kwa mara na kupelekea kukosekana kwa haki hii ya msingi kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika ikumbukwe kuwa *ZBC* ndio mdomo wa serikali na sauti yake kwa wananchi, kusuasua huku kwa matangazo haya kwa mfumo wa sasa unaotumia ving'amuzi utasababisha sauti ya serikali kutosikika kwa wananchi ipasavyo. Hivyo Kamati inaishauri *ZBC* kujitathmini wenyewe kama bado ina uhalali wa kupokea ruzuku kutoka serikalini wakati huduma zake bado haziridhishi.

Aidha, Kamati haioni sababu wala haja kwa sasa chini ya mfumo tulionao wa matangazo na ubora wa vipindi vyetu kufikiria kuanzisha chaneli ya *ZBC 2* wakati hii moja iliyopo hali yake hohe hahe. Matangazo hayaridhishi, maslahi ya watumishi bado madogo na hata mafunzo yenyewe ni kwa tabu kupatikana.

Mhe. Spika, kuongeza kwa *channel* nyengine maana yake ni kuongeza mahitaji ya ruzuku kutoka serikalini, kuongeza idadi ya watumishi, gharama za uendeshaji n.k na ndiyo maana hatuoni sababu ya kufikiria kwenda huko, na badala yake ni kuiimarisha hiyo moja iliyopo ili iweze kutoa huduma za kuridhisha si kwa serikali tu bali pia kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Spika, lengo la serikali wakati inalianzisha Shirika hili la *ZBC* ni kulipa ruzuku mwanzoni ili baadae liweze kujiendesha wenyewe kwa kujitegemea. Hivyo ni wazi kuwa suala la ukusanyaji wa mapato nalo ni muhimu. Bado kuna utamaduni uliojengeka kwa taasisi nyingi za serikali kutolipia matangazo yao pamoja na shughuli zao mbali mbali.

Mhe. Spika, suala hili lisipoangaliwa kwa ukaribu na umakini zaidi litalifanya shirika hili kuwa tegemezi maisha, na kutofikia lengo la kuanzishwa kwake, kamati inahofia mwenendo huu unaweza hata kuliua shirika kabisa. Hivyo, kamati yangu inatoa wito kwa taasisi zote za serikali kulipia huduma zote wanazopatiwa na *ZBC* ikiwemo matangazo yao ili yale malengo mazuri ya serikali ya kuanzisha shirika hili yaweze kufikiwa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kwenye Sekta hii ya Habari, kamati tunaishauri wizara kuangalia upya suala la malipo ya wafanyakazi wa *ZBC* kwani deni hili ni la muda mrefu. Hivyo ni vyema likamalizwa kabla ya mwaka huu wa fedha haujamaliza.

Aidha, kwa upande wa wafanyakazi wa sehemu ya Ofisi ya Gazeti la Zanzibar Leo, ni vyema mazingira yao ya kazi yakaimarishwa, hasa kutokana na ukweli kwamba eneo wanalofanyia kazi haliendani na vigezo vya matakwa ya vigezo vya usalama kazini. Eneo lao ni dogo lakini ni chumba ambacho hata madirisha hakina.

SEKTA YA UTALII

Mhe. Spika, sote tunaelewa kuwa utalii ni sekta mama inayochangia pato la nchi yetu hasa baada ya kupungua kwa thamani ya zao la karafuu kwenye soko la dunia.Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watalii wanaoitembelea Zanzibar imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka watalii 132,836 (laki moja na

thalathini na mbili elfu mia nane na thalathini na sita**)** mwaka 2010 hadi kufikia watalii 311,891 (laki tatu kumi na moja alfu mia nane na tisini na moja) mwaka 2014.

Hata hivyo, sote tunaelewa kuwa Sekta ya Utalii inategemea sekta mbali mbali kuimarika kwake ili iweze kukua na kujitangaza wenyewe. Miongoni mwa sekta hizo ni barabara, maji, huduma mbali mbali ikiwemo za kifedha na mawasiliano, miundombinu ya umeme na umeme wa uhakika, ulinzi na usalama, amani na utulivu, mazingira mazuri na kadhalika.

Mambo yote hayo kufanikiwa kwake na kuwa katika hali ya kuridhisha ni kivutio tosha na kishajihisho cha kuutangaza utalii wetu na nchi kwa ujumla. Kwa mintarafu hiyo basi, serikali haina budi kutambua na kufanyia kazi kwa vitendo uimarishaji wa miundombinu ambayo ndiyo kichocheo kikubwa cha kuutangaza utalii wetu.

Mhe. Spika, kamati inaelewa kwamba serikali imeanzisha kitu kinachoitwa "Maabara ya Utalii" kikiwa na dhamira ya kuimarisha utalii wetu na kuongeza thamani ya watalii wanaokuja kuitembelea Zanzibar kuwa wa daraja la juu.

Licha ya dhamira nzuri ya serikali kwa kuanzisha maabara hiyo ya utalii, lakini kwa bahati mbaya sana kwa mwaka unaoishia Juni 30, 2016 hadi Kamati inapokea taarifa kulikuwa hakuna hata shilingi moja iliyoingizwa kwa kutekeleza kazi hiyo. Kamati inaelewa hali ya fedha kwa mwaka uliopita ilivyokuwa na changamoto zote ambazo nchi ilikumbana nazo, lakini inahofia hali hii kujitokeza tena kwenye bajeti ya mwaka huu na kusababisha kurudisha nyuma juhudi za kuimarisha na kuendeleza utalii Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa upande wa kuutangaza Utalii wetu kama waswahili wanavyosema: *"Biashara itangazwayo ndiyo itokayo"*. Tunapenda kutoa wito kwa serikali kuzidi kuitangaza nchi yetu nje hasa kwa kutumia njia za kisasa badala ya kutumia njia za kizamani ambazo matokeo yake siyo mazuri sana.

Aidha, kamati haijaridhishwa hata kidogo kwa fedha zilizotengwa kwa bajeti ya mwaka jana kwa ajili ya kuutangaza utalii wetu kupatikana shilingi 32,822,800 (thalathini na mbili milioni laki nane ishirini na mbili alfu na mia nane) hadi Machi 2016 ambazo ni sawa na asilimia 10.7 ya fedha zote. Kibaya zaidi mwaka huu ikapunguzwa kutoka shilingi 304,500,000 (shilingi mia tatu na nne milioni na laki tano) za mwaka jana hadi kufikia shilingi 208,505,000 (shilingi mia mbili na nane milioni na laki tano na alfu tano) kwa mwaka huu

kitu ambacho kwa kuutangaza utalii kwa mwaka hasa nje ya nchi ni fedha kidogo sana.

SEKTA YA UTAMADUNI

Mhe. Spika, Utamaduni ni nyenzo muhimu katika kulinda historia yetu, kudumisha mapenzi baina yetu, umoja, mila, desturi na silka njema katika jamii. Hivyo ni vyema juhudi maalum zikaelekezwa katika kulinda na kuyahifadhi maeneo yetu ya kihistoria ikiwemo makumbusho ili tuweze kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kulinda na kuhifadhi utamaduni wetu wa Kizanzibari.

SEKTA YA MICHEZO

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba michezo sio afya tu bali ni ajira duniani. Michezo mbali mbali iliyokuwa ikitajikana Zanzibar sasa imekuwa kama inakufa kabisa au inakosa ladha ile iliyokuwepo kipindi cha zamani.

Licha ya kuongezeka kwa idadi ya wapenda michezo na wachezaji wa Kizanzibari wanaocheza ligi za nje ya Zanzibar, lakini bado maendeleo ya michezo kwa ndani yamekuwa ni ya kusuasua sana. Mhe. Spika hali hii inachangiwa sana na migogoro ndani ya vyama vyenyewe vya michezo, kukosekana kwa ufadhili, upungufu wa wataalamu wenye ujuzi na mbinu za kisasa, miundombinu ya viwanja vya michezo na hata mtizamo wa wananchi kwenye suala la michezo, pia migogoro ndani ya *ZFA* ambayo kwa namna moja au nyengine inarudisha nyuma maendeleo ya Michezo Zanzibar, kwani muda mwingi *ZFA* inakuwa kwenye kutafuta suluhisho la matatizo yake na si kuendeleza michezo nchini.

Mhe. Spika, ni imani ya kamati kuwa kupitia Programu maalumu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo changamoto zote hapo juu zitaweza kugeuzwa na kuwa "changabaridi", ili michezo iwe haiimarishi afya tu za watu wetu bali ni chimbuko la ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, kwa mnasaba wa suala la ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse- Tung, kamati inaipongeza serikali kwa hatua iliyofikiwa ya kutafuta mfadhili wa ujenzi wa uwanja wa Mao Tse-Tung ambapo Serikali ya China itachangia asilimia kubwa ya ujenzi huo na SMZ kuchangia shilingi milioni mia sita katika kufanikisha ujenzi huo.

Licha ya hatua hiyo iliyofikiwa, kamati inatahadharisha juu ya usalama wa eneo husika kwa sasa, kwani eneo haliko vizuri na ni hatari kwa wananchi hasa

waendeshao vyombo vya moto. Hivyo, kamati inatoa wito kwa wizara na serikali kwa ujumla kuchukua hatua zozote za dharura kunusuru maafa yasiyotarajiwa katika eneo la Mao.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 wizara imepanga kutekeleza programu kuu tano (5) ambazo ni Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji, Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo, Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii, Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii, na ya mwisho ni Programu ya Uendeshaji na Mipango katika sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Kwa kuwa utekelezaji wa programu zote hizi unafuata mfumo wa kibajeti wa *PBB*, licha ya changamoto zilizojitokeza kwenye mwaka wa mwanzo wa utekelezaji wa bajeti chini ya mfumo huu mpya, ni imani ya kamati yangu kuwa kwa mwaka huu utekelezaji wa bajeti utakuwa wa mafanikio makubwa na kuongeza ufanisi kwenye utendaji wa serikali.

Mhe. Spika, kamati yangu inaamini kuwa kufanikiwa kwa programu hizi ambazo zimo ndani ya fungu la wizara ambalo limeombewa jumla ya Shilingi 15,169,000,000 (Kumi na Tano Bilioni, na Mia Moja na Sitini na Tisa Milioni) kwa kazi za kawaida pamoja na kazi za Maendeleo.

Mhe. Spika, kuimarika kwa Sekta ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kutawasaidia wananchi katika kuimarisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa ujumla hasa katika nyanja za kiuchumi. Hivyo, kamati yangu inaliomba Baraza lako tukufu kwa kauli moja kuidhinisha fedha zote zilizoombwa na wizara hii ili iweze kutekeleza vyema majukumu yake waliyojipangia.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu hii naomba kwa mara nyengine na kwa umuhimu wa kipekee kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, kwa mashirikiano makubwa wakati wa kazi yetu ya mwanzo ya kupitia bajeti ya wizara hii.

Ni matumaini yangu kwamba mwanzo huu mzuri tutakwenda nao huo huo hadi tutakapomaliza muda wetu wa kuhudumia kamati hii kama kanuni zinavyoelekeza.

Mhe. Spika kwa kipekee kabisa naomba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii kwa kazi nzuri ya kuratibu kazi za kamati na kutuongoza vyema wakati wa upitiaji wa bajeti ya wizara hii.

Aidha, napenda vile vile kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kuwa watulivu na makini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Pia nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya kamati yangu ndani ya Baraza hili.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutamka kwamba, kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Gando kuwa naiunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.
Aidha, nawaomba wajumbe wote waichangie na kuiunga mkono Hotuba ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake na malengo waliyojipangia ipasavyo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Maryam Thani Juma, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Gando. Waheshimiwa Wajumbe sasa nitaanza kuwaita ili muanze kuichangia hii hoja na mchangiaji wetu wa mwanzo leo atakuwa Mhe. Suleiman Sarahan Said yeye aliomba tangu jana huyu, atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf na Mhe Dkt. Makame Ali Ussi ajiandae. Mhe. Suleiman Sarahan tafadhali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika salama na kuamka salama na Ramadhani yetu ya kwanza. Mwenyezi Mungu atujaali kila la kheri na baraka nyingi kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, na mimi kwanza niipongeze kamati hii ya habari kwa uono wake wa mambo mengi ambayo nimehisi kweli yanawakereketa katika maendeleo ya nchi yetu. Pia niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao na mambo yao mpaka kuifanya *ZBC* katika watu wanaonesha matangazo kufatiliwa kwa ukaribu vizuri sana ni umahiri wa Baraza la Wawakilishi hongereni sana Waheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Spka, mimi nataka nichangie kuhusu Wizara hii ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ni kwamba nafikiri kwa kipindi kirefu tunaichukuwa Wizara ya Habari kama michezo ya Mipira na kila kitu. Lakini nataka nioneshe umahiri wa taasisi hii katika kumbukumbu zangu za miaka yangu ya ujana niliona vita vya Iraq, Marekani na Uengereza ambavyo Waziri wa Habari alikuwa kwa wakati ule akiitwa kama sikosei El-Sahaf aliikamata nchi kwa

wiki mbili ikiwa hana silaha kwa mdomo wake tu akaimarisha nchi yake wakati wanajipanga kufanya mambo mengine.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Habari pamoja na kituo hiki cha Habari ni kitu muhimu sana na mimi naweza nikasema hii inaingia kwenye Afisi ya Rais kabisa kutokana na upeo wa mambo yake ni mambo makubwa sana ya afisi hii tusiyachukulie kijuu juu kuona tu michezo. Hii ni nchi na Habari ndio nchi. Kwa kweli naipongeza kwa sasa hivi hasa kwa serikali yetu tukufu kwa jinsi ilivyoipa kipaumbele Wizara hii ya Habari.

Mhe. Spika, mimi nataka niendelee na kuchangia. Mimi nasema kuhusu habari ya Viwanja vya Michezo takribani Zanzibar nzima kuna sekta mbili. Mimi nataka Waziri anambie kwamba vile ambavyo tayari viko serikalini au vinajulikana na Wizara ya Michezo ni vingapi ambavyo vimeshapimwa na viko katika hatua nzuri ambayo hata kama havijashughulikiwa. Lakini wananchi wana tabia ya kuvifata viwanja mpaka chini ya goli wakajenga nyumba. Viwanja vile baadae vinapoteza hadhi na inakuwa tabu kuja kumuondoa mtu.

Kwa hivyo, ningeshauri wizara ikatoa vipimo vya viwanja vile kwa sababu mtu akishakuja kumuondoa inakuwa tabu ya kisheria hilo ni la kwanza. Lakini na hapo hapo nikaongezea kwamba (A na B) ni kwamba kuna viwanja ambavyo tayari wananchi wanavitegemea katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba ambavyo tunaviita viwanja vya timu. Serikali huwa vinavitegemea viwanja vile kwa kiasi fulani ingawa vinakuwa haviko chini ya mamlaka yao.

Mimi ningeomba serikali viwanda vile wakavitambua na wakaviweka katika mipango maalum ya kuwasaidia wale ambao wanaviwanja vile maana wengine wanavunja timu wanauza kiwanja inajengwa nyumba. Viwanja vile Mheshimiwa ni muhimu visingetakiwa tena katika maeneo yakajengwa nyumba kama timu itagombana kiwanja kile kibakie ni mali ya serikali. Kwa sababu kinawahudumikia wananchi wengi na huwa kuna wananchi wengine wanataka kujumuika navyo.

Mhe. Spika, sasa niendelee kwenye Uwanja wa Gombani. Mhe. Spika, Uwanja wa Gombani ni uwanja ambao kwa kweli mimi naweza kusema kwa Tanzania hii na *East Africa* ni uwanja mmoja katika viwanja vikubwa ule ni uwanja na umejengwa kimahiri sana.

Mhe. Spika, kweli katika kisiwa chetu cha Pemba bado hatujawa na nguvu za kuweza kumiliki ule uwanja kwa kutegemea vianzo vya pale. Sasa ningeishauri hii wizara yetu ikatafuta mbinu katika uwanja ule ule kuna maeneo mengi huku

katika maeneo ya milango yake huku pembeni pembeni, ina maeneo mengi wakafanya jitihada za kuweka mageti kukodisha watu kama *store* na vitu vyengine kama inaweza au vitu vyengine au kufungua hata maofisi. Lakini pia ina sehemu za kumbi za mikutano.

Mhe. Spika, sijaona umuhimu sana uliofichika katika suala la kiwanja kile kama wanajitangaza kwamba tuna kumbi za mikutano na bei kidogo zikawa nafuu *facilities* zile zikawa nzuri zikaweza kuvuta angalau mapato kwa vile tunahitaji mapato zaidi. Uwanja ni mkubwa sana umegharimu mabilioni tusiuache tu tukauangalia. Ni lazima tutizame kwa hali na mali ule uwanja umegharimu kiasi gani tusiutupe, umekuwa kama ni uwanja wa serikali tu mwenye sherehe yake ya kiserikali ndio anafanya na ule unatakiwa ufanywe kibiashara.

Mimi ningeshari sana uwanja tunauombea kila siku umewekwa mataa. Uwanja ule sifikirii maana yake ule unatumia mita za LUKU nafikiri mita yake inatiwa labda milioni moja ndio uanze kutumika, sifikiria kama umewahi kutiwa milioni moja katika LUKU yake angalau zikawashwa taa. Watu wakaona tu ule uwanja kwa muda wa wiki, mbili, mwezi zina jaribiwa.

Kwa hivyo, itafika siku tutaka kuziwasha haziwaki tena itakuja kuwa kazi kweli kweli hasa nchi yetu ni nchi ya upepo wa chumvi mara nyingi zile zinaganda katika sehemu zake inakuwa ni tabu kuja kupata tena utaalamu wa kuja kuzifanyia kazi. Nishauri wizara ikajitajidi na Uwanja wa Gombani ndio uwanja wa pekee.

Mhe. Spika, si rahisi serikali kujenga uwanja kama ule ni kazi kweli kweli. Nimeona ile hulka yake ya mwazo ulikuwa na maji, ulikuwa na samaki mbele, maji yale hayapo na samaki wale wameshakufa ungerudishwa katika hadhi yake ile ya Gombani, ningeshauri hili, mengine ataendelea Mhe. Waziri rafiki yangu, tutakwenda kagua tuangalie nini cha kufanya.

Mhe. Spika, jengine niliangalia sisi hapa toka juzi watu wanapiga makofi mengi, wanafurahia sana mawaziri wameshikamana kama serikali moja hii, nawapongeza sana. Sasa nimeangalia utaratibu kama sikosei kuna nyumba ambazo kazijenga marehemu mzee Abeid Amani Karume yale Mahoteli yale ya Chake, Wete na Mkoani ambayo ndio ya mwanzo na sio majumba yale lakini zile ni hoteli.

Mhe. Naibu Spika, zile hoteli labda ile ya Chake Chake ndio naona imo katika *process* ya kuwa hai zile mbili zimekuwa ni nyumba za wala unga. Ni nyumba

za mambo mengi yanayofanyika katika vituo vile. Hazina ulinzi, hazitizamwi na ziko hali mbaya. Kama wizara Mheshimiwa imeshindwa hakuna haja apewe Mhe. Haji Omar Kheri ana vikosi vingi, ana mambo mengi atatengeza hoteli zitarudishwa na kama imeshindikana peleka Wizara ya Fedha ndio watu wanaohusika, lakini zishughulikiwe, zipo mijini, zinatia aibu! Mhe. Haji Omar Kheri amesema mara hii miji anataka kuirekebisha. Sasa zile hoteli ni aibu. Mhe. Spika, ningeshauri sana kwamba zile hoteli kama Serikali Kuu ziangalie pahali gani pa kupelekwa, zifanikiwe hata kama ni mapato yatarudishwa tena kwa kukodishwa.

Mhe. Spika, napenda kutilia mkazo tena serikali imejikita inataka kufanya Uwanja wa Mao Tse Tung kuwa uwanja tena wa kisasa unaorudi. Mhe. Spika, tumeshaona wakandarasi na mambo mengi na utafiti wa mambo, tunajenga vitu vikubwa sana na baadae vinakuwa na matatizo.

Mhe. Spika, uwanja ule nauhisi unakaribiana na uwanja wetu huu ambao uko Mnazi Mmoja katika mazingira yake ya ardhi.

Napenda kuishauri Wizara ya Habari kabla ya uwanja ule haujajengwa ukapoteza mamilioni ya pesa tukaja kucheza mle na maji ya goti. Ufanyiwe utafiti wa kutosha unajazwa, unapandishwa na unawekwa katika hadhi gani, tusije kuja pale mvua inanyesha asubuhi mpaka siku ya tano maji gotoni. Mheshimiwa tunakuwa hatujafanya ya maana, tunarudi nyuma baada ya kwenda mbele. Ningeshauri sana ufanyike utafiti wa hali na mali.

Mhe. Spika, nirudi kidogo kwenye *ZBC* Habari hapa imeshazungumzwa *ZBC* bado viwango vya *ZBC* havipo kwa umuhimu wake na ndicho chombo pekee kinachosema ukweli kwa Zanzibar kwa mambo yote na matukio yote. Vyengine vyote ni ubabaishaji wengine wanaongeza zao kwa uzoefu wao.

Mhe. Spika, hiki chombo kinaangaliwa na wengi na wengi wale wanaotaka usahihi na wanaotaka ukweli na uhakika lazima watizame *TBC*. Mhe. Spika, mimi nashangaa wakati wa mwaka kuanzia 1972 sijui kuendela mbele nilikuwa mdogo basi ilikuwa *TVZ* inaoenekana mpaka Kengeja, Mtambwe tena unafungua tu, ngoma hiyo. Leo sijui mnasema tuko kwenye *Digital*.

Mhe. Spika, hatuoni popote mpaka upate king'amuzi na king'amuzi chenyewe mashaka kwa nini hatutafuti mtambo wa nguvu hapa kamati imeshasema mnatafuta *ZBC* na pili mwende ya tatu wakati ya kwanza hatuiwezi hebu tuifanyieni ukarabati ukifungua tu *ZBC* kwanza ili tuone uhakika mnajiweza kutekeleza hilo. Pia tunataka umahiri wa wale wafanyakazi muwasomeshe,

hatuna ulazima wa kutafuta watu kutoka mbinguni wale wale wasomesheni watarudi katika viwango.

Mhe. Spika, vifaa Pemba tunaangalia matukio kwenye video kwamba unarushiwa kwenye *WhatsApp.* lakini *ZBC* haioneshi ukweli kama ni uongo unakuwa uongo na kama ni ukweli wameshindwa kuupinga. Kwa sababu hamna *camera* za kutosha.

Mimi Mheshimiwa niko pale zaidi. Mimi nakaa Pemba niko Chake Chake mji Mkuu pale. Mheshimiwa pale ndio kwenye Idara ya Habari yenyewe ukitaka matukio ya kila kitu unaambiwa *camera* moja amekwenda nayo waziri ya pili haipo. Mhe. Waziri mtu binafsi ana *camera* tano, ndani Idara ya Habari inashindwa kuwa na *camera* 10 Pemba. (*Makofi*)

Halafu ufatiliaji mna kigari kimoja ki- *escudo* ndio nakiona basi Mhe. Waziri basi vespa tano sita waandishi wa Habari wapeni hata kama wanaenda kuchukuwa maharusi ule muda hautokei matukio tutayapata kupitia *ZBC* ya kweli.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri sana mkawatafutia vifaa Unguja na Pemba sijasema kwa ajili ya Pemba lakini huku Pemba kumeoza. Wewe ukitaka chochote utafute mtu akakurikodie halafu huko kwengine anakwenda kufanya mambo mwenyewe atakutilia anayoyataka. *ZBC* tunaipenda, tunaihitaji tunashauri sana iwepo katika maelekezo zaidi.

Mhe. Spika, michezo naweza kusema ukiacha Afisi ya Rais na Tawala za Mikoa na nyengine na Mawasiliano na Wizara ya Elimu. Lakini michezo imo katika ajira kuwa kuisaidia serikali. Hakuna na sifikirii kama kuna wachezaji wa michezo au kuna watu wa michezo waliokuwa tunao rikodi ya kitaifa ambao angalau wanalipwa na sekta za kitaifa. Hatuna mtu anakwenda siku moja akirudi hapa anakaa kitako, hata akiomba pesa za kufanya mazoezi hamna. Sasa Mheshimiwa tutakwenda wapi kwenye suala la michezo.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri sana Wizara ya Habari irudi tena kujipanga, tusivamie mataifa kabla chini hatujajipanga. Itakuwa sie tunapeleka uwakilishi, tutakuwa kama tunakwenda kutia chamvi tu unapiga chamvi unarudi huna unachokifanya. Tungewaandaa watu wetu, tungeandaa mambo yetu, tungeandaa matamasha yetu hata hizo habari pamoja na utalii wangekuja.

Mhe. Spika, hajui "umundi, hajui kumbaya, hajui gonga, hajui jeuri sitaki, hatujui kelbu taabani" hatuji chochote. Lakini hajui kwa sababu bado

hatujaweka sawa haya mambo. Mimi ningeshauri vikundi vingi lakini maneno tutavishughulikia, utaratibu wake uko wapi?

Mimi ninacho kikundi kimoja pale cha Mkoani sijui kinaitwaje lakini hicho ndio kikundi kimoja kinakuja kwenye starehe, kinakwenda kwenye sherehe zote basi hamna kikundi chengine. Msewe mpaka ukakodi watoto wa skuli hakuna wengine, ng'ombe hamna.

Mhe. Spika, sasa enzi zilizokuwa za Sultani huko nyuma ng'ombe ilikuwa ikiheshimika.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Dah! Mheshimiwa niongeze kidogo nina mambo mengi na mimi natoka Pemba tena Mji Mkuu japo tano Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sawa najitahidi. Sasa huu mchezo wa ng'ombe ningeshauri iwe ndio sura yetu na dira yetu. Mtu hawezi kufuga ng'ombe yule ambaye, kwanza niwaambieni yule ng'ombe anakuwa *trained* kuna na ngoma yake ya umundi. Kuna kiumbizi, kuna kila kitu kama vile mnavyofanya *rehearsal*, sio unamchukua ng'ombe tu dume la gari ukalichukua halipigi, yule ng'ombe apewe *training* lazima ile sehemu ifanyiwe ukarabati wa kutosha. Yule ng'ombe anasikiliza mlio wa kirungu taa, taa, anajua sasa nikapige wapi.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba nataka kusema mambo ya kale. Mheshimiwa umenifurahisha umesema una maeneo karibu 48 mengine 20, lakini ningeshauri kama ikiwa muda utakuwa mdogo wa kunielezea nitafutie haya maeneo 48 nina mengine pengine huyajui. Kwa sababu kuna Kaburi la Mwana Mwari liko kule nikikuuliza liko wapi utasema hulijui, lakini sitaki niseme hayo. Mwana Mwari huyo alizikwa huko Ndagoni, aliyeshika mimba... sitaki niseme Ramadhani hii, lakini iko historia hatuijui. Kwa hivyo, ningesema tu hivyo.

Mhe. Spika, chengine sasa hivi tungekua zaidi kimichezo. Pemba hakuna mchezo wa ndani kama hivi tulivyofungiwa *indoor games* hamna jengo, ningeshauri atafute eneo tujenge *indoor games* michezo ya ndani ambayo haitaki upepo tuna michezo vingi ya vinyoya na mingine ile haitaki upepo inataka sehemu kama hizo tulizofungiwa hatujaamua jambo hilo Mheshimiwa, ningeshauri sana tuangalie.

Mhe. Spika, kuna sehemu moja ushabiki wa mpira Zanzibar umekufa angalau Bara sasa hivi Simba na Yanga ndio wamekamata hatamu, hata *Small Simba* na ni Katibu Mkuu wako ndiye aliyekuwa mchezaji mkubwa namjua Mheshimiwa wangu, lakini arudishe michezo...

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said:... ushabiki Mheshimiwa, nakumbuka tu hapa miaka kidogo ya 1990 pale mwanzo. Mheshimiwa naunga mkono hoja basi, sijamaliza lakini haya. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kama kawaida yangu kunijaalia uzima wa afya na vile vile nimshukuru kwa kuniwezesha kufika Ramadhani nyengine, ili kupata kufanya ibada na kusamehewa baadhi ya madhambi.

Vile vile niipongeze serikali nzima kwa utendaji wake mzuri wa kazi pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kupitisha hotuba yake vizuri, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mimi kwa kuwa muda ni mdogo nitakwenda moja kwa moja kwenye kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, nitatoa tu mchango wangu kwa elimu yangu ndogo niliyokuwanayo na vile vile baadae yatafuata maswali yangu ili aje anijibu.

Kwanza nitaanza kwenye suala la utalii. Utalii Mhe. Waziri, mgeni yeyote ni mfalme. Ikiwa mgeni wa ndani ya nchi au ikiwa mgeni wa nje ya nchi. Yeyote kwanza tufahamu mgeni ni mfalme. Na kumaanisha kwamba mgeni ni mfalme, maana yake ni kwamba mgeni anatakiwa apewe *services* nzuri asikereke ili mara ya pili aweze kuja tena ndani ya nchi yetu. Wageni mara nyingi, kwa nini nikatumia lugha hii ya kwamba mgeni ni mfalme. Anatoka safari refu na anapokuja nchini kwetu ina maanisha kwamba yeye kapenda kuja, kaona nchi nyingi duniani ambazo anaweza kwenda zaidi ya mia mbili au mia tatu, lakini akahisi aje Zanzibar. Sasa hicho kitu kimoja kwanza tukifahamu kwamba anakuja Zanzibar, inamaanisha kwamba kaipenda na kaona Zanzibar ni muhimu kwake kuja kutembea.

Lakini anapofika kuna vitu vingi vinavyomfanya yule mgeni baadae akereke mpaka tena inafika ya kwamba hataki hata kuja mara ya pili Zanzibar, kwa sababu tu pale atakapofika *airport*, usumbufu kwanza ule wa mabegi, mizigo, foleni ambayo huchukua muda mrefu. Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri,

akaweka wasaidizi maalum wa Wizara yake pale *airport*, kuhakikisha kwamba wanawasaidia wageni wale kwa njia yoyote ile. Ikiwa ameona kuna shida anapata kuwauliza na kuweza kusaidia kidogo na wakajitambulisha kama wao ni katika Wizara ya Utalii, wakasaidiwa wale wageni.

Vile vile, ningemuomba sana Mhe. Waziri, suala la Polisi. Wageni wanatoka huko wanatoka zao kutoka *airport* mpaka kufika mahotelini wanasimamishwa zaidi ya mara ya kumi au mara saba. Inategemea kuna sehemu kama atataka kutoka *airport* mpaka Kaskazini basi hakikisha kishapigwa mkono zaidi ya mara nane dereva yule ambaye amepakia wageni. Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, ungeshirikiana na Wizara husika ambazo zitaweza kustahi hawa wageni, kwa sababu mgeni kishatoka *airport* inamaanisha kwamba keshasachiwa hana tatizo na keshachoka. Ya nini kusimamishwa zaidi ya sehemu saba mpaka nane mpaka anafika kwenye hoteli. Ningeomba sana ungeshirikiana na Wizara husika ambazo inayoshughulikia na mambo ya Polisi, ukawashauri kuwa wale wageni wasipewe matatizo kama haya ya kusimamishwa kila wakati na kusachiwa au kusimamishwa simamishwa bila ya kazi maalum.

Vile vile, ningeenda kwenye suala la *airport*, hasa Mhe. Spika, ningeomba nimshauri tena Mhe.Waziri, kwamba angetengeneza kitabu maalum katika wizara yake ambacho hichi kitabu kiwepo *airport* na kiwepo bandari, kwa wale wageni wote wanaofika ndani ya *airport*. Kile kitabu kieleze kila kitu ndani; kieleze pesa yetu kwa Dola inakuwa Exchange *Rates* kiasi gani, Dola ya *pound* ni kiasi gani, *Euro* kiasi gani ili mgeni haja yeye ya kwamba hata kwenda kuuliza *Bureau de change,* lakini anakuwa ameshafahamu kubadilisha kuhusu *currency* yetu.

Vile vile, kwenye kitabu hicho angewaeleza ndani wale wageni, hii Zanzibar kwenye mambo ya utalii tuna vivutio vingapi; Mfano pana *Bay Island, Prisoner Island*, kuna sehemu za *history* ambazo azi-*mention* ndani ya kile kitabu pamoja na *map* ya *Stone Town* na *map* ya Zanzibar, ili mgeni anapofika pale basi kile kitabu kufunguliwe ofisi maalum pale ambayo wanunua wale wageni kwa Dola tano au kwa mtu ambaye wa *East Africa* kwa elfu kumi. Kuliko kwenda nje, mgeni anafika Zanzibar hata sehemu ya kwenda kutembea hajui aanzia wapi amalizie wapi. Mimi ningemshauri sana Mhe. Waziri, Mhe. Spika, hichi kitabu angelikitengeneza kwa kushirikiana na Wizara yake, kuhakikisha kwamba ndani ya kitabu kile kila kitu ndani kinaeleza nini Unguja na Pemba na anaweza kufaidika mgeni yule kwa kwenda kuangalia, kutembea au kwa matumizi ambayo ya *shopping* na vitu vyengine vya mambo ya utalii.

Mhe. Spika, vile vile, ningemshauri Mhe. Waziri, atengeneze taasisi zake binafsi zitakazoweza kumsaidia yeye pamoja na wizara yake. Hizi nimezitunga mimi lakini ninampa kama mfano. Angetengeneza kitu *CFIB.* Hichi ninaweza kumtafsiria kidogo tu. Maana yake nimekitunga sasa hivi baada ya kupata kitabu chake. Hii ni *Chamber of Foreign Investors Board (CFIB).* Maana yake kwamba atakapotengeneza Bodi hii au taasisi hii ya wale wageni wote walioko Zanzibar ma-*investors*, angejaribu kuwaita.

Halafu vile vile angetengeneza nyengine *Chamber of Local Investor Board (CLIB).* Hii vile vile akaitengeneza taasisi hii ikampa mashiriano mazuri na matatizo mengi ambayo yanatokeze ndani ya mahoteli, ndani ya uchumi wa utalii katika mazingira tofauti kwenye nchi yetu. Kila baada ya muda akawa anawaita hawa wanashirikiana kumtatulia matatizo na vile vile, yeye akawasikiliza na wao wakamsikiliza Waziri wakashirikiana. Mimi ningemuomba sana Mhe. Spika, angetengeneza kitu kama hichi, kwa sababu hivi sasa matatizo mengi yanatokezea katika mahoteli, katika sehemu za ma-*investors* kwenye sehemu zao walizo-*invest*. Lakini wanapata tabu wale wageni wengine hawajui waanze wapi waende wapi.

Mhe. Spika, atakapokuwa Mhe. Waziri, kaitengeneza hii na kawaita siku moja, yaani kaiandaa na kaiunda basi yeye itampa yeye urahisi zaidi kwenye kushirikiana na wageni bila ya matatizo. Halafu kutakapokuwa na matatizo, yule kiongozi wa Bodi ile anakuwa anaenda kumpa habari Mhe.Waziri, kwenye kikundi chetu cha *foreign investors* kuna tatizo fulani, fulani na changamoto yetu ni hii. Mhe. Waziri, kwake yeye itakuwa wepesi sana katika kutatua. Mhe. Spika, kwa kukata muda lakini atakapotaka maelezo zaidi Mhe. Waziri, nipo tayari wakati wowote kushirikiana naye kwenye kusaidiana na suala hili. (*Makofi*)

Vile vile, Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri, kuitangaza nchi. Nchi yetu ya Zanzibar ni maarufu sana duniani lakini naamini kuna nchi anazijua tunazo zamani kama alivyosema *Italy* na nchi nyengine kama *UK*, Oman ni nchi ambazo zamani tunazo historia nazo na tuna umaarufu nazo kwenye wageni. Lakini kuna nchi mpya ambazo zimetajwa vile vile kama Urusi, Ukraine, China. China si mpya, China yetu, ni ndugu zetu, lakini hizi mpya, kweli zinaleta wageni, lakini je, wizara yake imeshawahi kufika huko kwenye hizo nchi kwenda kujitangaza au wamejitangaza kwa kupeleka maombi tu.

Mhe. Spika, mimi ningemuomba Mhe. Waziri, ikiwezekana hata yeye mwenyewe na baadhi ya watendaji wake *personally* wakenda baadhi ya nchi kama hizo, wakenda ili kujitangaza na kuonana hasa na ma-*investors* wa

mambo ya mahoteli na wale wenye *tours operators* kubwa kubwa ili kuitangaza nchi. Vile vile, Mhe. Spika, utangazaji wa nchi upo katika aina tofauti. Kuna mfano kama haya mambo ya *world cup*. Tushajua *world cup* itakuwa Brazil, itakayofuatia itakuwa *Qatar, world cup* itakayofuatia itakuwa Urusi, kwa nini Mhe. Waziri, asiweze kwenda kushiriki. Kwa sababu tunapozungumza *world cup* ni dunia nzima pale inakwenda. Akatafuta kisehemu wizara yake ikakodi kwa niaba ya Zanzibar, ikatangazwa katika sehemu kama zile. Zile sehemu zina wageni dunia nzima wanafika pale. (*Makofi*)

Na katika mzunguko kama ule Mhe. Spika, yanakuwepo maduka madogo madogo mengi ya aina ile, wangekwenda wakakodi hata kwa bei kubwa madhali ni muda wa wiki mbili au mwezi mzima inatosha kwa kutangaza. Wakenda kama nchi hizo *Qatar* inayofanya *world cup*, Urusi ina *world cup*, Brazil ina *world cup*. Ni sehemu za kutangaza vile vile kwa njia ya michezo, kwa njia ya utalii na kwa njia nyengine ambazo zinazoweza Zanzibar ikavutia. Vile vile, tuna *Expo 2020* Dubai. Ni karibu sana hata tiketi zake ni rahisi, wangekwenda. Kuna mambo mengine tusingojee lazima kwamba labda maonesho haya yawe ya utalii ndiyo uwende. Wewe ukiona maonesho yoyote yenye watu wengi, watu wamekusanyika kwa wingi, wewe nenda kaitangaze Zanzibar kwa njia yoyote ile ya ujanja, almuradi tufahamike tu kwamba Zanzibar ipo.

Mhe. Spika, ningemuomba vile vile, Mhe. Waziri, kwenye masuala ya mahoteli akahakikisha sana kwa sababu wananchi tutawahisi wakorofi, lakini saa nyengine si wakorofi. Kwa sababu mgeni anapo-*invest* sehemu ile basi angalau awape *priority* wale Wanakijiji kwenye kuwapa ajira au hata kwenye kuwasaidia labda katika mambo madogo madogo. Lakini unakuta pengine mahoteli mengine hata ile *pump* ya maji ya laki mbili wanakuwa hawawezi kuwasaidia wananchi na ajira pia hawajawapa.

Sasa ningemshauri Mhe. Waziri, akalifuatilia kwa kina kwenye mahoteli yote ya Zanzibar. Angalau akawauliza kwenye mji huu, wewe umejenga katika kijiji mfano cha Pwani Mchangani changu mimi ninajitaja. Katika hoteli yako umetoa hata ajira moja kwa mwananchi wa kijiji. Ikiwa hata ulinzi, usafishaji, *receptionist* au *house keeping* wanakijiji umewapa kama *priority*. Na je, kama hujawapa, kwa nini huwapi wakati nafasi zipo za kuwapa hata watu waliokuwa hawajasoma.

Mhe. Spika, isitoshe vile vile angeweza hata kuwauliza hata kama hujatoa ajira, ni kiasi gani ambacho umewahi kusaidia tokea umejenga hoteli katika kijiji,

kwa sababu kuna changamoto nyingi. Ningemuomba sana Mhe. Spika, Mhe.Waziri, suala la ajira kwa hasa wale wanakijiji angewapa *priority* sana kwa kushirikiana na wamiliki wa mahoteli na wale wote ambao walo-*invest* waliopo kwenye maeneo yao.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu kwa upande wa utalii nimesema nizungumze haya na sasa niingie kwengine.

Vile vile, ningemshauri Mhe. Waziri, angeweka *comments box* katika *Airport* na Bandari. Wageni wowote wanaosafiri, wanaorudi katika nchi zao basi wawe wanapewa karatasi ndogo tu ya *comments* ambayo itaeleza tu ndani tarehe aliyoondoka, aliingia lini na *servicea* ya Zanzibar kwa upande wa utalii upo vipi. Kama karidhika atie *tick* ya '*yes'* au labda hajaridhika '*poor' and 'excellent'*, atengeneze vitu kama hivyo. Zile *papers* zitolewe bure ili mgeni aweze ku-*comments*, halafu yeye wizara yake itampa *feedback* baadae kwamba wageni wana-*complain* kitu gani. Ajaribu kuorodhesha vitu tofauti, labda *beach* fulani na wageni wapate kutia *comments* zao. Lakini hichi kitu sifikirii, inawezekana ikawa ile *box* ipo, lakini kwa kuwapa *papers* hakuna. Sasa ningemuomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri, angegharamia kidogo kwa njia ya kutangaza vikaratasi vidogo, lakini kuhakikish wale wageni wanaotoka ndani ya nchi ambao wameshakaa Zanzibar, basi waweze kutoa *comments* zao wameridhika vipi na Zanzibar na jambo gani limewakera ili sisi Zanzibar nzima tukajaribu kulirekebisha kwenye masuala haya ya matatizo.

Vile vile, Mhe.Spika, nakuja na maswali yangu sasa naomba uje unijibu haya kwenye suala la utalii. Suala la mwanzo. Je, utahakikisha vipi wageni wanapata haki nzuri bila ya usumbufu. Yaani kwa ufupi kama nilivyokwambia mwanzo kwamba wanapata matatizo mengi na hasa kwa hawa mapapasi, ma-*beach boys* wanawakera sana. Ni vipi utakuja kudhibiti suala hili kwa njia yoyote ile na kama tunavyofahamu kwamba mapapasi wengi siyo watu wa kawaida, wengi ni watu wavuta unga na wengine unafikiria kama mwendawazimu kama vile alivyo kwa hali yake aliyokuwa nayo. Je, uta-*control* vipi suala hili ili wageni wasisumbuke na wasikerwe.

Kwa sababu hali hii...

Mhe. Spika: Una dakika mbili, Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al- Wardy: Eeh! loo! Ahsante sana.

Vile vile, ningeomba kumuuliza Mhe. Waziri. Je, suala langu la ajira, *priority* kwa ajira kwa watu wanavijiji, atahakikisha vipi kukaa na watu wenye mahoteli wananchi wakapata ajira kwenye zile sehemu zilizokuwa zimeshakuwa *invested* katika hoteli.

Suala langu jengine. Una mpango gani wa kutafuta masoko mapya hasa nchi ambazo hazijaanza kuleta wageni wake Zanzibar au hazileti wageni kwa wingi Zanzibar. Vile vile, Mhe. Spika, ningeomba kumuuliza Mhe. Waziri, suala langu jengine wizara yako imeshawahi kushiriki mara ngapi maonesho ya utalii au yoyote ya kuitangaza nchi yetu, Bara la Afrika hapa duniani kwa ujumla. Hilo suala langu jengine. Suala langu jengine ni lini wizara yako itakaa na wageni kuwaalika na kubadilishana mawazo ya utalii pamoja na mambo mengine. Kwa maanisha kwamba lini hasa imekaa pamoja na wageni kuwasikiliza matatizo yao kwa ujumla. Ninataka kujua suala hili aje anijibu hapo atakapoleta masuala yake mengine.

Kwenye masuala ya utamaduni na michezo Mhe. Spika, kwa kweli sikuwahi kuyachangia kutokana na dakika, lakini ninayo nitaweza kuyachangia kwa maandishi ili nisipoteze muda. Isipokuwa nimpongeze sana kwa utendaji wake mzuri wa kazi alipoanza kuingia pamoja na mashindano ya mpira ya ligi yaliyofanyika *ZAHILFE*. Yamekuwa ni mashindano mazuri na yamevutia sana.

Kwa hilo, ninampongeza sana kwa sababu mimi mwenyewe nilikuwepo, niliona kidogo ijapokuwa kuna watoto kama mimi, lakini ile hali ilikuwa nzuri na inavutia. Ninampongeza sana kwa asilimia tisini, asilimia kumi yangu atakaponijibu masuala yangu ndipo nitakapokuja kuipitisha.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na atafuatia na Mhe. Nassor Salim Ali. Halafu baada ya hapo nitampa Mhe. Mwanaasha, achangie kwa sababu baadae itabidi aje achukue nafasi.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo ambapo ni mwanzo wa Ramadhani ili niweze na mimi kuchangia katika Hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Kwa kweli hotuba hii ni nzuri sana. Kama ingekuwa ni wanafunzi wameandika hii, wakaniletea mimi mwalimu kuisahihisha basi wasingepungua *marks 75*

ambayo kwa kweli ni *distinction*. Mwanafunzi anapata *distinction* kwa kupata 75. Hivyo, hakuna sababu ya kuikataa bajeti hii. Ni bajeti nzuri. Na ninasema bajeti zote ambazo zimewasilishwa, hii ni ya tano. Zote ni bajeti ni nzuri na inaashiria kwamba bajeti zitakazofuata nazo pia zitakuwa nzuri. (*Makofi*)

Mimi mchango wangu katika wizara hii utahusu mambo ya habari, michezo, utalii na kidogo nitakwenda kwenye hii bajeti. Lakini kabla sijasema lolote, niseme kabisa hapa hapa kwa sababu muda ni mfupi. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na nimsifu sana Mhe. Waziri. Juzi tulikuwa na ligi pale Mtopepo. Kwa sababu ligi ile ilikuwa imekwenda vizuri sana. Nikamuomba mheshimiwa huyu Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo aje awe mgeni rasmi. Alikuja ninamshukuru sana na baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi walikuja kama Mhe. Ali Salum Haji Mnadhimu, alikuwepo. Walishuhudia ligi ile ilivyokuwa nzuri sana.

Na baada ya mchezo ule ambao wananchi walihamasika sana na walikuwepo kwa wingi sana. Na ninawapongeza sana wananchi wangu wa Mtopepo kwa kujitokeza kama vile. Ninataka pia au ninawaomba pia katika mambo ya maendeleo washiriki kama vile tulivyoshiriki kwenye ligi hii.

Baada ya kumaliza mchezo Mhe.Spika, tulikwenda na kuonana na wasanii. Kwa kweli wasanii wale walimfurahia sana Mhe. Waziri. Wasanii wa filamu hizi kwa sababu kule Mtompepo kwa kweli kuna wasanii na kuna watu wa aina mbali mbali wa michezo. Na aliwaahidi kuwasaidia na waliondoka pale wamefurahi sana. Ninampongeza sana Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa nikianza na habari. Habari tunazo sisi ndani ya mioyo yetu. Habari tukiziacha ndani ya mioyo tusipozitoa zinakuwa si habari na haziwezi kusaidia chochote. Ninatoa mfano hapa hapa kwenye ukumbi wetu. Anaweza kutokezea muandishi wa habari akaandika habari ya kusisimua hapa hapa ndani ambayo sote tunaona na wananchi wote wakavutika. Lakini pia habari zinaweza kupotosha na kusababisha madhara makubwa kwenye nchi.

Sasa habari ambazo ni nzuri ni zile ambazo huwa zinahamasisha, zinafurahisha, zinatoa taaluma, zinatoa taarifa na zinaelimisha na pia huwafanya watu wawe karibu zaidi kwa kuendeleza urafiki, upendo, ujirani mwema salama na amani pia. Aidha, husababisha kuleta mshikamano mkubwa sana pamoja na ushirikiano ambao ndiyo nguzo kubwa sana ya maendeleo.

Kwa ufupi kabisa ili hata kutuliza hili vurugu ambalo linatokezea siku hizi kwenye siasa. Kama tutaweza kupeleka habari kwa vizuri zaidi na kwa fasaha zaidi kwenye Mikoa, Wilaya na Majimbo yetu, ninadhani hata hizi vurugu vurugu zinaweza zikatoweka kabisa. Kwa sababu zinakuja vurugu kwa sababu watu wanakosa ile habari ambayo itawasaidia wao kuishi kwa salama na amani na kuleta maendeleo yao.

Kwa hivyo, ninasema kwamba lazima tutumie sana habari kwa faida ya maendeleo yetu. Na wale ambao ama kwenye *internet* au kwenye vyombo vya habari, magazeti wanaopotosha habari. Mimi ningeshauri sana Wizara husika wawapeleke mbele ya sheria ili wawache kabisa mtindo wao wa kupotosha potosha habari.

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye michozo. Kwa kweli michezo nayo kwa sifa inalingana na habari, kwa sababu huhamasisha, hufurahisha, hufanya urafiki na huleta upendo na kila kitu katika nchi. Pia, michezo huleta afya na ni ajira. Mwanamichezo akitambulikana kwamba ni mzuri hapa basi aende popote duniani atapata marafiki, aende popote duniani atapata ajira hata kama hana elimu ya kutosha, ingawa elimu itamsaidia kumwezesha kufanya mambo yake vizuri, lakini hata kama hana elimu ya kutosha anaweza kwenda duniani popote akapata ajira ya michezo. Wanamichezo wengi sana ambao hawana elimu wamekuwa wakiishi maisha ya kifalme.

Mhe. Spika, mfano mdogo ni David Beckham, mfano mwengine wa upande wa msanii wa ngoma hizi Michael Jackson nasikia tajiri mkubwa na wengine wengi wamekua hivyo. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Habari, Utalii na Michezo itilie mkazo sana mambo ya michezo, ikiwemo michezo ile ya utamaduni, kucheza karata, kucheza bao, kula maandazi, mchezo wa magunia, yote hii ni michezo ambayo kwa kweli kama itachezwa basi italeta mshikamano mkubwa sana katika taifa letu.

Mhe. Spika, nije sasa kwenye utalii. Nakwenda haraka kwa sababu muda hautoshi. Nije kwenye utalii, mimi nina uzoefu mmoja wa utalii wa ndani na nje pale Rwanda, tulikwenda Rwanda siku moja tukakuta pale Kigali pana makumbusho.Makumbusho yale hakuna kubwa lililooneshwa pale ni makumbusho ya vita vya Rwanda vilivyotokea, mauaji ya Kigali yanaoneshwa pale kwa njia ya ama ya *audio* au kwa njia ya maandishi na kadhalika. Sasa watalii wengi sana walikuwa wanakwenda pale wa ndani na nje ya nchi na walikuwa wanalipia. Kwa hivyo, mimi naishauri wizara kwamba waitumie makumbusho, tujenge makumbusho ambayo watalii watakuwa wanakuja, wanaingia na wanalipa, tunaongeza mapato ya nchi yetu.

Vile vile, kuna siku nilishauri hapa kwamba duniani siku hizi kumeingia mtindo wa kuwa na *International Healing Centres*, ni vituo kama vya afya. Hizi zinasaidia sana wale watalii matajiri kabisa duniani ambao kwa kutafuta zaidi mali, kwa sababu binaadamu hatoshiki kila akipata zaidi anataka zaidi, mwisho wake anapata *frustration*. Sasa anapokuwa na *frustration* huwa anataka mahala pa kupumzika, ni hizi *International Healing Centres* ambazo ndizo wanazozitumia kuja kwa mapumziko.

Kwa hivyo, naishauri wizara tuanzisheni utaratibu wa kuwa na *International Healing Centres*, ziko kwenye *Internet* maelezo yake yako vizuri sana, wanazo India, Uingereza, Marekani na kila pahala zipo katika dunia hii kwa ajili ya kuvutia watalii. Sambamba na hili, kuna hizo *Conference Tourism* na kadhalika, zote husaidia kuingiza mapato katika nchi.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuingia kwenye bajeti. Hii bajeti nasema ni nzuri tena sana. Kitu kimoja tu ambacho kidogo kimenishangaza, katika ukurasa wa 41 pale ndipo ilipoanzia. Pale kuna *Miscellaneous Expenditure* ambayo ni matumizi mengineyo. Ziliidhinishwa shilingi milioni 749, lakini hadi kufikia Machi zimepatikana asilimia 24 tu ya fedha zote hizo. Sasa mimi nilikua nashangaa kwa sababu *Miscellaneous Expenditure* hii ina umuhimu wake, kwa sababu inakuwa mambo mengi yameshapangwa hiki kitumike hivi na hiki kitumike hivi, sasa hii *Miscellaneous Expenditure* inatumika kwa mambo mengine mengine yatakayotokezea.

Sasa naona imepatikana kidogo sana hadi kufikia Machi. Sijui kuna tatizo gani hapa kwamba fedha hazikuwepo au zimetengwa zije zitumike katika kipindi hiki cha miezi mitatu iliyobakia au miwili, sijafahamu. Lakini kama fedha hazikupatikana kwa sababu hazipo, basi hilo ni tatizo la kawaida. Lakini kama hizi shilingi 183 zimetosha kwa wiki tatu na zilizobakia pengine hazitazidi pengine ni shilingi milioni 100 basi nashauri sana maombi ya bajeti yatakayofanywa bora yawe *realistic* ili isijekuwa tumetaka kingi na kinaonekana kingi, kumbe tulikuwa tunataka cha kiasi tumepata cha kiasi. Kwa hivyo, nashauri sana hizi bajeti tuziangalie wakati wa kuzifanya tufanye bajeti zetu ziwe *realistic*.

Mhe. Spika, halafu nichangie kwenye mapato nako hali ni kama ile. Kuna Baraza la Kiswahili, lilitegemea kupata kama milioni 1,799,000, lakini zilizopatikana hadi leo ni asilimia 4 tu ya mapato yote, sasa sijui hii iliangaliwa kwamba mapato yao ni kiasi fulani au ilikaa tu ikakisiwa wakusanye milioni hizi na mpaka leo wakapata asilimia 4. Mhe. Spika, ninachokisema hapa kwamba, ni bora tuwe na bajeti ambayo ni *realistic*, tusione haya kusema

tutapata kidogo, kwa sababu tukisema tutapata kikubwa halafu tukapata kidogo, hapo tena ndio inakuja mambo ya uaminifu sasa, inaonekana mtu sio mwaminifu kumbe umebajeti vibaya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nadhani mimi nikae ndani ya muda nisizidishe, kwa sababu pengine wachangiaji ni wengi na mambo ni mengi niishie hapa. Nimalizie kwa kukupongeza sana Mhe. Waziri na mawaziri wote kwa uteuzi wao na inaonekana kwamba tutakwenda vizuri sana na wao, tafadhali tushirikiane. Majimboni huko kuna matatizo mengi sana na namuomba sana Mhe. Waziri hapa uwanja wetu wa Matemwe kule Mtopepo, ambako kuna vijana wazuri sana wachezaji wa mpira, ule uwanja uko kwenye mteremko kidogo, hivyo, umeliwa sana na maji. Kwa hivyo, nimeomba *dozer* na Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano, ameniahidi kuwa atanipa *dozer*, na Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo, tushirikiane kuvitengeneza viwanja vya ndani, kwa sababu kule ndiko wanakozalishwa wanamichezo. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia, ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali (Aljazira): Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Utalii na Michezo. Pia, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri. Vile vile, nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kumteuwa Mhe. Rashid Ali Juma, kuongoza wizara hii, mimi nasema hapa amepata jembe na jembe hili nadhani ni jembe la trekta.

Vile vile, nimpongeze Katibu Mkuu kwa uteuzi wake ambao ameupata na nina imani kwamba majembe haya mawili yatafanyakazi vizuri katika kuendeleza sekta mbali mbali za habari, michezo na mambo mengine. Kwa sababu namfahamu vizuri sana Mhe. Katibu Mkuu, ni mwana michezo mahiri, ameiletea sifa kubwa Zanzibar na nadhani wengi wanamfahamu kutokana na umahiri wake huo wa uwanamichezo.

Mhe. Spika, nianze na uimarishaji wa *ZBC*. Mhe. Spika, nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuanzisha Shirika la Utangazaji *ZBC*, ni nia nzuri na inastahili pongezi serikali kwa kuanzisha shirika hili. Mhe. Spika, miongoni mwa Sera za Chama cha Mapinduzi CCM katika Ilani ya kuimarisha sekta ya habari Zanzibar. Hii ni moja katika sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Lakini Mhe. Spika, *ZBC* bado inahitaji kuimarishwa zaidi kabisa, kwani *ZBC* hii au Shirika la Utangazaji sio ile ambayo tulikuwa tumezowea zamani.

Mhe. Spika, wakati ule kwenye miaka ya 1990,1994,1998 mpaka 2002 *ZBC* wakati ule ilikuwa ni *TVZ* ilijenga heshima kubwa sana, ilikuwa inaonesha makombe ya dunia yote ambayo nimeyataja katika miaka hiyo, ilifanyakazi

nzuri. Hata katika mashindano mbali mbali ya *Africa Cup*, ligi kuu ya Uingereza *TVZ* katika kipindi kile ilifanya kazi nzuri na ilikuwa na mashabiki au waangaliaji wengi sana. Lakini msukumo ule kwa kweli umepotea. Sasa niishauri wizara na serikali ili liwezeshwe Shirika hili la Utangazaji *ZBC* ili lijiendeshe kibiashara na itawapa fursa Wazanzibari, Watanzania na ulimwengu mzima ili kuweza kuiona *ZBC* yetu.

Mhe. Spika, juzi nilikuwa naongea na shemegi yangu mmoja yuko Belgium, alinisifia kwa kuiona *ZBC* Belgium, ni hatua kubwa sana kwamba leo *ZBC* inaonekana Belgium, maana *Europe*. Lakini ipewe msukumo zaidi ili ijiendeshe kibiashara Mhe. Spika, tuondokane na hapa tulipo.

Mhe. Spika, sisi humu tuna waandishi wa habari ambao tunakanao kuanzia asubuhi mpaka jioni, baridi yote wanaipata humu. Mhe. Spika, Baraza lako tukufu chini ya uongozi wako nikupongeze sana kwa uongozi wako mzuri ambao umeanza vizuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakuongoza vizuri na kuweza kutuongoza sisi. Nimeweza kutoa fungu la kuilipa *ZBC*, ili tuendane na wakati vizuri na wananchi wetu waweze kuona mambo mazuri ambayo yanazungumzwa na viongozi wao.

Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri, atakapokuja atueleze ni kiasi gani cha fedha ambazo umeshalipwa na Baraza la Wawakilishi na kiasi gani ambacho hawa ambao tunaishi nao kuanzia asubuhi mpaka jioni wameshalipwa kiasi gani, kwa sababu wanafanyakazi kubwa. Aje atueleze ni kiasi gani wamepata na kiasi gani ambacho wamelipwa waandishi hawa wa habari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nije katika sekta ya michezo kurejesha hali ya michezo Zanzibar. Mhe. Spika, kweli juhudi zimefanyika, kama ambavyo Mhe. Waziri, alivyoeleza katika hotuba yake kwenye ukurasa wa 17. Juhudi ambazo serikali imezichukua katika kuendeleza michezo, lakini bado juhudi hizi Mhe. Spika, zinahitajika kuongezwa ili kurejesha hadhi ya michozo Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hadhi ya michezo Zanzibar imepotea kutokana na migogoro ya vyama vya michezo, kukosekana kwa viongozi wenye uwezo wa kuongoza michezo. Mhe. Spika, migogoro na hii sio siri, sote tunajua, takriban miaka mitano ambayo tumemaliza Zanzibar michezo imeanguka hadhi yake kutokana na matatizo ya migogoro, hususan mchezo wa mpira wa miguu. Kwa hivyo, ni vyema wizara ikalifanyia kazi hili ili tuondokane na matatizo haya ya migogoro ndani ya vyama vyetu vya michezo.

Halikadhalika, kutoendelezwa na kuimarishwa mfumo wa ukuzaji wa vipaji vya wanamichezo wetu, mambo haya yamechangia kuporomoka kwa hadhi ya michezo. Nini tufanye, mimi nadhani Mhe. Spika, ili tuweze kurejesha hadhi ya michezo kwa kuimarisha viwanja vyetu vya michezo. Tutakapoimarisha mambo ya michezo, hata yale mambo mengine ya kukaa vijiweni kuzungumza mambo ambayo hayana msingi, kuzungumza siasa ambazo hazina msingi. Wananchi watakwenda katika viwanja vya michezo kuangalia michezo, lakini kazi ambayo tunayo ni kuimarisha ili michezo yetu iende juu.

Mhe. Spika, kwanza, tuweze kudhibiti dalili za kuondoa hii migogoro. Pili, Mhe. Spika, Baraza la Michezo libadilike, vile vile, libadili sheria na kuwa na chombo chenye uwezo wa kuchukua majukumu ya chama chochote ambacho kinaleta migogoro. Lazima kubadilishwe sheria ili kuweza kudhibiti migogoro hii ya vyama vyetu vya michezo.

Jengine Mhe. Spika, hata hawa viongozi wanaochochea lazima wadhibitiwe, bila kudhibiti haya basi tutakuwa tunapiga kelele kila siku. Jambo jengine ambalo tunaweza tukafanyakazi kwa kuendeleza vipaji vya vijana wetu na kuanzisha mifumo ya kukuza na kuendeleza vipaji vya wanamichezo wetu. Mhe. Spika, ni lazima tuangalie mipango ambayo inaweza kuimarisha vijana wetu. Hivi sasa hata mashindano ya kuimarisha na kuvilea vipaji vya wanamichezo wetu havipo.

Mhe. Spika, kuna maeneo ambayo yanatumiwa na wanamichezo wetu *football* na *basketball*, kuna maeneo ambayo tumeyawacha yamevamiwa. Kuna kiwanja cha *basketball* pale Malindi, leo kinatumika kwa shughuli za kuweka madaladala pale, tunakwenda wapi, lazima tufanyekazi, tusimamie na tukemee mambo ambayo yanasababisha kudumisha michezo yetu.

Mhe. Spika, kuna kiwanja pale katika Uwanja wa Demokrasia ambapo vijana wengi wanatumia viwanja vile kwa ajili ya shughuli za michezo, lakini pia vinavamiwa, watu wanakwenda kuweka magari yao pale, halafu vijana wanakosa sehemu za kucheza, sasa ni vyema tukalifanyia kazi suala hilo na kuviendeleza hivi vipaji, mimi niipongeze sana kwa roho safi kabisa Chama cha Mpira wa Miguu Wilaya ya Mjini kinafanya kazi nzuri *ZFA* Wilaya ya Mjini inafanya kazi vizuri, ni chama ambacho cha Wilaya lakini kinafanyakazi vizuri, juzi nimeshuhudia pale wamefanya mambo mazuri, lakini tatizo sijui ni nini kwa *ZFA* Taifa. Mheshimiwa, hebu twambie pengine wewe jembe hili limeshaanza kulima lima kwa sababu kuna jembe la mkono Katibu wako Mkuu pengine mshajua, njoo utwambie tatizo ni nini.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka nilizungumza ambalo pia nimeliona ni suala zima ambalo linahusia timu zetu za Taifa, hivi sasa duniani kumeanza mashindano ya *Copa America* na baadae kuna mashindano ya *Europe*, nchi nyingi ambazo zinashiriki mashindano haya, nchi husika zimesaidia timu zao za Taifa na hata katika mashindano ya Afrika, nchi zinatangazia timu zake za taifa, sasa ni vyema Serikali yetu tukajikita zaidi kusaidia timu zetu za taifa. Lakini hapa Mhe. Waziri, ukimuliza, mwakilisha saidia, mwakilishi atasaidia mangapi na vilabu vingapi huko jimboni, juzi Mhe. Gavu, ananambia ana timu 16, zote zinahitaji jezi na mipira anaweza kuzimaliza zote hizo, anaweza kwa sababu ya mapenzi yake na imani yake, ndio, lakini timu za taifa ni jukumu la Serikali.

Sasa niiombe sana Serikali kuhakikisha kwamba tunatafuta wadhamini kwa timu zetu za taifa ili kuweza kushiriki vizuri katika mashindano ya kimataifa...

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, katika miaka ya nyuma katika kumbukumbu zangu nakumbuka kulikuwa na Kamati inaitwa *SAZI* (Saidia Zanzibar Ishinde) na kamati hii ilifanya kazi nzuri, kipindi kile Mwenyekiti wake alikuwa Mhe. Raza, nakumbuka, Katibu wa kamati alikuwa ni Mwalimu Abdalla Mwinyi Mkuu wa Mkoa Mstaafu, ilifanya kazi nzuri sana, sasa nashindwa kwa nini Serikali haiundi kamati kama ile ili ikatafuta wadau ambao wana uchungu na mapenzi na nchi yao, wana uchungu mapenzi na michezo kuunda kamati ambayo itaisaidia Zanzibar. Kwa sababu Serikali ina mambo mengi, ina masuala ya kuendeleza jamii, ina masuala ya kupeleka maendeleo ndani ya majimbo katika sehemu mbali mbali, mabarabara. Sasa ni vyema kuunda kamati, wako wafanyabiashara ambao nina imani ikiundwa kamati nzuri kama ile ya Mhe. Raza ya *SAZI*, basi mambo yatakuwa mazuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie kwa wasanii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kubwa sana kwa kutambua juhudi za wasanii wetu ambao wamejiajiri kupitia vipaji vyao, lakini juhudi hizi zinarudishwa nyuma kwa malipo kidogo ambayo wanayapata, bahati nzuri mimi niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mirahaba, nalijua vizuri suala hili. Sasa nimalizie kwa sababu najua taa imeshaanza, lakini Mheshimiwa, baadae nitamuandikia kwa maandishi haya ili kuweza kuwasaidia wasanii wetu, ili tuweze kukuza vipaji vyao juzi alikuwa mgeni rasmi aliona mambo ya wasanii wetu ambayo Zanzibar wameanzisha, mambo mazuri, kwa hivyo, ni vyama tukawasaidia wasanii wetu ili kuweza kupata ajira kuendeleza wao na kuendeleza familia.

Baada ya maneno hayo Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia 95, ahsante sana Mheshimiwa (*Makofi*)

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuichangia hotuba ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Lakini kwanza kabla sijaanza katika kuchangia napenda niwapongeze au nimpongeze Mhe. Waziri na utendaji wake wote kwa jumla kwa kufanikisha hotuba hii ambayo imebeba mambo mengi ambayo tulikuwa tunayatarajia katika Wizara hii.

Lakini vile vile nimpongeze Mhe. Rais kwa kuona umuhimu wa filamu na miziki kwa kuwafungulia *studio* hapo Rahaleo, kwa hivyo, nichukue fursa hii kumpongeza Rais.

Lakini nianze kwa upande wa kuchangia ambayo na mimi nimeyaona katika hotuba hii, kwanza, nilikuwa naomba kuchangia katika hotuba yake, ukurasa wa 28, kuhusu maeneo ya vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, hapa nimeona vipaumbele vingi ambavyo vimeletwa katika hotuba hii kama ifuatavyo:

1. Kuimarisha miundombinu ya *Digital* na ununuzi wa Ving'amuzi
2. Kuimarisha Makumbusho ya Pete Unguja.
3. Kukamilisha Sera ya Michezo na kujenga viwanja vitatu vya michezo vya wilaya.
4. Kutangaza sekta ya utalii ndani na nje ya kwa kutumia njia za kisasa.

Lakini Mhe. Spika, nilikuwa namuomba sana Waziri, aingize kipaumbele cha wasanii wa filamu na muziki, kwa sababu wasanii hawa wengi ni vijana na tayari wameshajiajiri, kwa hivyo, nilikuwa namuomba sana Waziri aingize suala hili ili iwe kipaumbele na wao wasanii kwa vile wameamua kujikusanya na kujiajiri wenyewe, kwa hivyo, hapa pia namuomba Mhe. Waziri, alione hili.

Lakini chengine katika hii hotuba ya Mheshimiwa, bado sijaona kama kuna vipaumbele ambavyo vimewachukua watu wenye ulemavu katika suala zima michezo, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja katika kufanya majumuisho yake aniambie kuna mipango gani mikakati au vipaumbele gani ambavyo wameviweka katika sekta hii ya michezo, kuhusu watu wenye ulemavu ili na wao wajioni ni sehemu ya jamii katika nchi yao.

Jengine, Mhe. Spika, ambalo nataka niiombe hii Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, wawe na mashirikiano ya karibu sana na Wizara ya Elimu kwa kuinua vipaji vya michezo maskulini, kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Wizara iwe na mahusiano ya karibu na Mashirikiano ya karibu sana, najua wana mashirikiano lakini nilikuwa naomba wawe na mashirikiano ya karibu sana ili kuona tunaibua vipaji kupitia michezo ndani ya mshule yetu.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka nichangie kwa upande wa Redio. Mhe. Spika, redio yetu ni nzuri, lakini kuna mapungufu yake kidogo hasa katika sehemu ya utayarishaji wa vipindi pale Redio, mimi nakumbuka katika kipindi cha kampeni tuliwahi kwenda pale tukafanya mahojiano na mtangazaji Nasra Mohammed katika eneo lake lile la matangazo na utayarishaji wa vipindi, kwa kweli inasikitisha Mhe. Spika, lile jengo halina hadhi, haliko vizuri na mpaka mtangazaji mwenyewe anaona tabu kukukaribisha katika kufanya mahojiano ambayo ni mazuri tu na kwa nia nzuri.

Kwa hivyo, lile jengo halina hadhi kusema kweli kama redio nyengine, kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, akija katika majumuisho yake aje atueleze ni mkakati gani au taratibu gani ambazo atazifanya katika kuboresha maeneo yale ili na sisi tuone tukienda pale tunajua tumekwenda katika chombo cha habari ambacho Redio na kina hadhi kama redio nyengine.

Mhe. Spika, pia, nilitaka kujua katika Wizara hii Serikali ina mipango gani kuona wasanii wetu wanawezeshwa ili kuongeza pato la taifa kupitia sanaa za filamu. Lakini chengine pia Mhe. Spika, ambacho nilitaka kuchangia nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri wa Habari, aichukue kwa makusudi mazima kuona kwamba wasanii wetu wa filamu kuwapatia mafunzo, au kuwaletea wataalam ili kuona kuwa wanawafahamisha vizuri tuone wale wasanii wetu na wao wanaingia katika ubora wa filamu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri, alichukue na hili ili taratibu zifanyike kuona wana filamu hawa wanapatiwa mafunzo ya kitaalam ili tuweze kuona filamu zetu zina ubora wa kimataifa.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwanza kabisa nataka nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi kuweza kuchangia hotuba hii, lakini awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo kukutana hapa na tarehe mosi Ramadhani. Namshukuru Mungu kwa sababu mimi nimepata fursa kwa mara ya kwanza kuzungumza kwenye

Baraza hili na kilichosababisha nikapata fursa hiyo kama mnavyojua ni kutunukiwa na Mhe. Rais, uteuzi wa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana kwa sababu wale wenzangu waliokwenda kwenye majimbo wamenihadisia kwamba haikuwa rahisi, wengine wameparwa parwa kwenye kura za maoni, wengine wamekwaruzwa kwaruzwa kwenye uchaguzi, kwa hivyo, mimi sina budi nimshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuweza kuniteua na nikafika hapa, nikapata fursa hii ya kuzungumza na Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi.

Nampongeza Mhe. Rais kwa kuchaguliwa tena kwa kura nyingi sana katika uchaguzi wa marejeo, naamini kwamba ilikuwa ni haki yake kuchaguliwa kwa sababu Mwenyezi Mungu alijaalia kwamba kulipita uchafuzi na uharibifu wa uchaguzi ule ambao ulipangiwa tarehe 25 Oktoba, 2015. Mwenyezi Mungu yule yule ambaye ametujaalia kufanya Mapinduzi nchi hii na tukafuzu ndio Mwenyezi Mungu yule aliyejaalia kujua udhaifu ambao wenzetu wa Upinzani walioufanya ili wapate madaraka, na yalipotokea yale kanikumbusha maneno ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema kwamba; "katika nchi ya kidemokrasia nendeni mkagombee Urais, lakini msitegemee kwamba mtaupata Urais kwa ujanja ujanja". (*Makofi*)

Napenda pia kumpongeza Mhe. Rais kwa kumteua Balozi mwenzangu, kaka angu, rafiki yangu aendelee kuwa Makamu wa Pili wa Rais, chaguo hilo naamini Mhe. Rais Dkt. Shein hakubahatisha wala hakubabaisha kafanya uchaguzi mzuri sana, napenda kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa kukalia kiti hicho, naamini una sifa zinazotakiwa na imani yangu ni kwamba Mwenyezi Mungu atakujaalia utuendeshe kwa upeo mkubwa uliokuwa nao na pia kwa busara. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika kuendelea kuishukuru napenda kumshukuru sana rafiki yangu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa na nilikuwa naisikiliza kwa makini na hajakosea neno hata moja, nimeisikiliza kwa makini, nimeipenda hotuba ile na ndio maana nikaamua kuchangia Mhe. Spika, kwa sababu hayo nitakayoyasema mnayajua lakini nataka nikukumbusheni.

Kulikuwa na Rais mmoja alikwenda kuambiwa kwamba katika uchaguzi uliopita hatukupata viti vya kutosha kwenye Baraza la kutunga sheria, kwa hivyo, itabidi tuunde Serikali ya pamoja na Upinzani, akasema sawa, lakini mnapochagua mawaziri huko chagueni zile Wizara muhimu zilizokuwa nzuri

nzuri, lakini katika Wizara hizo muhakikishe kwamba Wizara ya Habari tunashika sisi. Alipoulizwa kwa nini akasema kwa sababu mkija mkiwaachia Upinzani wakashika Wizara muhimu kama hii Wizara ya Habari watakwenda kuwadanganya watu, watawapotosha watu halafu watakuja kutuletea matatizo kwenye uchaguzi utakaofuatia. Haya ninayozungumza nafikiri nyote mshajua nayazungumzia kwa nini, tuhakikishe kwamba Wizara hii pamoja na Wizara zile muhimu tunazikamata wenyewe Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Nataka kukumbusha tu kwa wale ambao hawakuwepo siku ile ya Mapinduzi mimi nilibahatika kuwepo hapa, tuko siku nyingi, siku ile agizo la mwanzo kwa Wanamapinduzi lilikuwa kwamba Nendeni Rahaleo mkakamate kituo cha habari na ndivyo ilivyokuwa, tuliona umuhimu wa habari, tukenda tukakamata kwanza kituo cha habari Rahaleo ili kutangaza Mapinduzi na wale walikuwa wanatangaza wanayotaka wao walikuja wakaonekana kwamba wanasema uongo. Mapinduzi kweli yalitokea siku ile na yakatangazwa nchi nzima na rafiki yangu nafikiri alisikia kwa sababu hata huko Tumbatu alisikia kwamba leo Mapiduzi. (*Makofi*)

Kulitolewa mfano hapa wa vita vya Iraq, nakubali kwamba, kule Iraq wakati wa vita vile kulikuwa na Waziri mmoja alikuwa anashadidia kwamba Marekani waongo, alikuwa anasema hao Wamarekani hao waongo, hata hapa Iraq hawajafika akaonyeshwa kwenye *TV*, akasema hao wameshaingia wameshachukua *Airport*, akasema hapana uwongo huko kwao Marekani wanatengeneza michezo ile ya kuigiza *Hollywood*, halafu akatia progamu yake yeye ya zamani, akasema mnaona tunaingia hapo *Airport* na askari wetu wapo, pale aliwababaisha watu wengi sana na ndio maana narejea yale niliyosema mwanzo Mhe. Spika, kwamba shughuli za habari ni muhimu sana.

Hata hapa kwenye Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kuna watu wanatuletea habari hapa, lakini na wao pia nawashauri kwamba katika maisha yako jaribu kudanganya danganya kokote lakini usende kudanganya kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, katika uchaguzi ule ambao ulifutwa wa Oktoba wa mwaka 2015, Wapinzani wetu walitumia vyombo vya habari kutaka kudanganya watu na kupotosha watu na kwa upande mmoja nusura manusura wende wakawadanganye watu, lakini kwa kuwa habari za ukweli zimepatikana, basi tuliweza kuwajuulisha wananchi kwamba uchaguzi ule ambao ulivurugwa umefutwa na baada ya kufutwa ule uchaguzi tukafanya uchaguzi wa marejeo tarehe 20 Machi, 2016 na uchaguzi umekwenda vizuri na umekwenda vizuri kwa sababu habari tulizozitoa zilikuwa ni za kweli.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nayarejea haya mara mbili, tatu kwa kuonesha umuhimu wa hii Wizara ya Habari, tena tumeishika wenyewe Chama cha Mapinduzi. Ningeomba tena nigeomba sana kwamba kabla hata sijamaliza mazungumzo yangu nakuombeni ombi langu kwenu tuipitishe bajeti ya huyu Mheshimiwa, na huko tunakokwenda katika bajeti ya mwaka unaofatia tumuongeze fedha.

Sasa nataka kumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kutuletea huu mpango mpya wa *Programme Base Budget*, hii ina umuhimu wake kitaalamu kwamba tusipange tu matumizi mwaka huo huo tu, tunabahatisha mwakani tunapanga hapana. Katupangia mpango mzuri utakwenda katika matumizi ya mwaka huu 2016-2017 na halafu akatuonesha na *projection* zake za 2017-2018 na 2018 mpaka 2019, baadae tutapotengeneza bajeti ya mwakani atatupa na hiyo *projection* yake mpaka kufikia mwaka 2020 ambao tutakuwa na uchaguzi. Kwenye hili nasema tupitishe bajeti hii na pia tuji-*commit,* yaani tuhakikishe kwamba katika miaka inayokuja tunamuongezea fedha ili kumuongezea nguvu katika shughuli ambazo anazifanya.

Kwenye hili katika kuchangia zaidi hili suala la kwamba *information is power*, yaani habari ni kitu kina nguvu sana. Nataka kusema kwamba kuna kiongozi nchi hii, yaani Kiongozi wa Upinzani kawapa wafuasi wake *wrong information,* kawadanganya kuwaambia kwamba msishiriki katika uchaguzi huu kwa sababu kutokushiriki kwenu kutasababisha nchi hii ufanywe uchaguzi mwengine ambao utasimamiwa na watu wa nje, aliwadanganya, habari hiyo haikuwa sahihi, na sisi ilikuwa wajibu wetu kuwapa wafuasi wake habari ya usahihi na leo nilitaka kusema kwamba, kazi hiyo tumeifanya vizuri na mimi nataka niwakumbushe kupitia Baraza lako Tukufu kwamba wasikae na wanaongozwa na kiongozi ambaye anawapa habari potofu.*(Makofi)*

Nimebahatika, mlinipeleka nchi za nje kuwa balozi na nimekuwa balozi nchi nyingi sana na nilistaafu kuwa *dean* wa mabalozi wa Tanzania. Ninakuhakikishieni na ninawakikishia wale ambao wananisikiliza nchi nzima kwamba hakuna nchi hata moja duniani iliyokwenda kuufuta utambuzi wa nchi wa nyengine kwa kuwa eti uchaguzi wao haukwenda vile walivyotegemea wao. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetambuliwa na karibuni nchi zote duniani na Zanzibar ikiwe ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetambuliwa na karibuni nchi zote duniani na hakuna nchi hata moja iliyotishia kwamba kutokana na kufutwa uchaguzi eti watakwenda ku-*withdraw recognition,* yaani watakwenda kutangaza kwamba hawatutambui tena kama ni nchi, habari hiyo iliyotolewa na Kiongozi wa Upinzani ni habari potofu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nataka tu Mhe. Spika, kwa kuwa hatuna muda wa kupasha wa kueleza mambo mengi, nilisema tu kwamba katika hili suala la habari ni muhimu na tumkubalie Mheshimiwa, mimi nimeshakubali *hundred percent*, apitishiwe.

Lakini pia nataka kwenda kuzungumzia kidogo kuhusu masuala ya utamaduni ya kusema kwamba, sisi Wazanzibari tuna utamaduni mzuri sana ambao unajulikana dunia nzima na ni wajibu wetu kuuendeleza utamaduni wetu na utamaduni wetu pia umeingia kidogo katika mambo ya dini na leo tarehe mosi Mfungo wa Ramadhani, imekuwa sasa sio tu tunafuata maagizo ya dini yetu, lakini imekuwa ndio utamaduni wetu.

Mhe. Spika, watu wengi watakuja wakati wa utalii kuja kututembelea hapa, msije mkaona ajabu kuja kuangalia vivutio vya utalii, lakini kivutio kimoja ni kule kusema, hivyo kweli kuna nchi watu wanaweza wakafunga kutwa, hawali, hawanywi mpaka jioni na wanakuja wanakwenda kuthibitisha kwamba ni kweli na wanaandika makala huko, wanatoa habari hizi njema kuwa ni kweli. Tembeleeni kule Zanzibar mtakuta watu wanafunga mwezi wa Ramadhani tena karibuni siku zote, hii inaonesha *discipline* ambayo tuliyokuwa nayo sisi Wazanzibari na utamaduni huo ni lazima tuuchunge na tuulee.

Sasa suala la michezo limezungumzwa michezo sio tu mambo ya riadha, lakini Mhe. Spika, inasaidia pia kwamba katika michezo tunapeleka timu zetu nchi za nje, wale wanakuwa kama ni mabalozi, wanakwenda kule nchi za nje wakiambiwa kwamba hii timu inatoka Zanzibar, basi watavyojiweka wale wanariadha wetu ndio watu watapotujua sisi Wazanzibari ni watu wa aina gani, kwa hivyo, hili tulitilie mkazo. Kama vile utalii kwamba watalii wanakuja hapa wanakuwa kama mabalozi wa nchi zao wanaporejea kwao kule wanakwenda kutuzungumza vizuri, wasitutegemee na sisi kwamba tunapeleka timu zetu na wao tuwaandae vizuri na wao watuzungumzie kwa uzuri.

Mhe. Spika, ninajua kuwa muda wangu umemalizika, lakini kwa kumalizia kabisa nitoe tena shukurani kwa Mhe. Waziri, kwa kutupa bajeti nzuri na mimi ninaiunga mkono na ninakuombeni muiunge mkono. Lakini la mwisho kabisa mzungumzaji aliyezungumza kabla ya mimi nataka nimpe pongezi kwa ujasiri wake. Katika uchaguzi tangu ule wa tarehe 25 Oktoba, 2015 aliwahi kutamka kwamba yeye atakwenda kupambana na mtu yeyote ambaye anaipinga CCM na kweli alishinda kwenye uchaguzi ule, wakenda wakatukoroga koroga huko, lakini Mwenyezi Mungu mkono wake umepita katika uchaguzi wa marejeo, karejea na kachaguliwa kuingia katika Baraza hili kihalali. Kwa hivyo, na mimi

ninamuunga mkono, Mungu amjaalie, ampe wepesi katika kufanya shughuli zake.

Mhe. Spika, namalizia kwa kuomba tena kwamba Baraza lako Tukufu lipitishe hii bajeti ya Wizara yetu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Balozi Ali A. Karume, naomba sasa nimwite Mwenyekiti ili aje achukuwe hii nafasi. Inaonekana kama hajawa tayari basi nitachukua nafasi sasa kumwita Mhe. Ussi Yahya Haji, aanze kuchangia, samahani amefika Mwenyekiti, kwa hiyo, nitampisha akishakufika atachangia Mhe. Ussi Yahya Haji.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti,Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nami nitoe shukurani zangu kwako kwa kunipa nafasi hii ndogo nichangie hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Kwanza Wizara hii Mhe. Mwenyekiti, ndio inao uzalendo na utu wa Mzanzibari na nishukuru kwa dhati kabisa kitabu chake cha waziri namna alivyo kisanifu tangu Kiswahili, maudhui na utamaduni wa Kiswahili hicho, ninamshukuru sana Mhe. Waziri.

Lakini la kwanza kabisa mimi nitazungumzia zaidi kuhusu maeneo ya historia. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina historia kubwa sana na katika mambo ya utamaduni kuna *commercial culture* na *preservation culture*. Kuna unatamaduni wa kibiashara na utamaduni wa kuweka na kuuenzi. Mimi nitakuja katika utamaduni wetu wa kuenzi. Mhe. Mwenyekiti, leo tuna Baraza la Wawakilishi liko Chukwani lakini Baraza la Wawakilishi halikuanzia Chukwani tulikuwa na *Legico* kabla ya Mapinduzi, jengo lile halijatunzwa, ninaiomba Wizara itunze jengo ambalo tangu mwanzo kwa kuweka mabaraza ya kutunga sheria Zanzibar tulikuwa tunalo, naliomba jengo hilo liwe *preserved* na litunzwe na historia hiyo iwekwe na vizazi vijavyo waelewe na hata watalii wetu watakapokuja watapenda kwenda katika sehemu hiyo. Jengo hilo liko *Victoria Garden* ambalo sasa jengo hilo linatumika kama Taasisi ya Kuzuia Rushwa, jengo hilo lilikuwa *Legico* la Zanzibar na ningelimuomba Waziri akalitupia macho na kuli-*preserve.*

Baada ya Mapinduzi mwaka 1978 tukawa na Baraza la Wawakilishi nyumba ambayo Mhe. Waziri, anaitumia kama wizara yake na hii nayo ningelipendekeza sana ikawekwa kama makumbusho. Au kama haikuwekwa kama makumbusho yenyewe basi kuwepo na utaratibu ambao utajulikana

kwamba Baraza la Wawakilishi la pili baada ya *Victoria Garden* ilikuwa pale Makumbusho. Hilo lilikuwa ni wazo langu la kwanza.

Wazo la pili, nimshukuru Rais kwa kuiweka Wizara hii chini ya Kamanda wetu, kijana wetu shupavu ameanza vizuri sana katika Wizara hii na hii ni dalili kwamba ule utamaduni wetu na utu wetu na uzalendo wetu utalindwa kwa sababu kulinda historia ni kulinda utu wako, bila kuweka historia hutoujua utu wako na ndio maana kulikuwa kuna alama alama za kuiua historia yote ya Zanzibar. Yale mambo yote ya historia yalikuwa yanaanza kutoweka tuweka. Mimi nashangaa sana ninamuomba Mhe. Waziri, aangalie sana nyumba ya Living Stone, nyumba ya Living Stone ina historia kubwa katika Afrika Mashariki, leo nyumba ile imewekwa *Chamber of Commerce*, mimi sifahamu *Chamber of Commerce* Zanzibar ni nzuri, iwepo lakini si kwa kuiua nyumba ya Dr. Living Stone tukaweka *Chamber of Commerce* ningelimshauri Waziri jengo lile likarejeshwa katika hadhi yake. Hilo lilikuwa la pili.

La tatu, tuna nyumba ya Tip Tip ambayo Tip Tip huyu ana historia kubwa sana na nyumba yenyewe sasa hivi hasa haijulikani na leo kwa vile tunatangaza utalii Zanzibar na watalii wote wanaokuja Zanzibar pamoja na kutalii kwao kote basi utawaona kwamba *spice tour* wanakwenda Kizimbani, Mahamamni, Kidichi, Nungwi, Kizimkazi, Darajani, tuna majengo mengi ya historia ambayo tunayaua makusudi ili utamaduni usifahamike. Kwa hivyo, tungeliomba na nyumba hii ya Mtip Tip nayo ikaangaliwa na ikawa *preserved* na kwa kweli majengo mengi ya historia tulikuwa tunayaua na tunayaua tulikuwa hatujui kwa nini, lakini mimi ninafikiri labda ilikuwa yanafanywa makusudi ili utamaduni wa Muafrika wa Zanzibar utoweke. Kwa mfano tunaambiwa siku hizi kuna hadithi zinatoka hapa kwamba Wazanzibari hawakufanywa watumwa. Wazanzibari tulifanywa watumwa lakini inazungumzwa kutoweka toweka tu isifahamike fahamike.

Mimi ningelimshauri Mhe. Waziri, anacho kitengo kizuri cha utafiti na anao wataalamu wazuri wa watafiti wafanya kazi ya kutafiti Zanzibar tulitoka wapi, tunakwenda wapi na tuko wapi na nini chimbuko la watu wa Zanzibari, kwa sababu kuna wengine wanasema Zanzibar ni *cosmopolitan,* yaani hakuna mwenyewe, *no,* Zanzibar kuna mwenyewe na Zanzibar ina historia kubwa sana na watafiti wa Wizara hii ikiwa watafanya utafiti watagundua hata uislamu umekuja mwanzo zaidi Zanzibar kuliko Madina na fanya utafiti, kwa sababu Zanzibar kuna makaburi yamegundulika hapa zaidi ya miaka elfu sita mtu amezikwa kiislam. Ninashukuru wameweka hapa katika eneo hilo la Unguja Ukuu zaidi ya miaka elfu sita, miaka elfu sita mtu amezikwa kiislamu Unguja Ukuu pale, ninashukuru kwamba katika utafiti wanaoufanya wametaja na

Unguja Ukuu. Lakini bado utafiti wa Zanzibar haujakamilika na unafutwa futwa hivi ili usifahamike.

Ninaiomba wizara hii ikae na ina wataalam wazuri sana naielewa, watafute utamaduni wetu wauweke na uso wa dunia ujue Zanzibar ilikuwa na wenyewe na wenyewe wa kwanza Zanzibar takriban ni Watumbatu, hakuna yeyote aliyevamia kuja Zanzibar basi aliwakuta Watumbatu, na Watumbatu ndio waliokwenda Kaskazi na Kusini. Huyu Kizimkazi (Mkiz) alikuwa ni Mtumbatu pia, lakini hakuna historia inayowekwa, kuna kina Mwana wa Mwana, kuna Mwanafatima, hawa wote ni Watumbatu, Mwinyimkuu, Mkamandume hawa wote historia yake bado inafutika futika tu. Kwa hiyo, ningeliiomba wizara hii ikachimbua utamaduni huo, kwa sababu Mwinyimkuu alikuwa ni mtawala wa visiwa hivi na ni Mswahili.

Nashukuru sana Mhe. Waziri, kuna vijana wa mila na utamaduni miaka ya nyuma walikuwa na mchezo wanaita Ukombozi wa Muafrika, walikuwa wanamuonyesha Mwinyimkuu namna alivyotekwa na watawala hapa wakamsukuma na wakamuua. Ule mchezo wa Ukombozi wa Muafrika urejeshwe nasikia ulikatazwa katazwa hapo nyuma, lakini ule mchezo ni muhimu sana, sana ili kuweka historia. Na gofu la Mwinyimkuu mpaka leo lipo lakini bado lina mwitu tu, liangaliwe kwani inasemekana Mwinyimkuu kauliwa pale *People's Bank* nyuma ya Ngombe Kongwe ndio penye kaburi lake, lakini hakuna anayejua.

Kwa hiyo, naiomba sana wizara hii iangalie sana tamaduni zetu, tunatoka wapi, tulikuwa wapi, kisiwa hiki wenyewe nani, *cosmopolitan* tunajua kwamba *cosmopolitan* kweli baadae walikuja Wachina, wakaja Washirazi, akaja Ali bin Hassan akawa hapa anaitwa Mshirazi, ndio maana tukapata vimaji maji vya Kishirazi shiraza hapa. Lakini wenyewe hasa hapa ni Watumbatu na Watumbatu ni Waswahili. Kwa hivyo, historia ya visiwa hivi lazima iwe *preserved*, lazima ieleweke, lazima ijuulikane. Na Waswahili wa hapa wana *affiliation* na Bara, haiwezekani historia ya Mswahili yeyote kuwa mtu wa Bara kuja visiwani awe mgeni kuliko mtu anayetoka kilomita 4000 awe mwenyeji hapa, haiwezekani hata siku moja.

Ni kweli watu wamekuja katika pepo za *West East Monsoon,* walikuja kufanya biashara na ndio maana kuna mabaki ya sahani za Kichina china huko na ndio maana hata visiwa vyetu hivi tumepata mazao mengi kutokana na mawimbi ya bahari kuleta minazi, kuleta mashoki shoki, kuleta mishelisheli. Lakini walipokuja hapa hao wafanyabiashara waliwakuta Waswahili wapo hapa wanafanya kazi, na Waswahili hawa kama utafanyika utafiti ikafahamika, kwa

sababu hii Unguja, maana yake ni “ungo umejaa”. Wavuvi wamekuja kutoka Bara wakakaa dago huko na wakavuna vuna mazao wakasema ungo umejaa, ndio hii Unguja.

Wenzetu wataalamu wakasema *Zenj Empire,* maana yake sehemu ya Waswahili weusi. Kwa hivyo, hiki kisiwa wenyewe hasa watu weusi na ndio maana hata mimi binafsi, mimi sipendi sana kusema Mzanzibari, Mzanzibari, Waswahili wa Unguja na Pemba ndio wenye visiwa hivi. Japo wanasema Wazanzibari, Wazanzibari, sawa, kwa sababu tunaweza kusema Watanganyika, Waganda, Wakenya ukiita Wazanzibari, sawa, lakini hasa wenyewe hapa ni Waswahili wa Matumbwi wa visiwa hivi. Kwa hivyo, naiomba wizara hii ijitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuhusu wasanii, namuomba Mhe. Waziri, tukaangalia sana kuwaenzi wasanii wetu. Visiwa hivi palikuwa na wasanii wengi sana na wasanii hao wamejaribu ku-*preserve* utamaduni wetu kwa siku nyingi. Wako wafinyazi hapa, wako watunzi hapa, wako watunzi wa nyimbo za taarab, wa mashairi, wasusi. Leo ususi ambao wizara hii inauhusu sana, ususi wa Zanzibar unatoweka, haidhuru tunakubali kwamba dunia inabadilika, leo badala ya kuwa na mkeka una mazulia, badala ya kuwa na ungo una mabeseni…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, una dakika mbili.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Lakini nashukuru sana, sana ndugu zangu wa Pemba wamejaribu kufanya makumbusho ya kuweka vifaa vya zamani. Leo utakuta kuna hando, chano, mkeka, kishibaka, kikamshi, kijana wa leo hajui kikamshi wala halijui hando na vile vyote vinapotea. Kwa hivyo, naiomba wizara hii kumbusho lilofanywa Pemba na liwekwe na Unguja ili tuweke vifaa vyetu tulivyokuwa tunatumia. Utamaduni wetu tunashukuru, mimi nashukuru kitu kimoja watawala wote waliotutawala Zanzibar hawakutunyanganya utamaduni wetu, wametunyanganya ardhi, wametunyanganya elimu, wametunyanganya utajiri wetu, lakini utamaduni wetu bado tunao wenyewe. Na tunao wenyewe utamaduni wetu hivi leo sote hapa tuliokuwepo hapa kila mmoja akifa jamaa yake utakuta anazikwa na wote, utamaduni ule hatukunyang'anywa sisi. Utamaduni wetu hatukunyang'anywa tumenyang'anywa mambo mengine tu. Kwa hivyo, lazima utamaduni wetu tuutafute na tuuweke na tuujue kwa ajili ya vizazi vijavyo. Kwa hivyo, hawa waliokuwa wanashughulikia mambo ya utamaduni wetu lazima uwe *preserved*.

Kwa mfano tunasahau sana watamaduni wetu, mfano utasikia kuna matamasha hapa na wanazawadiwa wasanii, lakini wasanii wamesahaulika hawajuulikani kama kina Juma Sheha Mkoa, kina Sami Haji Dau, kina Hija Saleh, Mwapombe Hiari na wengine hawafahamiki. Kwa hiyo, wizara hii ikae kitako iwatafute wasanii wetu wa zamani walikuwa wapi, na walifanya nini na nini. Kwa hivyo, yale yote ambayo ningelishauri yakawa *preserved* na ku-*commercialize culture* ni kuweka nyumba zetu za historia na tukawaambia wenzetu wazitunze.

Mhe. Mwenyekiti, ningeliomba wizara hii ikafanya utafiti, utafiti ambao nasikia sina hakika kuna baadhi ya nchi waliofanywa watumwa wamelipwa fidia. Nina hakika Waswahili wa Zanzibar kama kuna taifa lolote duniani wamewafanya watumwa na dalili zipo za kufanywa sisi watumwa. Kwa sababu kuna njia ya utumwa iliyotoka tangu Congo mpaka Zanzibar. Imetoka Congo, imepita Kigoma, imepita Tabora, imepita Singida, imepita Bagamoyo mpaka Zanzibar na alama zipo za Waswahili wa Zanzibar kufanywa watumwa. Sasa kama na sisi tumefanya watumwa na kama kuna dola lolote duniani wamefanya watumwa wazee wetu watulipe fidia, na alama za kufanya watumwa sisi zipo. Kuna minyororo pale ya Waswahili wametiwa na hakuna katika minyororo ile picha zile za mnyororo hapa Mkunazini lakini wale waliotiwa minyororo wote hakuna Muhindi wala Muarabu wala nani aliyetiwa minyororo, utaona picha za Waswahili watu pale. Sasa kama kuna dola imetufanya watumwa lazima wizara hii ifanye utafiti, lazima koo zile zitafutwe na zilipwe fidia…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia wala sina matatizo. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia salama na uzima wa afya na leo hii tukaanza mwezi mtukufu wa Ramadhani, nawatakia Ramadhan Kariimu kwa wote.

Baada ya hapo vile vile nampongeza Mhe. Waziri, ambaye amewasilisha hotuba hii kwa mbwembwe na madaha mingi sana pamoja na uzuri uliokuwemo humu katika kitabu hiki. Lakini alikipamba kwa usomaji wake na

sisi sote tukapeleka akili yetu na kumsikiliza kile anachokizungumza, hongera sana Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kukuchagulia *midfielder* wa zamani wa timu yangu ya *Small Simba* kuwa Katibu wako, najua kwamba michezo imefika kwake na lengo letu ni kwamba michezo Zanzibar inakuwa hususan mpira wa miguu. Kama unavyofahamu Mheshimiwa, mpira sasa hivi imekuwa kama kichwa cha mwendawazimu kwa Zanzibar, *league* haifahami, *league* ina timu karibu 32, lakini nchi yenyewe ina watu 1,200,000 ni maajabu makubwa sana. Lakini huo ni muundo mzima wa Chama cha Mpira cha nchi yetu, kwa matumaini yangu waziri ni msikivu na Katibu halikadhalika ni mchezaji mzuri alikuwa na anaumia na mpira, nafikiri atafanya maarifa rasmi kuhakikisha kwamba mpira nchi hii unachezwa na unarudi katika hadhi yake ile ya kawaida. Kama hapo nyuma kulipokuwa na timu za *Small Simba, Black Fighter*, Malindi, Vikokotoni na nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuchangia pamoja na hotuba yako nzuri mimi nitakamata pale kuhusu uwanja wa Gombani kuwekewa *tartan*. Kweli kulikuwa kuna Kampuni *Novel Investment Company* katika maelezo yaliyopita hapa ulitwambia kwamba katika matengenezo ya uwanja ule limepishana kidogo ikawa ule uwanja haujamalizika na ikapelekea kupata hasara ya wizara yenu karibu milioni 2.5. Sijui haya yamekuja vipi, naomba utakapokuja kufanya majumuisho utueleze kwa makini zaidi, kwa sababu ni moja ya masuala ambayo yalielezwa kwa muda mrefu katika kikao hiki, lakini ikawa jibu lake bado halijatolewa vizuri na tukaambiwa kwamba imeingia hasara serikali ya milioni 2.5 na imeokoa milioni 64. Sasa je, baada ya hayo, sijui mmechukua hatua gani juu ya wizara ile na mikataba inasemaje.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye Shirika la Utangazaji (*ZBC*).Nakumbuka kwamba kulikuwa kuna rai nzima Zanzibar kutoka katika *analogy* kuingia katika *digital*, na kwa nia safi kabisa tukaingiza Kampuni moja ya *AGAPE* kuingiza vingamuzi katika nchi yetu. Kusema kweli lile jambo lilinisikitisha mpaka dakika hii hata ukiuliza kwa wawakilishi ukiwauliza ni wangapi wanaotumia vingamizi vya *ZBC* vilivyotolewa na *AGAPE* hawafiki hata watano. Kwa maana tayari mradi ule *totally* tumefeli na hatujui tumefeli vipi na ule mradi umetumia gharama nyingi kwa mawazo yangu, nitaomba utapokuja Mhe. Waziri, uniweke wazi ule mradi umefikia gani mpaka dakika hii, kwa sababu sisikii watu kwamba wanaangalia kingamuzi cha *ZBC*, wengi wao nafikiri wanatumia vingamuzi vya televisheni nyengine kama *Azam TV* na vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kuna changamoto nyingi sana katika *ZBC*, kuna hili suala zima la ajira kwa hawa vijana wanaojitolea kufanya kazi muda mrefu katika televisheni. Lakini imefika hatua kwamba wale wanaonekana si watu baadae wanakuja watu huko nyuma wanapewa vikaratasi tu wanaajiriwa na hawa ambao wanaojitolea ndio walimu wao. Sijui kuna utaratibu gani wa ajira katika masuala yale. Kwa hiyo, naomba tuangalie hawa ambao wanaojitolea muda mrefu wameshafanya kazi katika taasisi ile, lakini inapokuwa nafasi ya kupatiwa ajira hao huonekana hawafai wanakuja watoto wa mjomba, shangazi kutoka anakotoka anawekwa pale, lakini yule ambaye amejitolea ndio anapewa kipaumbele cha kumfundisha kazi, nafikiri hawatendewi haki kwa kweli.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, katika upande wa televisheni yetu pale tunajua tuna mafundi wazuri sana, na kwa masikitiko tu Zanzibar tumepoteza ma-*camera women* wazuri, *camera men* wazuri, ma-*editors* ni wazuri wa televisheni ile wamechukuliwa na televisheni nyengine kama *TBC* wamechukuliwa wafanyakazi, wamechukuliwa *Star TV*, wamechukuliwa *Azam TV* na pengine na kutokana na maslahi mazima au changamoto zilizopo pale kwa kutosikilizwa au kutokuwa na ushauri katika masuala kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kiwango cha ubora, siku zote tunajivunia kwamba televisheni yetu ni ya pili katika Afrika kwa televisheni ya rangi, lakini ubora wa *TV* yetu kila siku ukienda baada ya kuendelea mbele unakuwa unapungua zaidi. Imekuwa tunarudi kule kule katika *TV* za *black and white*, rangi haifahamiki, sauti haitambulikani, mara minazi tu, samahani, nafikiri Mheshimiwa, hilo uje uturidhishe tatizo ni nini hasa. Pamoja na fungu kubwa ulilopewa au pengine fungu dogo basi uiombe serikali kama ni tatizo la fungu ikuongezee wewe kwa sababu huu ni mdomo wa serikali. Televisheni, redio ni mdomo wa serikali hususan hizi za taifa, nazungumzia *ZBC* ni midomo ya serikali ukiyasemea yale mambo yote ambayo mazuri.

Leo hii imekuwa televisheni nyengine au zile nyengine zina nguvu zaidi kutangaza vizuri zaidi na watu wanazi-*support* zaidi kuliko hii. Kwa hiyo, hata kuwapotosha watu wetu wengi sana wanapotoshwa na televisheni nyengine badala ya *TV* yetu kuiweka sawa. Mfano mdogo hata Kisiwa cha Pemba sasa hivi muonekano wa *TV* ya Zanzibar ni mdogo sana, kule watu wengi wamekwenda katika vingamuzi vya *Azam TV*, nafikiri na *Star TV* kulikoni vingamuzi vya Zanzibar hata upatikanaji wa *ZBC* Pemba umekuwa mgumu. Sasa kama Zanzibar basi na wao wafaidike na upatikanaji wa televisheni yetu Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuhusu suala la posho, mara baada ya Baraza la Wawakilishi kuanza kulipa hizi posho zenu stahiki za kuonesha vipindi *alive* kidogo zimekuja changamoto nyengine mpya ya watu kubaguana katika hili, nani anastahiki kupewa, nani hastahiki kupewa. Kwa hiyo, inaleta hata kushusha ari na morali ya wafanyakazi wetu, leo tunawaona wafanyakazi hapa waliahidiwa mpaka kupewa *uniform* hawa, lakini leo hii ni hao kwa hao na hakuna *uniform*, hata kwenye maposho wengine wanatolewa. Nafikiri Mheshimiwa, hilo unajua, wewe ni msikivu kupitia wewe na Katibu wako mtatwambia vizuri ili tukija hapa mtutosheleze kwamba haya matatizo yaliyokuwepo mtupe njia gani yakuweza kuyaondoa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, masikitiko zaidi yako kwenye posho kwa hawa wapandaji wetu wa minara katika vituo vyetu, hawa jamaa wanafanya kazi ngumu sana, kazi za kujitoa roho kwa sababu wanapanda mnara mrefu sana, lakini posho lao halipwi, imekuwa kilio cha muda mrefu jambo hili. Na hili jambo la kupanda mnara sio kila mtu anaweza, ni watu maalum waliojitolea kufanya shughuli hizo, imefika wakati kwamba hawa watu hawalipwi posho lao. Nafikiri Mhe. Waziri, tunakutegemea sana una nia kabisa ya kuibadilisha televisheni na shughuli zote za Zanzibar katika shughuli hizi za habari na michezo, nakuamini hilo suala utalisikiliza na kulifanyia ufumbuzi haraka iwezekanavyo, *Inshaallah* tupo pamoja katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine la masikitiko zaidi hata usafiri, vyombo vya usafiri kwa upande wa *ZBC* vimekuwa changamoto kubwa sana, leo hii sisi kama viongozi tunakuwa na *functions* zetu kama hujatoa gari yako kwenda kumchukua mwanahabari basi huwezi kupata habari, na ile ni taasisi ya umma.

Kwa hiyo, ufanywe mpango maalum kuwezeshwa ile juu ya zoezi zima la kupatikana angalau ziwepo gari panapotokea tatizo angalau upige simu tu pale kwamba kuna kazi yangu hii na hii basi baada ya muda watolewe watu waje pale wafanye ile shughuli ili waioneshe jamii, kwa sababu televisheni inafika mbali sana. Vyombo vile vimekuwa chakavu au pengine havipo kabisa, lakini hata vile vyombo vyenyewe vya kufanyia kazi kama *camera* zimekuwa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nazungumzia suala zima la vifaa, watendaji wetu hawapatiwi vifaa, kompyuta mpakato hawana, kwa sababu sasa hivi ni utandawazi inatakiwa kila mtu pengine katika waandishi wako wawe na *laptop* angalau za kuweza kuwarahisishia shughuli zao za kazi, *camera*, *recorders* zile wanashindwa kuwa nazo, siku hizi mtu anakuja kurikodi kwenye simu mambo ambayo si wakati wake sasa hivi. Sasa hivi tunakwenda kwenye *digital*, kwa

hiyo, *automatically* na sisi wenyewe tujipelekeshe huko huko kwenye *digital* hasa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala zima la uwanja wa *Mao Tse-Tung*, ulikuwa ni uwanja mmoja uliokuwepo katikati ya Zanzibar kwa lengo safi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kuuboresha, ulibomolewa ule uwanja nafikiri kabla ya kujitayarisha. Ilifika wakati hapa mechi za *league* ya nchi hii inachezwa Ndijani, inachezwa Bweleo pahali ambapo hazifiki hata ile hadhi, hakuna kama huku tunacheza *league* ya nchi. Kwa haraka ya uvunjaji wa uwanja ule wa *Mao Tse-Tung*, lakini mpaka dakika hii bado ndio kwanza wanatwambia serikali imeingiziwa pesa kwa ajili ya ujenzi huo.

Kwa hiyo, tunaomba basi haraka iwezekanavyo angalau kama kweli tunataka tupige hatua lazima tuwe na vyanzo vingi vya michezo, japokuwa wamesema kwamba mtajenga viwanja kila Wilaya ni jambo zuri sana, mimi nalipongeza sana kwa sababu mnaonesha wazi kwamba mnataka michezo ichezwe.

Lakini haya yasiwe kwenye maandishi tu, maandishi yameshatosha, sasa tunataka vitendo, hiyo ahadi ya kusema kwamba mtajenga viwanja katika kila Wilaya tunataka haraka iwezekanavyo, mara baada ya kupitisha bajeti hii basi tuone angalau ule mwanzo unaanza wa kujenga vile viwanja angalau watu watasema sasa kweli tunataka tupige kasi katika michezo twende na wazo zima la “Hapa kazi tu” liwe linaonekana katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ningependa kuzungumzia juu ya suala zima la kushuka soka la Zanzibar. Ni kweli soka limeshuka na nimeshazungumzwa mwanzo kwamba migogoro isiyokwisha. Kuna watu wamekuwa-*remoted* katika Chama cha Mpira Zanzibar, ndiyo maana inapelekea soka la nchi hii kushuka. Nafikiri Mhe. Waziri, unatakiwa uwe mkali sana katika hicho ili kuhakikisha kwamba kanuni na sheria zile ambazo zilizowekwa kwa ajili ya kuendesha kile chombo zinafuatiliwa, imefika *time* sasa hivi hata watendaji wamekuwa hawazungumzi lugha moja, huyu anasema twende kushoto, huyu mwengine anasema twende kulia, nafikiri hatuwezi kwenda hivyo. Nafikiri Mhe. Waziri, ungelichukulia jitihada binafsi juu ya chombo kizima cha *ZFA* Taifa kuanzia Mwenyekiti wake mpaka Makatibu mpaka na Watendaji wale tuangalie hawa wanautakia nini mpira wa nchi hii.

Mhe.Mwenyekiti: Mheshimiwa, naomba uielekee *microphone* yako.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni nini wanautakia hatma ya mpira wa nchi, kwa sababu kila mtu anapenda mpira wa nchi hii, lakini walio wengi kabisa wametokwa na mapenzi ya mpira wa nchi hii baada ya kuona mwenendo mzima wa mpira ule, tokea kuanzia kwenye viwanja, marefarii na hata hao viongozi wa mpira na hawa ndio *source* kwamba mpira wa nchi hii kuanguka. Kwa hivyo, kama unavyoona mpira ni moja kati ya ajira kubwa sana duniani, watu wengi sana wanatajirika katika mpira na sisi tulikuwa tuna hamu sasa hivi wenzetu wa Tanzania Bara wameweze kumtoa Mbwana Samata na sisi hapa Zanzibar tuwatoe basi.

Kwa sababu kama nilivyosema kwamba kwa vipaji sisi na wenzetu Tanzania Bara sisi tuko juu zaidi, yaani kuna vipaji zaidi Zanzibar kuliko hata Tanzania Bara, lakini wenzetu wamejikaza, wamejidhatiti na wamefanya ari kwa kuonyesha kwamba wanafungua *academy* kwa wingi, mpira unachezwa na sasa hivi tumeona baada huyu kwamba kuna mwengine Faridi ameenda Spain na amefudhu majaribio, kwa hiyo, na ile hamu na Zanzibar nao iweze kutoa wachezaji kama wale ili kuweza kuisaidia mapato ya nchi yetu, najua kuna Diaspora au namna nyengine watalipa kodi wale na Zanzibar itafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Waziri katika suala hilo usimuonee mtu haya, uvae uso wa bati usoni kwako kuhakikisha kwamba mpira unachezwa, tumeshachoka siku zote kusikia migogoro ya mipira, kila siku ukacha mara Mahakamani, mara kesi hivi, mara kesi hivi, kwa kweli mnatuumiza. Sisi kama wapenzi wa mpira mmetutoa hata hamu ya kwenda kuangalia mpira, sasa hivi akili zetu zote zimebadilika zimekuwa kwa Uingereza, tunaangalia Uingereza, Spain wakati sisi tunavyo vyetu vizuri zaidi hapa.

Hapa Mheshimiwa, kulikuwa na wachezaji wazuri hata kuliko hao unaowaona wewe akika Zedani hapa, kulikuwa kuna Abdulawakati Juma eh, *Super Star*, yule alikuwa anacheza mpira katika hali ngumu, umeona lakini alikuwa hodari kuliko hata yule ambaye anaanza tokea *academy* anaanza kuzaliwa miaka saba, nane anacheza mpira mpaka pale, walikuwa akina Juma Bakari Kidishi ndio wale pale sasa hivi ukimuona Rooney na Juma hawana tafauti, lakini yule kazaliwa Uingereza kawezeshwa akawa vile, lakini wetu sisi hapa Zanzibar katupwa tupwa tu. Kwa hiyo, lazima tutafute njia mbadala muarubaini wa mpira kwa kuonyesha kwamba mpira nchi unachezwa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo yote naona Mhe. Mwenyekiti, anataka kunambia muda, sasa basi naomba nisiendelee sana, niishie hayo, mchango wangu mimi ni machache zaidi, lakini nitaona raha zaidi utakapokuja Mhe. Waziri, unambie mlolongo mzima wa *AGAPE* ilianza anzaje hii na ilikuwa na

sifa gani hii kampuni kuweza kushinda *tender* ya kusambaza vingamuzi au kuendesha vingamuzi kwa televisheni Zanzibar na zilikuwepo kampuni ngapi ambazo zimeshindana nazo na zina sifa gani hata hizo zikashindwa hata huyu *AGAPE* akapewa nafasi ya kusambaza vingamuzi Zanzibar, lakini hadi dakika hii vingamuzi vyenyewe havifahamiki, havina ubora kwa kweli tumeingia hasara, hili kwa Mhe. Waziri, hili moja mimi sitoliachia, ila haya mengine yote ninaunga mkono asilimia tisini na nane lakini asilimia mbili yangu iko katika suala zima la *AGAPE,* naomba utakapokuja Mheshimiwa unijuilishe. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Abdalla Diwani, kwa mchango wako, anayefuata Mhe. Mohammedrazza na Mhe. Simai, ajitayarishe na Mhe. Panya.

Mhe. Mohammedraza Hasanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliweza kutupa pumzi hii na kutufikisha mwezi mosi ya Ramadhan, maana tumeanza leo *Alhamdullillahi,* Mwenyezi Mungu atujaalie atupe afya sote Wazanzibari na Watanzania kwa pamoja ili tuweze kufanikisha thaumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niichukue nafasi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na hotuba yake nzuri iliyokuwa na hekma, busara na usikivu pamoja na watendaji wake. Nichukuwe nafasi hii vile vile Mhe. Mwenyekiti, kumshukuru Mhe. Waziri hasa kwa umaarufu wake anaitwa 'Maalim' pamoja na watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi waliotangulia wamegusa sehemu mbali mbali ya michezo, lakini lazima tutafute njia ambayo ya kuweza kutatua matatizo ya michezo, maana yake unasema; *we have a problem, we have to find a solution,* halafu unasema *what is next*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, nimpongeze Makamo wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Mzee wangu Balozi Seif Idd. Mhe. Mwenyekiti, naliambia Baraza hili kukosekana viongozi hawa wawili katika miaka mitano iliyopita kwa kutosimamia michezo, leo Zanzibar ingelikuwa kabisa hata mchezo wa mchangani hakuna. Kwa sababu Wizara iliyopita ilikuwa haina uwezo wa jambo lolote lile. Kwa hiyo, viongozi wawili hawa kwa awamu Dkt. Shein na Balozi Seif Iddi, ndio waliofanikisha hali hii tuliofikia hapa kwa michezo, bila ya mikono yao kwa awamu iliyopita Zanzibar ingelikosa kabisa michezo, kwa sababu ya ubinafsi umimi, umimi, umimi na choyo, fitana na majungu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi namuomba Mhe. Waziri wa Habari kwamba, naamini pamoja na watendaji wake akiwemo Katibu Mkuu wa Habari na Michezo ndugu yangu Omar King kwamba, naamini wana uwezo mzuri, ni wasikivu na wanaweza kutufikisha hapa tunapotaka kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii nitasikitika sana kuona kwamba bado michezo itakuwa ya kusuasua kwa sababu nina sababu zangu. Mhe. Waziri ni Maalim Rashid, hilo peke yake 'Maalim' maana yake ni Mwalimu, halafu ana *midfielder* mzuri aliyekuwa Katibu Mkuu alichezea timu ya Taifa ya Zanzibar na timu ya Taifa ya Tanzania Omar King, alikuwa ni *midfielder* mzuri. Kwa hiyo, ninaamini kwa uwezo wake Omar King ataweza kuwatumia wachezaji wake wote wastaafu ambao alikuwa nao akina Mfaume, kina Abdulwakati, kina Njunju na wachezaji wenzake, naamini Wizara hii sasa inaweza kuleta miujiza ya kuweza kuendeleza michezo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii imepata viongozi, ninachoomba kwamba michezo, utamaduni, utalii, sanaa zote hizi zitafanikisha kama watakuwa tayari na wao kuwa-*deliver* wananchi na sisi kama wadau wa michezo tuko tayari kutoa misaada yote kwa Wizara hii inayohusika, tuna imani sana na Wizara hii na hawa watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vyetu hivi vinavyohusika vya *ZBC* vya habari, redio na sehemu nyengine, nichukuwe nafasi hii kuvipongeza vyombo vyote vya habari vya Serikali na vya binafsi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutuletea taarifa mbali mbali. Niipongeza *ZBC* kwa ushujaa na utendaji wao, mazingira magumu kwa kazi wanayoifanya lakini wamekuwa na uzalendo na uchungu wa nchi yao. Nampongeza Mkurugenzi Mtendaji ndugu yangu Mitawi na watendaji wote wa *ZBC* kwa kazi kubwa ya uzalendo wanayoifanya katika kuleta maendeleo na habari ambazo zenye uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Waziri, sasa hivi tumeingia kwenye soko huria ya habari. Ni uzuri sisi kama Wawakilishi na Wabunge kama walivyokuwa wenzetu kule Bara *ITV*, *Channel Ten*, kunakuwa na *programme* maalum ya Mwakilishi na Mbunge kutoa mchango mdogo ikaonekana ni jambo gani ambalo tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa hivyo, wapewe fursa Wawakilishi na Wabunge ambao wanaweza kuchangia wakaonyeshwa maendeleo yao katika majimbo yao katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, hiyo peke yake ni *incentive*, una *programme* yako umeifanyia kutekeleza Ilani ya Chama, waruhusiwe vyombo vinavyohusika wachangie.

Mhe.Mwenyekiti, sasa hivi kule wenzetu Bara kuna siku maalum ya Mwakilishi na Mbunge, wanapeleka taarifa zao unalipia laki mbili, laki tatu, wananchi wanajua, sasa hii italeta changa moto, *it will be a challenge for us*, Wabunge na Wawakilishi katika kuchangamsha kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara kwa kupitia vyombo vyake hivi vikatoa hiyo nafasi ili ikapata kujiwezesha. Unajuwa Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine vitu vidogo vidogo hivi kama hujaviweka kwa kutowa *incentive* kwa vyombo inakuwa ni vigumu sana.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara iamuwe kuweka kipindi maalum cha Wawakilishi na Wabunge tutachangia zitoke taarifa kwamba Mwakilishi na Mbunge katika jimbo lake kuna moja, mbili, tatu, sasa hiyo itafikisha *message* na itakuwa kama ni *challenge* kwa Wawakilishi wote na Wabunge kwenda katika majimbo yao kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza hili suala la *AGAPE* na *ZMUX*. Mimi Mhe. Waziri, nakuomba sana Mhe. Waziri, pamoja na kaka yangu Katibu Mkuu Omar King. Naamini sijui kwa Mwenyezi Mungu, naamini hii bajeti mlikuwa mshaikuta kwa sababu ya muda wa uchaguzi wetu tuliokuwa tumefanya.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kuomba tu Mhe. Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wake hili suala la *AGAPE* ni zito sana, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kama sikosei imeshatumia karibu gharama zake dola milioni nane. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Wizara hii ya Habari wakati wa Awamu ya Sita. Kwa hivyo, nina hakika na ninaelewa kwamba hili suala la *AGAPE* na hii *ZMUX* ni mambo ambayo ni mazito ningelimuomba Mhe. Waziri, nakuomba uwe msikivu, mwenye uchungu na nchi utizame haya mambo. Vitu hivi Mhe. Mwenyekiti, ni vikubwa, hii unayoiona hii *ZBC* wakati mwengine inayumba picha na mambo mengine, inatokana na matatizo ya *ZMUX*. Sasa halafu watuambie katika *programme* hii ni vyombo vingapi tuliokuwa tumefaidika na tuko wapi na tunafanya nini, kwa sababu asilimia ishirini iko kwenye Wizara, asilimia ishirini iko kwenye *ZBC* na *sixty percent* wanayo Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninataka nikwambie mwaka uliopita nilizungumza kwenye bajeti. Wakati *AGAPE* inaingizwa Makatibu Wakuu hawakushirishwa, lakini kwa sababu ya Rais wetu mpendwa anapenda wananchi wake, hili likasukumwa tu kwa mara moja ionekane ni jambo kubwa lakini matokeo yake Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hili jambo litatu-*cost* sana, dola karibu milioni nane. Kwa hili *AGAPE* na *ZMUX* hawa, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri,

ninakuomba sana kama inawezekana ufanye utafiti ningelikuomba nitakusamehe wala usije ukanijibu katika hili, lakini nakuheshimu sana Maalim pamoja na viongozi kwamba bwana hili hakuna kitu humu ndani, dola milioni nane, kwa hiyo, ningelimuomba na kwa sababu nayajua yote na nilikuwemo mule ndani, ilipowekwa huu mkataba Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi wa *ZBC* hakushirikishwa kabisa katika utaratibu mzima wa uwendaji lakini wao walitumiwa tu kuanzisha hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, aliitwa Mkurugenzi *ZBC* tulikuwepo kwenye kamati, tukamuuliza kasema hakuhusishwa kabisa kaambiwa tu atie saini. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba tu kwamba tuko hapa kwa niaba ya wananchi na tuko kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matatizo yako mengi lakini tunapoona ubadhirifu kama huu mkubwa si vibaya ushauri wangu ikaundwa Kamati Teule kama kuna haja ili ikaonekana kitu cha wazi, ningelimuomba sana Mhe. Waziri, namstahi sana Maalim Rashid. Na Mhe. Rais alisema jamani kama huna jawabu ya uhakika ni bora ukasema nipeni muda ili nilifanyie kazi. Mhe. Rais, amelitoa tamko hilo kwa Mawaziri; kwamba ningeliomba tu kwamba hili lifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kupitia Wizara hii ili suala la *TFF*. Suala la *TFF; TFF* si suala la Muungano, *TFF, ZFA* ni nchi mbili huru zimeungana tukapata Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndio maana leo hapa tunajadili Wizara ya Michezo. Kwa hivyo, ningeliomba Mhe. Mwenyekiti, kupitia Wizara hii, ili tuulize uhalali wa *TFF* kuubeba kama ni Tanzania uhalali huu kaupata wapi *TFF*, unaposema *TFF* maana yake ni Zanzibar, sasa huwezi leo *TFF* ukachukuwa uhalali wako wa Tanzania Bara au wa huko Tanganyika ukasema wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, sasa lazima tuwe na hoja na tujenge hoja, mimi nafikiri kuna haja Wizara ikapeleka mashtaka yake kwenye *FIFA* kwa sababu inawezekana na *FIFA* wamedanganywa, leo unaiita *National Team* ya Tanzania hakuna hata mchezaji mmoja wa Zanzibar, *how comes?* Mhe. Mwenyekiti, timu ya taifa inachaguliwa hakuna mchezaji mmoja wa Zanzibar, ina maana mnataka kutuambia hakuna mchezaji mmoja wa Zanzibar mwenyewe uwezo wa kucheza, halafu unasema '*National Team of* Tanzania', afathali usiseme Tanganyika, sema *National Team of* Tanzania Bara *Mainland. What is the problem?* Kwa hiyo, naomba sana wenzetu tuna utaratibu tukae tujengeni hoja. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wentu *TFF* wanapata mamilioni ya dola.

Mhe. Mwenyekiti: Umebakiwa na dakika moja.

Mhe. Mohammedraza Hasanaali Mohamedali: Mhe.Mwenyekiti, niunge mkono Wizara hii kwa imani yangu leo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini, naiunga mkono asilimia zaidi ya mia moja kwa Wizara hii kwa utaratibu wa watendaji ambao mliokuwa na naamini wanaweza kubadilisha sehemu nzima ya Wizara. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe.Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi nianze kuchukuwa fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, kwa hotuba nzuri, amejiandaa, yeye ni mtaalamu, mzoefu na ni rafiki yangu pia, kwa hiyo, nimpongeze kwa hotuba nzuri na maneno mazuri aliyoyatumia katika hotuba yake. Lakini pia nichukuwe fursa hii kumpongeza rafiki yangu, pia ni baba yangu kwa upande mmoja Mhe. Waziri Balozi Ali Karume, kwa mara yake ya kwanza leo kuingia uwanjani kutupa maneno mazito na mazuri kabisa, naamini wengi tumemsikia na tutakuwa tuna hamu naye siku za mbele kumsikia zaidi. Naomba hivi sasa niende katika hoja.

Mhe. Mwenyekiti, jana wakati tunachangia hapa kuna mijadala miwili ilizuka juzi na jana mmoja kidogo mrefu tukatoka nne na nusu. Lakini Mhe. Waziri, jana wakati anamalizia katika kuchangia alizungumza kwamba yeye kama Waziri, yeye hahitaji kuhimizwa, lakini kwa vile na muda uliokuwepo hapakuwa na mabishano mengi, lakini nilichokifanya nikenda nikasoma katiba, kwa hiyo, nikaangalia wajibu wetu sisi Wajumbe wa Baraza, lakini katika eneo moja ambalo linasema kwamba kwenye kifungu (91)(2) kinasema;

"Rais wakati wowote anaweza kuitisha Baraza la Wawakilishi kuendelea na shughuli zake", lakini (2) inasema; "Rais hatakuwa na uwezo wakati wowote wa kulivunja Baraza la Wawakilishi isipokuwa tu kwenye vifungu vitano".

Mhe. Mwenyekiti, najaribu kumaanisha kwamba ukenda kifungu nambari 63(1), kinasema;

"Kutakuwa na Baraza la kutunga sheria ambalo litajulikana kama Baraza la Wawakilishi litalokuwa na sehemu mbili; Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Wawakilishi kwa upande wa pili".

Ninachotaka kusema kwamba, lazima tujenge mahusiano pia ya kuheshimiana wakati sisi ni Wawakilishi wa wananchi na ni kimbilio la wananchi; kwa hiyo, ni muhimu Mawaziri wakati mwengine wanapochukuwa ushauri wetu na tumetoa maoni yetu basi maneno yao pia yaje kama tunahimiza basi na sisi pia tunahimizwa na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Sasa nikenda na wenzangu moja kwa moja kwenye hoja ya mchango wangu wa leo kwamba hii Wizara ni ndefu Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niseme kwamba Wizara hii inanikumbusha yale mambo niliyosoma kwenye historia kwenye *evolution*, kunaanza na *homo; homo erectus, homo sapiens, homo habilis,* yaani naona kama inakwenda nyuma hii wizara. Kila mwaka ukienda ukirudi inazidi kunyonywa na kuchukuliwa.

Nikiangalia nyuma tangu naijua wizara hii ilikuwa na visiwa, wizara hii ilikuwa na mahoteli; *Africa House, Zanzibar Hotel*, wizara hii ilikuwa na Hoteli ya Bwawani, wizara hii ilikuwa na *Living Stone House* ambao walikuwa na mpango wa kujenga *museum* pale. Pia wizara hii ilikuwa na Chuo cha Utalii ambacho sasa hivi kinataka kupelekwa *SUZA* nafikiri, sijui kama kitaishia huko huko.

Sasa ninachotaka kusema kwamba wizara hii katika historia yake naona kama itakuwa inarudi nyuma. Kwa sababu hapa tunasema kuna utalii ambao tunautegemea kwa asilimia kubwa sana katika nchi yetu, *infact* karibu asilimia 80 ya mapato ya *foreign exchange* yanatoka katika *tourism*, na huyu ndiye mlezi na ni kimbilio la wawekezaji wote. Kwa hiyo, hapa lazima serikali iangalie kwa undani kabisa. Waangalie wapi tumetoka, wapi tupo na wapi tunataka kwenda. Kwa sababu unaposema kwamba *tourism is the backbone of economy* ya Zanzibar, lakini ukienda katika sura ya wizara hii ukiangalia Kamisheni kutoka chini jengo lenyewe na watu wenyewe na huduma wanayoipata watu wamefulia, haiendani kabisa na hiyo *tourism* yenyewe inayozungumzwa, ni tofauti ukiingia katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais unajua, ukienda katika Ofisi ya Wizara ya Fedha unajua, lakini ukiingia katika Wizara ya Utalii na Kamisheni ambayo ni *policy makers* hawaendani. Kwa hiyo, hapa inabidi kwa ujumla serikali inabidi iangalie hasa kuhusu suala hilo na sizungumzi kwa kubahatisha, nazungumza kwa sababu ninafahamu.

Pia nilitaka nichangie katika eneo moja kwenye wizara hii ni suala la Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Baraza la Sanaa na Filamu ya Utamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, tunayo makumbusho yetu pale Beit el Ajaib na kwengine, lakini ukiangalia makumbusho haya na historia tulikotokanayo lazima tuangalie katika hii historia ya nyuma, na lazima yaboreshwe na kutokana na huko tunakotaka kwenda.

Pia kuna umuhimu kwa wizara hii kuanzisha *Modern Museum* (Makumbusho ya kisasa). Kwa mfano, niliwahi kuzungumza katika Baraza la Biashara,

Zanzibar ilikuwa inatumia gari za ZNZ, tulianza na ZNZ 1, ZNZ 2, ZNZ 3 gari ya mwisho iliyotembea ZNZ ukichukua kile kibao chake ukipeleka *museum* utasema kwamba hii gari ndio ilibadilishwa namba ya mwisho. Hiyo ni sehemu ya historia yetu.

Leo ukilichukua joho la Mhe. Spika ukiamua kulibadilisha ukipeleka na historia yake kwenye makumbusho yetu baada ya miaka 20 itakuwa na thamani yake, ina uwezo wake na watu inakuwa ni sehemu ya historia yetu.

Kwa hivyo, nashauri serikali iangalie kujenga makumbusho ya kisasa itafute eneo, najua mimi ningependa sana eneo kama la *Eacrotanal*, lakini waangalie wapi watapata eneo ambalo litakuwa na *modern museum* wakaunganisha pia na *art*, kuna *modern art* pia ili vijana wenye *talents* zao waweze kuzipeleka, pia watu waweze kutembelea.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hilo hilo siku hizi vijana wengi wameingia katika masuala ya sinema hii michezo ya kuigiza na muziki ambao unaitwa muziki wa kisasa. Kwa kweli vijana wetu wa Zanzibar wapo wengi na vikundi vingi wamejipanga, tatizo lao ni kujitangaza, kupata fursa kuweza kujionesha nini wanaweza na cha tatu ni fedha. Haya nayajua, najua unaniangalia kwenye picha pale TV kwa hiyo nasema hivi vitu navirudia; fedha, kujitangaza na kufanya eneo la tamasha lao. Sasa nini tufanye.

Mimi namshauri Mhe. Waziri jambo la kwanza aitishe mkutano, *Zanzibar Conference for Local Artists, Music and Cinema*, tena tusifanye kwa mikoa tufanye moja kubwa kama hawa vijana waliokuja hapa kwa Mhe. Mwenyekiti, watu wako kutoka Chukwani tena hongera sana, najua huko juu wananisikiliza wanafurahia kule. Kwa hiyo, hapo atapofanya hivyo ndipo tutaweza kujua kuna hizi *talents* tuweze kuwaangalia na kuwasikiliza, siku ya kwanza tuanze na *conference*, siku ya pili mazungumzo, kwenye majumuisho siku ya tatu tamasha. Eneo gani lifanyike tuko tayari kusaidiana tutafute sehemu tafauti tuangalie wapi tutafanya, wapi tutapata fedha na jinsi gani ya kuli-*promote* likawa, ili tukaweza kujua. Mimi tayari namhakikishia Mhe. Waziri kwa niaba yako Mhe. Mwenyekiti, nimezungumza tayari na Meneja wa Diamond anaitwa Bab Tale yuko tayari kuja kushirikiana na sisi kuja kutoa somo na jinsi gani yeye alivyoanza mpaka alipofika kuweza kusaidia na vijana wa Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akiwa tayari wote hawa watu naweza kukuunganisha nao ili kuweza kuwapata.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala la jimbo langu kidogo, jimbo langu ni kama eneo la Jimbo la Malindi la Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi,

Mawasiliano na Usafirishaji tuna maeneo tafauti ya kihistoria. Ninalo eneo la kale kule Unguja Ukuu, tuna bahari, tuna visiwa, tuna mashamba pia tunaunganisha na majimbo mengi jirani. Nina majimbo karibu sita, kuna Fuoni, Paje, Chwaka, Uzini na kwa upande wa Mwera nipo pia na Mhe. Mihayo Juma N'hunga. Sasa hivi visiwa sina hoteli hata moja kubwa ya *three stars* kwendea juu katika jimbo langu lakini nina rasilimali ya kutosha.

Kuna vyuo vikuu, tuna taasisi nyingi za serikali, ninazo Afisi za Mkuu wa Mkoa, Wilaya, Makao Makuu ambayo inakuja kujengwa mji mpya lakini sina hoteli hata moja ya wawekezaji. Naomba Mhe. Waziri alichukue hili na jinsi katika maeneo ambayo tunataka tuyajenge anisaidie kuunganisha upande wa kusini kwa upande wa Unguja Ukuu na Kikungwi tuweze kuangalia moja kwa moja. Na upande mmoja pa kutumia fursa hii kwenye mikoko ya kisiwa cha Uzi kukawa na wananchi, wale kidogo hawapendi utalii utakaozidi kupita kiasi, wanataka uwe na mila na desturi ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, ile mikoko lakini ni eneo ambalo tunaweza tukaanzisha pia *excursion* mpya, Zanzibar tunakosa kuwa wabunifu, tuanzishe *excursion* mpya ambayo tutapita katika mikoko ya Uzi tukaunganisha pamoja na upande wa Muungoni na Jozani kwenye bahari, ili watu wanapotoka Paje, Jambiani na Bwejuu wapate fursa ya kuona *excursion* mpya ambayo tutawaunganisha pamoja na *excursion* ya kwenda Kizimkazi pamoja na *dolphin tour,* itakuwa ni *day trip,* wanapiga *dolphin* unakuja Uzi, Jozani, unaangalia maeneo unapiga *picnic,* unaona nchi yako, kabla ya kwenda Kizimkazi unaondoka zako unarudi. *Full day* tunauza mpaka Dola 120.

Mhe. Mwenyekiti, upande mmoja mwengine nataka nizungumze kwamba Mhe. Waziri inabidi yeye sasa kwanza nimshauri, anapokwenda kukaa kwenye Baraza la Mapinduzi na wenzake bora afanye kama amechanganyikiwa, anakuwa kama mwendawazimu. Kwa sababu kama hajapiga kelele, hajapigana mambo yake hayatakuwa, *the only* yeye aende asiende kama waziri wa kawaida apambane kweli kweli, na hili namwambia kwa sababu mimi nimeshazungumza sana kwenye Baraza la Biashara, tunahitaji *public beach* Zanzibar kwa Wazanzibari. Visiwa vyote vimetolewa Wazanzibari leo sikukuu yao biriani na pilau waende wapi? Nungwi yote imetoka, Chwaka imeshakwenda, Mangapwani *traditional* watu wote washakwenda *picnic*, wazee wangu wote wa zamani, kaka zangu nyote mshakwenda maeneo hayo, leo hakuna Mzanzibari kwenda akakaa akaenda kwenye hoteli anaonesha muziki wake anaambiwa aondoke atakera wageni, ni kweli atasumbua wageni sasa aende wapi.

Mimi nashauri *public beach* ya Kama ipo pembeni ya vile vikosi vyetu tutafute utaratibu jinsi gani tutapajenga pale ili Wazanzibari waende. Kwa sababu maji yake mazuri, mchanga mzuri, yana mvuto na Mzanzibari anastahiki kupata bahari yenye mchanga mzuri pia, na yeye akastarehe, msingojee tukawapeleka Fumba kwenye mawe mkasema hiyo ndio *public beach*, *public beach* iliyobakia nzuri ni ya Kama. Kapambane Mhe. waziri kwenye Baraza la Mapinduzi, sisi pia huku nyuma Barazani lete tutapambana mimi ni kinyume, mimi mtu mmoja sawa sawa na watu 20 nitakuunga mkono kwa hilo.

Upande mmoja nataka nizungumze pia katika suala la *regional tourism*, *local tourism* ambayo ni ya ndani na *international tourism*. Nilizungumza suala la upande wa *visa* lakini kwa kweli katika suala la *regional* inabidi tupambane sana katika hili, na nilizungumza suala la magari yetu Wazanzibari tukitaka kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara, *Local tourism* au huo utalii wa ndani ninaouzungumza kutoka hapa kwenda Bara na kwenda kuunga mkono wenzetu kule kwa umoja na Muungano wetu hauwezi kukua, kama mimi siwezi kuondoka na gari yangu kwa utaratibu mwepesi kabisa, sio kuweka *deposit* ya fedha ili niweze kwenda zangu Bara, lazima niwe na haki zangu kama Mzanzibari ya kwenda. Kwa hiyo, hilo Mhe. Waziri namuomba pia alikamate aende akapambane atuletee.

Suala jengine ambalo nimekuwa nalisikia linapigiwa kelele sana ni ajira ya Wazanzibari. Mimi ni mfano mzuri wa Chuo cha Utalii, na Maalim Abass pale kanisomesha, nilichukua *front office* mwaka 1992/1993 wakati kile chuo kilikuwa chini ya *UNDP* pamoja na serikali na Kamisheni ya Utalii. Lakini chuo hiki sivyo kama kilivyo hivi leo, hatuwezi tukawafundisha vijana wetu ukampeleka pahala ambapo uwezo wake wa lugha ya kuzungumza, kujieleza *CV* yake ukatarajia awe *supervisor*.

Naomba niwaeleze, mara nyingi hapa sisi tunazungumza suala la *tourism* na *hotel management*. Hivi ni vitu viwili tofauti, *hotel management* sio *tourism*, *tourism* ni suala jengine kabisa, yaani kwenye *hospitality industry*.

Unapozungumzia *hotel management* unazungumzia *front office*, kuna *house keeping*, kuna *accounts*, kuna *marketing*, kuna *food and beverages*, kuna *maintenance*, kuna *laundry*, hizo zote ni fursa kwa Wazanzibari, ni katika hizi ambazo mtu unaweza ukamfundisha akapata nafasi nzuri kule aingie, na ili uwe *hotel manager* lazima uzunguke na uzijue hizi *departments* zote, unaweza kuchukua zaidi ya miaka 20.

Mimi nawajua hii *Management* ya *Serena Hotel* wao wanafanya *in-house training*, japokuwa mameneja wao wamesoma kwa mfano mwenye *Utalii College* Kenya pamoja na Switzerland, lakini wanawafanyia *in-house training* na hadi kupata Mtanzania kuwa Meneja walihangaika sana mpaka wakapata, watu wengi walikuwa wanatoka Kenya. Kutokana na *standards*, wewe kwenye hoteli huweki mtu kutokana na kwamba huyu ni Mzanzibari au Mtanzania, kwenye hoteli tunaangalia uwezo, na uwezo kwenye hoteli unaweza kufanya masaa 14 unaingia asubuhi unamuandalia mgeni *breakfast*, unamuandalia *lunch*, unamuandalia *dinner*, unarudi nyumbani saa tano, unafanya kazi *seven days a week*.

Kwa hiyo, elimu hii na hii *trend* kwa chuo chetu tutabakia hivi kupiga kelele, na tutaimba wimbo wa taifa vijana wetu wanakosa ajira, kama hatujatengeneza hiki chuo kuweka wataalamu vizuri, na tukakaa kitako kupanga na kukubali kwamba kweli hiki chuo hakistahiki kwa *quality* ambayo tunayo Zanzibar, basi tutabaki kuimba na kulalamika kila siku vijana wetu hawana kazi wako hivi na hivi.

Yapo maeneo ya kazi kweli wanaweza na wanaingia. Mimi mwenyewe nishatuma zaidi ya vijana 300 katika mahoteli tofauti kwenda kufanya kazi, wamo kibao, na kila nikienda wananitambua wananambia Simai ahsante, lakini wale kupanda juu wanahitaji elimu, na nimesema ili vijana wetu wa Zanzibar kwamba tunao vijana kutoka Tanzania Bara wanafanya kazi hapa ili tuunganishe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa bidii ya makusudi, wazungumze na Serikali ya Jamhuri ya Muungano tujenge chuo cha utalii cha Muungano hapa Zanzibar kama kile Chuo cha Sokoine. Wamejenga vyuo vingi vyao vya Muungano kule Tanzania Bara, basi kuna tatizo gani Rais Magufuli na Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein wakajenga chuo cha kisasa Zanzibar tukafaidika sote. Wale ndugu zetu kutoka Tanzania Bara watakwenda kufanya *refresher courses* na wale wa Zanzibar watakwenda kufanya.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi): Dakika tatu ee, ahsante. Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ya televisheni yetu ya *ZBC*.

Kwanza niwapongeze sana *Zanzibar Broadcasting Corporation* kwa kutuunga mkono sisi Barazani na vipindi vyao nimekuwa naangalia mara nyingi sana siku hizi, lakini pia Gazeti la Zanzibar Leo.

Katika gazeti zuri *East Africa* basi Zanzibar Leo ni gazeti moja zuri sana. Kwa nini nasema hivyo? Zanzibar Leo ina *East African* News, Zanzibar Leo lina *Sports, International News*, Zanzibar Leo lina-*cover Regional News*, Zanzibar Leo lina-*cover* pia *Local News*. Njia moja ya kuboresha lile gazeti ni kuachiwa kidogo angalau liwe linakuwa huru linafanya maamuzi kwa ajili ya jamii pia. Kwa hiyo, vichwa vyao vya habari kila siku vinajirudia pamoja na picha za mbele. Wajaribu kujichanganya ili matangazo ya kibiashara yaongezeke nje na hili gazeti letu liweze kununulika zaidi huko mbele.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mengi, ninayo mengine ya kuzungumza ningehitaji kama masaa mawili, nilikuwa naomba tena kwa mwisho kumwambia Mhe. Waziri kwenye vikundi vya *Acrobat* ambavyo viko vingi pia Zanzibar, aanze kuviangalia katika hilo tamasha la vijana ambalo tutalipanga kama atalipokea hilo wazo, basi achukue tena vikundi vya *acrobat*, viko katika Mkoa wa Kusini na Kaskazini na pia Mjini tuwaunganishe ili mwaka ujao tuwe na tamasha la vijana wa Kizanzibari, ambapo vijana wetu sinema ya kuigiza tuanze kuondoa na tuweke jina katika filamu za sinema za Zanzibar, *Zanziwood*.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana, nawashukuruni pia kwa kuweza kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai Mohamed (Mpakabasi) kwa mchango wako mzuri, lakini bado unayo nafasi ya maandishi kwa Mhe. Waziri kumpelekea michango yako iliyobaki. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia siku ya leo tukaweza kufika ambayo ni siku tukufu ya Mwezi wa Ramadhani. Nimuombe Mwenyezi Mungu atujaalie yale mema yote yaliyopangwa katika mwezi huu tuweze kufanikiwa kuyapata, *Inshaallah* Ramadhani hii iwe *maqbuul* kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba na mimi nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameweza kutuletea hotuba yao hii nzuri na ina vitu vingi. Lakini mimi katika hotuba hii nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri kuona wanazibagua zile sekta na sio kama ilivyo hivi. Kwa sababu ukiwa hupo pale alipokuwa anasoma Mhe. Waziri basi ukija kutafuta sekta utapata tabu kidogo kwa sababu kama zimechanganyika na sekta nyengine, ni muhimu kama Baraza la Kiswahili ambalo mimi nalithamini sana.

Kwa hiyo, nataka vitu hivyo viwe viko wazi vinaoneshwa katika mtiririko wake ili tujue hapa Mhe. Waziri kazungumza kitu hiki na hiki na wewe utapata kuvifuatilia. Lakini hotuba yao ni nzuri na imebeba mambo mazuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia mafanikio hasa ninavyomuona waziri mwenyewe anajitahidi katika kuona hii wizara inapata mabadiliko.

Mhe. Mwenyekiti, nianze katika programu ya maendeleo ya utamaduni na utalii ambayo imeeleza katika kazi zake basi moja itawaendeleza wasanii kiuchumi na kuwapunguzia umaskini pamoja na kuwa na rasilimali watu wenye ujuzi na ustadi wa kukuza utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kweli ni kazi nzuri na kweli tunawapongeza vijana wetu wote ambao wanajitokeza katika sanaa kwa kuona sasa wanajisaidia kimaisha, na serikali kama ilivyojipanga basi naomba isije ikaregeza kamba hiyo, iwakumbuke na kuwasaidia kwa kweli waweze kufanya vizuri. Lakini jambo moja ambalo nilikuwa nataka niliombe au niishauri wizara, basi vijana wetu hawa wanapofanya hizi sanaa zao ni vizuri, serikali ingeangalia vijana hawa hawatoki ndani ya mila na utamaduni wetu, ili wakaweza kuwa zile sanaa zao ziwe nzuri na za heshima, na zingezidi kutujengea uzuri kwa sababu bado tutakuwa tumebaki katika mila yetu, na mtu kubaki ndani ya mila yake na utamaduni ni heshima kubwa kwake lakini hata kwa taifa lake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba vijana hawa waweze kuona wanafanya sanaa zao na utamaduni wetu bado unaendelea kuwepo, hasa ukiangalia mavazi yanatakiwa yawe mazuri ambayo yataleta heshima. Hata sisi waangaliaji itatufanya kupendezewa katika kuangalia michezo ile ambayo itakuwa na mafunzo mbali mbali pamoja na familia zetu bila ya kuathirika na chochote. Kwa sababu wakati mwengine sanaa zinazooneshwa zinatushinda kuangalia tukiwa tuko pamoja na familia zetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa ushauri wangu huo, ziangaliwe zisikiuke mila na desturi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika programu ya habari. Pia nipongeze sana vijana wetu ambao wanashughulika na habari zetu hizi kuzitoa hasa katika hiki chombo chetu cha Baraza, kwamba kinaonekana *live* katika matangazo yetu haya ni hatua moja kubwa. Pia niombe au niishauri wizara kuona katika sehemu ya utangazaji, kwa sababu sisi hapa Zanzibar tunasema wataalamu wa Kiswahili, Kiswahili chetu ni fasaha, kizuri, kilaini, kinapendeza kwa mtu yeyote kukisikia. Kwa hivyo, ni vizuri wale watangazaji tukahakikisha wanahakikiwa wakati wanapotaka kuajiriwa katika sehemu ile, ili wakaweza kuwa na ufasaha katika utangazaji hali ambayo tunaelewa mtangazaji yule anaonekana duniani kote. Kwa hiyo, Kiswahili ambacho atakitumia kikiwa

vizuri pale, maana yake ataweza kuitangaza nchi yetu vizuri na kuonekana Kiswahili chetu ni kweli chenye kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu nitoe mfano mdogo kuna watangazaji unawasikia kama neno 'Magharibi' analiita 'Makharibi'. Kwa kweli huu sio ufasaha mzuri au neno 'fadhila' analiita mtu 'fazila', sio ufasaha katika lugha ya Kiswahili, na sisi ni mabingwa wa kukifinyanga Kiswahi, kwa hiyo Kiswahili kiwe ni tija kwetu, tuwe popote ambapo tutaweza kutoka kwenda kufundisha wenzetu basi tuonakane lafudhi zetu zinapatikana kama yalivyo yale maneno yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika habari niseme bado naomba uongeze juhudi katika kuona tunazitangaza habari zetu, habari zetu hatuzitangazi ipasavyo, na hasa habari zinazohusu historia ya nchi hii Mhe. Ussi Yahya Haji kanifilisi pale kidogo. Historia ya nchi inatakiwa iendelee kutangazwa, kwa sababu vizazi viliopo na vijavyo viweze kujua wapi tumetoka wapi tupo na wapi tunaelekea kupitia nchi yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, naishauri sana serikali kuweka kipindi ambacho kitaweza kutoa taaluma katika historia ya nchi hii, kuanzia utawala ule wa Masultani mpaka kufikia maraisi wetu hawa ambao wameweza kutuongoza kwa awamu mbali mbali. Hii itasaidia kuwaona vijana wetu wanaelea Mhe. Ussi Yahya Haji alieleza pale kuhusu historia ya mabaraza ni wapi imeanzia ni muhimu kabisa.

Watu wanaweza wakaona aliyechipukia akajua Baraza hili tu kumbe tumeanza mbali. Kwa hii kujua maraisi tumetokea wapi mpaka hapa tulipo, ni muhimu vijana wetu wakaweza kujua hayo.Vyenginevyo ndio utakuja vijana wanajiuliza hawajui wameanzia wapi, wametokea wapi, utakuta ndio maana wanayumbishwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika mchango wangu katika suala zima la hawa waandishi wetu ambao tunao. Wenzangu wamelisema lakini kwa kuwa ni jambo muhimu, na mimi napenda nitoe msisitizo niliseme.

Mhe. Mwenyekiti, hawa vijana wanatutumikia sana katika kazi hizi za kuonesha hizi shughuli za Baraza, lakini ni kwa nini inafikia wadai tangu kipindi hicho kilichopita mpaka hii leo, haipendezi kwa kweli. Kwa kweli, serikali ijitahidi kuwaona vijana wetu hawa, kwanza niseme kazi wanayofanya ni ngumu lazima na sisi kama binadamu tuweze kujenga fikra.

Vijana wanasimama pale kutwa nzima hiyo ni *stamina,* lazima uwe na lishe nzuri ambayo ndio utaweza kusimama. Kwa hiyo, tunatakiwa hawa lazima tuwajali sana, na wana moyo wa kizalendo, vijana hongereni, endeleni kuwa na moyo huo. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa katika vijana hawa wanajenga taifa kwa muda mrefu sana, na zinapotokea ajira hatuwapi thamani hawa, wanatokea wengine ambao hawajajitolea kama hawa. Naomba sana Mhe. Waziri, na nakuona ni waziri makini naona utalishughulikia ipasavyo. Naomba sana hawa tuwajali tuone kazi wanayoifanya ni ngumu na ni kwa maslahi ya nchi yetu kwa hiyo tuwapatie posho lao. Na mimi nilitaka kujua labda wale vijana ambao wanaendelea kujenga taifa labda wako wangapi ambao hatujawaajiri na wanaendelea kujenga taifa na wapo kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hilo nilikuwa nataka kulijua, lakini pia hao kama fedha zao zishalipwa au vipi pia mnaweza mkatwambia.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilitaka kuongelea katika Shirika letu hili la Habari *ZBC* redio na *ZBC TV*. Mhe. Mwenyekiti, tunawapongeza kwa kazi ambazo wanazifanya, kwa sababu wanajitahidi, wanafanya kazi inaonekana hata hivyo vitendea kazi ni vichache lakini wanajitahidi kwa jitihada zao. Lakini mimi nataka kuuliza Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo gani mpaka hii *ZBC* yetu Redio tunapata shida kabisa kuisikia ni kitu ambacho kinasababisha, labda sisi tukose kuisikia wakati redio nyengine zimeanza hivi karibuni zinasikikana vizuri kabisa. Sisi yetu ambayo tunaitegemea sisi ndio wadau wa *ZBC*. Kwa hiyo, tunapenda kusikia habari zetu kwanza tukisikia hizo nyengine ziwe za nyongeza zetu tuzipate kwanza.

Kwa hiyo, mimi nataka kujua kuna tatizo gani. Lakini hata katika vipindi vya *TV* kunaonekana kuna habari vipindi vinajirudia hivyo kwa hivyo, ambavyo vinatuchosha kuangalia na watu wanatamani kuangalia *TV* nyengine. Sasa hili linarejesha nyuma, kwa sababu mtu kile chako unakithamini. Sasa na sisi tunapenda kuthamini vyombo hivi, basi tayari tuwe na matayarisho ya kuona vipindi vinakuwepo vizuri vyenye kuvutia halafu tuendelee kukiangalia chombo chetu hichi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamesema mengi na mimi nilisema niseme machache, kwa sababu kabla sijamalizia Mhe. Mwenyekiti niseme hili ni la mwisho naomba sana wizara yako iwaangalie sana mafundi mitambo.

Mhe. Mwenyekiti, hawa ni watu muhimu sana, na nataka kuchukua fursa hii kuwapongeza kabisa tuna mafundi stadi wazuri katika vyombo vyetu hivi, na mimi najivunia kila siku kusema jambo hili kwa sababu nina kaka yangu fundi redio, fundi *TV* na alikuja kusoma hapa anaishi Dar- es- Salaam lakini alikuja kusoma hapa *TVZ* baadae tu alisafiri kimaisha kaenda huko, lakini alisoma *TVZ*, na nikwambie alikwenda kusoma Ethiopia mafunzo ya wasomi wanaoshughulikia haya mambo ya *TVZ* na Redio wakaenda kupata *course* huko katika mtu aliyefanya vizuri katika Tanzania alikuwa kaka yangu.

Sasa najisifu kwa sababu ufundi huo kaupata hapa, sasa tuelewe kama hawa mafundi tulionao tusije kuwabeza ni mafundi wazuri sana. Kwa hivyo, naomba tuwaangalie maslahi ili wasitutoroke mafundi hawa tutakuja kuyumba sisi katika vyombo vyetu hivi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri kulishughulikia jambo hili, ili tuone mafundi wetu wa mitambo bila ya wao tusingejivua kuwa hapa sasa kuna *ZBC* Redio na *ZBC TV*. Isipokuwa wao ndio wanatuwezesha moja kwa moja kufuata vyombo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninachukua fursa hii mimi kwa niaba yangu na wanawake wa Mkoa wa Kaskazini kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, na kwa kuwa najua waziri msikivu na mfuatiliaji nina matumaini makubwa ya chombo kwamba kitakwenda katika *speed* ya mageuzi haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mhe. Waziri nakutakia kila la kheri uweze kufanya kazi zako vizuri katika wizara hii, na hichi ndicho chombo ambacho tunakitegemea, ndio matumaini ya Wazanzibari Mhe. Mwenyekiti.

Ahsante naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako, lakini pia nikupongeze kwa kutumia muda wako sahihi na ipasavyo. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuichangia hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, Mhe. Rashid somo yangu.

Vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru yeye mwenyewe Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kuweza kuiandaa hotuba hii, na yeye mwenyewe

kuiwasilisha kwa ustadi mkubwa sana kuliko hotuba zote ambazo zimetangulia, namshukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, alikuwa na msisitizo wa aina yake kuonesha kwamba anaumwa na mambo yanayohusiana na habari.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niishukuru kamati ambayo ni ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa ripoti yao nzuri na ushauri wao mwingi sana kwa wizara inayohusika.

Vile vile nichukue fursa ya kumpongeza sana muwasilishaji wa hotuba ile Mhe. Maryam Thani; Mwakilishi wa wananchi jimbo la Gando. Ni mara yake ya mwanzo lakini kaonesha umahiri mkubwa sana, lakini vile vile nimshukuru jirani yangu hapa, nimpongeze kwa msisitizo sana wa michango yake pamoja na Wajumbe wengine ambao wamechangia hutoba hii.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba hotuba hii ya bajeti ya wizara hii mimi nitangulize kwamba naiunga mkono asilimia mia kwa mia. Ni hotuba ambayo imesheheni mambo mengi yaliyogusa katika wizara hii mambo mbali mbali. Lakini pamoja na uzuri wote huo, ningependa na mimi vile vile kuchukua nafasi hii kuichangia hotuba hii ili kuweza kumrahisishia waziri mpya wa habari kuweza kufanya majukumu yake vizuri zaidi.

Kwanza nimpe pole kwa kuweza kurithi manyago mengi katika wizara hii, lakini yeye mwenyewe anaonekana sasa yuko kidete katika kuweza kuitetea na kuweza kulinda na hatimaye kuleta maendeleo sahihi ndani ya wizara hii. Na tunajua kwamba matatizo mengi ya wizara hii ni kwa sababu ilikuwa haiko chini ya mikono salama ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na suala la matamasha. Imeelezwa hapa kwamba kuna matamasha mengi ambayo taasisi yetu hii imeshiriki na vile vile imeratibu, lakini bado nahisi kwamba kunahitaji aidha uwezeshwaji au msisitizo zaidi wa chombo chetu hichi kinaratibu matamasha haya.

Tuna matamasha mbali mbali Zanzibar lakini yanaanzishwa kwa shangwe, lakini badala yake tunaona kwamba yanadorora siku hadi siku.

Niiombe sana wizara yake Mhe. Waziri akiwezeshe kitengo hichi ambacho kinaratibu na kusimamia matamasha haya kuweza kusimamia vizuri, lakini kubwa zaidi kuweza kuwa na mashirikiano na zile jamii ambazo zinaanzisha matamasha.

Kuna matamasha kwa mfano lile la Mangapwani lilianzishwa lakini sijalisikia tena. Kuna matamasha haya ya vyakula vya asili yanaanzishwa lakini sijasikia tena. Lakini kubwa zaidi hili tamasha la Mzanzibari ambalo lilianzishwa zamani lakini siku hadi siku nahisi linaporomoka. Tujitahidi sana kuweza kuona matamasha haya yanalindwa, kwa sababu ndio yanayoimairisha asili ya utamaduni wa Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee katika suala la Utalii. Utalii ni moja kati ya sekta muhimu sana kwa hapa Zanzibar. Uchumi wa Zanzibar kwa asilimia kubwa unategemea sekta hii.

Nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuweza kufuatilia maeneo mbali mbali katika kipindi kifupi kuweza kuona jinsi gani utalii unaendeshwa. Nimsaidie tu katika mambo matatu muhimu.

Moja ni Chuo cha Utalii, Chuo hichi ni muhimu sana katika kuweza kuandaa vijana kuweza kuajirika katika sekta hii, lakini vile vile kuweza kujiajiri.

Kwanza nipongeze sana Chuo hichi kwa kuweza kuona kwamba na kuhamasisha vijana suala zima la kujiari. Kwa sababu orodha inajionesha ni kwamba vijana wengi wanaomaliza vyuo basi wanategemea zaidi kuajariwa kuliko kujiajiri. Kwa hiyo, nipongeze juhudi hizi za kuweza kuhamasisha wahitimu wetu kuweza kujiajiri na hii mfano wa watu saba. Mimi nafikiria bado chuo hakijafanya utafiti wako wengi zaidi ya saba.

Kwa hiyo, nichukue fursa hii kukitaka chuo kufuatilia zaidi kwa sababu kuna vijana wengi ambao wamesema pale masuala ya mapishi, na hivi sasa wamejiajiri katika suala zima la mapishi mbali mbali.

Kwa hiyo, kitengo hicho kiweze kufuatilia vizuri kuweza kupata takwimu, hawa vijana wako wengi ambao wanajiajiri. Lakini vile vile chuo kiweze kuchukua juhudi za aina yake kuweza kuwafuatilia wahitimu na hususan wale Wazanzibari kuweza kuona kwamba wanawasimamia na kuwaunganisha na waajiri, ili kuona kwamba kwa kiasi kikubwa Wazanzibari wanaajiriwa katika sekta hii ya utalii, vyenginevyo itakuwa sisi tunanufaisha watu kutoka maeneo mengine lakini Wazanzibari wanabaki kuwa hawana ajira katika sekta hii muhimu ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika masuala ya mapato katika sekta hii ya utalii. Hivi sasa utaratibu ambao mahoteli mengi wanautumia ni utaratibu wa *package* ambao malipo yao yanalipwa nje.

Nimuombe sana Mhe. Waziri afuatilie suala hili kwa sababu nahisi sana linavujisha mapato ya utalii kwa nchi yetu. Kwa hiyo, tutabaki kwamba tunawanufaisha wageni katika kuwekeza lakini Zanzibar itaendelea kudidimia wakati nchi nyengine zinawekeza katika utalii ziko katika hali ya juu. Ningemuomba sana rafiki yangu alishughulikie sana suala hili.

Suala la migogoro ya wawekezaji kuna miradi ambayo imewekezwa na wawekezaji kwa njia ya ubia baina ya wazalendo na wageni. Kumejitokeza suala la migogoro ambalo hili halitatusaidia, na wakati mwingi wanalalamikiwa Wazanzibari waliowekeza ubia na watu hao wageni wataondosha imani katika kuwekeza katika visiwa vyetu.

Nimeiona kesi moja Mhe. Waziri anaishughulikia, nampongeza sana na namuomba aendelee kuzichunguza kesi nyengine za aina hii ambazo kama zitaachiwa ziendelee wawekezaji kutoka nje wataachia, na sisi wenyewe nina imani kwamba wengi wetu kwa sababu ya mitaji yetu midogo tutashindwa kuendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika suala la michezo. Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kwamba Zanzibar kipaumbele chetu sana katika michezo tunataja mpira wa miguu, na hapa wachangiaji wengi sana walikuwa wanaekelekea huko.

Mimi naelewa kwamba Zanzibar ilikuwa inasifika sana katika michezo ya *badminton*, riadha, *table tennis* michezo hivi sasa imedidimia sana, na kipaumbele hakipo. Ningemuomba sana Mhe. Waziri kuweza kuitizama michezo hii ambayo imeiletea sifa sana Tanzania mpira wa vinyoa, *badminton* na *table tennis*. Hii Wazanzibari wengi walichukua medali Tanzania na Afrika Mashariki lakini hivi sasa huisikii.

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Zanzibar bado mpaka hivi sasa haina ukumbi wa kitaifa wa kuchezea michezo ya ndani. Hii ni aibu kubwa kwa taifa letu kwamba mpaka leo hatuna ukumbi wa kitaifa ambao unaweza kuchezewa michezo hii ya ndani.

Jamani kama tunatembea huku kwa wenzetu skuli ya Msingi tu au ya Maandalizi ina ukumbi wa michezo ya ndani, ina *swimming pool*, sisi tutajisifia nini hapa katika mchezo wa kuogelea iwapo taifa lenyewe halina hata *swimming pool* ya taifa, kwamba vijana wanaweza kwenda kufanya mazoezi pale. Mhe. Waziri nakuomba mimi ni mtaalamu wa michezo nitumie sana katika hilo. (*Makofi*)

Nije sasa katika suala zima la viwanja. Mhe. Waziri alisema hapa kwamba kuna mradi huu wa viwanja vitatu ambavyo vitajengwa katika Wilaya. Sijui lakini kutokana na uzoefu wetu pengine ni vya *football*, lakini nimuulize tu viwanja hivi ni vya michezo gani na vitajengwa katika maeneo gani ya wilaya hizo tatu, na vigezo gani vimetumika kwamba viwanja hivyo vipelekwe kwaza katika wilaya hizo. Lakini gharama kiasi gani ataweza kuzitumia katika ujenzi wa viwanja hivyo, na kama ndani ya hivi hamna viwanja vya michezo mengine basi vile vile alione kwamba kuna michezo inapaswa ipelekwe katika vijiji na ijengwe viwanja kama *volleyball* na michezo mengine.

Lakini katika suala zima la ufundishaji wa somo hili la michezo tusitarajie kwamba tutakuwa na vipaji vizuri vya vijana wetu katika michezo bila ya kuwafundisha.

Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Habari ashirikiane kwa karibu sana, na aipe msukumo mkubwa sana ndani ya Wizara ya Elimu, kwa sababu Wizara ya Elimu ndiyo ambayo inawanda vijana na hatimaye kuweza kuviona hivyo vipapi na vipaji vinaanza kuonekana darasani katika ufundishaji. Na hili somo la michezo Mhe. Waziri huko maskulini limekufa.

Naomba sana ushirikiane na Wizara ya Elimu na uisaidie kwa hali na mali kuona kwamba somo hili linafundishwa ili hao vijana unaowatarajia wakusaidie kimichezo katika wizara yako basi uwapate.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie sana katika Vyombo vya Habari. Vyombo vya Habari vya Zanzibar nivipongeze sana kwa kuweza kutupa habari, kutuburudisha na mambo mengine ambayo tunayapata kupitia vyombo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo hivi vinahitaji kuangaliwa kwa jicho la huruma sana, mitambo mingi ni michakavu, lakini wafanyakazi wana hali ngumu ya kimaslahi na maposho. Wenzangu wameyasisitiza na mimi ninaendelea kuleta msisitizo.

Mhe. Waziri amejitahidi katika kipindi hichi kifupi kufuatia maposho, lakini kuna wafanyakazi tunao hapa hapa ndani ya jengo, wao hawamo katika maposho hayo. Naomba uratibu ufanyike vizuri ili kuona wafanyakazi wote wenye haki ya kupewa maposho haya, wanapewa maposho haya yanayostahiki. Isiwe kuna ubaguzi huyu kapata, huyu hakupata. Hiyo itawanyong'onyesha wafanyakazi wengine. (*Makofi*)

Vile vile aniambie Mhe. Waziri kile Kitengo chetu cha Redio pale Magogoni Dar es Salaam. Hichi kitengo kina matatizo na kina malalamiko mengi. Nilimuona katembelea karibuni Mhe. Waziri na nimpongeze sana. Naomba sana hicho kitengo akishughulikie. Kina malalamiko mengi. Wafanyakazi wananyong'onyea sana. Kitengo hicho wakati mwengine hakirushi kipindi cha magazeti. Sisi wasikilizaji wa vipindi utaambiwa tunaomba radhi, sijui vipi. Lakini kumbe masuala tulipoulizia ni madogo madogo sana. Kwa hivyo sisi tunaosikiliza magazetini kutoka kwenye redio yetu. Hivyo akiimarishe kitengo hichi ili kiweze kufanya kazi zake vizuri zaidi.

Lakini sasa nije katika suala la magazeti, hususan Zanzibar Leo. Mwenzangu Mhe. Simai Mohamed Said amelizungumza. Hili gazeti kwa kipindi kirefu kuwa taarifa niliyonayo linachapishwa Tanzania Bara. Hapa nijiulize sasa, hivi sasa tunacho kiwanda ambacho kimeingiziwa mitambo mipya. Serikali imesema hapa. Sasa nimuulize Mhe. Waziri ni lini gazeti la Zanzibar Leo litachapishwa kwa kutumia kiwanda chetu. Kwa sababu ninafikiria sana unapochapisha nje, basi gharama zinakuwa ni kubwa zaidi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba ninaishukuru wizara hii kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake hii na niwapongeze watendaji wote wa wizara hii, na waendelee na juhudi zao za kuweza kuiona wizara hii inapata maendeleo, kwa sababu ni moja kati ya wizara ambayo ina mihimili ya uchumi wa nchi hii, ni Idara ya Utalii.

Baada ya hayo mimi niseme tu kwamba ninasisitiza tena kuunga mkono asilimia mia kwa mia ya hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Anayefuata ni Mhe. Salma Mussa Bilal, Mhe. Shamata Shaame Khamis, Mhe. Abdalla Ali Kombo ajitayarishe na Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma kwa kutupa afya na uzima hasa ukizingatia leo ni siku ya mwezi mosi Ramadhani kwa kukutana leo hapa tukiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Mwenyekiti, pili nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii leo na mimi nichangie alau machache, ukizingatia kwamba mengi yameshazungumzwa na wachangiaji wenzangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tokea limeanza Baraza hili, ukiacha juzi nilipowasilisha maoni ya Kamati ya *PAC* ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuzungumza.

Kwa hivyo naomba kwa ruhusa yako fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti, na Mwenyekiti mwenza wako na Mhe. Spika na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kishindo kuliongoza Baraza hili la Tisa la Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pongezi za pekee zikujie wewe na Naibu Spika kwamba mumechaguliwa kwa kuliongoza Baraza hili wanawake wenzangu, ikiwa ni kwamba tuna hamsini kwa hamsini tumeianza mwaka huu kwenye Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kwa heshima kubwa niwapongeze wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa pongezi za pekee ambao waliniwezesha na kunichagua kwa kishindo na kuweza kupata ushindi wa kuingia katika Baraza hili la Kutunga Sheria kwa kipindi cha pili. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia sina budi kuishukuru familia yangu. Bila ya kumsahau mume wangu mpenzi Bwana Issa, lakini siyo Issa Gavu. Kwa kunistahamilia, kunishauri kwa kipindi chote cha uchaguzi na hadi kufikia leo kuwa nimeingia katika Baraza hili la Kutunga la Sheria. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niwapongeze kwa dhati wale Wawakilishi saba walioteuliwa na Mhe. Rais na wao kushiriki katika Baraza hili, na kwa pamoja ninasema wanayo kazi ya kufanya ili kuweza kuipeleka nchi yetu mbele.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo pia naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe.Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa umahiri wao wa kuweza kutuletea hotuba hii yenye mvuto na leo hii tunaichangia kwenye Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nichangie machache hasa ukizingatia kwamba mengi wenzangu wameshachangia, na *points* ambazo nilikuwa nimezipanga, nyingi tayari zimeshazungumzwa. Kwa hivyo naomba na mimi nitoe msisitizo ili na mimi niwemo katika *hansard* kwamba nimechangia hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba nianze na Shirika hili la Utangazaji *(ZBC-TV).* Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa niwapongeze wafanyakazi wote wa *ZBC-TV* kwa umahiri wao, uhodari wao na uzalendo wao mkubwa

ambao walionao kwa kushirikiana na sisi vikao vyote ambavyo tunakuwa tunaendesha kwenye Baraza hili. Wafanyakazi hao asubuhi, mchana tunakuwa nao, tukiondoka usiku tunaondoka nao.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa masikitiko makubwa kabisa bado naomba nisisitize kwamba wafanyakazi hawa posho zao hawalipwi ipasavyo. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa Mhe. Waziri atwambie hasa ni sababu gani hasa inayosababisha wafanyakazi hawa wanafika vikao vitatu wanakuja tunashinda nao, lakini posho zao hazipatikani. Naomba aje anieleze Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ninadhani kwa umahiri wake alionao na upya wake alionao pengine Mwenyezi Mungu amjaalie yeye lisiwe hili, kwa sababu ninaweza kusema labda sababu zilizokuwa zinasababisha hili pengine ilikuwa ni *sabotage* ya makusudi kwamba washindwe kufanya kazi zao. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri naomba atupe sababu za msingi, lakini pia naomba achukue juhudi za makusudi ili aweze kuwaona kwa jicho la huruma wafanyakazi hawa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikiacha hawa wafanyakazi ambao wamo ndani. Pia naomba niwapongeze wafanyakazi wote wa *ZBC* kwa kazi zao nzuri pamoja na mazingira magumu ambayo wanafanyia kazi. Mazingira kama walivyokwishasema wenzangu mazingira ya vifaa chakavu na mambo mengine, lakini ninawapongeza.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja naomba niende katika chumba cha kurushia matangazo cha *ZBC* pale Makao Makuu.

Mhe. Mwenyekiti, chumba kile kuna mashine ambayo inaitwa *server*. Mashine hiyo ni mashine ambayo *very expensive*, imo mule ndani katika chumba cha kurushia matangazo. Mashine ile kwa umuhimu wake haipaswi kukaa chumba kile ambacho wamo wafanyakazi. Kwa sababu mashine ile inatakiwa iwe na baridi ya ziada kwa uzima wake ile mashine.

Lakini kilichofanyika Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ile mashine ya *server* imetiwa ndani ya chumba kile cha urushaji wa matangazo. Chumba kile inabidi kiwe na baridi ya ziada na mule muna binadamu. Na baridi ya chombo na baridi ya binadamu ni tofauti. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana Mhe. Waziri ufanye utaratibu au kuna utaratibu gani wa kuihamisha mashine ile ya *server*, kuitoa mule katika chumba cha matangazo kuiwekea chumba

chake makusudi iweze kuishi kwa ile baridi ambayo inatakiwa, lakini isilinganishwe mashine na maisha ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wale ambao wanaofanya kazi mule kwenye chumba cha kurushia matangazo wanafika kung'ang'anaa kwa baridi kali. Mhe. Mwenyekiti, hawapati maposho yao ipasavyo, hawagaiwi hata lita moja ya maziwa kutokana na mionzi inayotokana na mashine ile.

Kwa hivyo naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri uwaone na wao. Wanapolalamika kwamba hii baridi kali humu, wanasema wanaoweza atakaa asiyeweza basi! Mhe. Mwenyekiti, kauli nyengine zinakuwa siyo nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana vijana wale ama mashine ile kuwe na utenganishi. Baina ya mashine, kila kimoja kina umuhimu wake. Mashine ina umuhimu wake lakini na wale watumishi ambao tunawatumia kuturushia matangazo yetu pia wana umuhimu wao. Hivyo tuangalie afya ya mashine, tuangalie na afya ya wale watu tutawaua kwa baridi.

Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri unapoingia wewe katika chumba kile baridi inapunguzwa kwa makusudi lakini ukitoka kila kukicha baridi inazidishwa tutawaua. Tuwaangalie kwa jicho la huruma wafanyakazi wetu Mhe. Waziri.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, halafu pia Mhe. Waziri toka kuanza matangazo ya masaa 24. Kunakuwa kuna *shift* za usiku. *Shift* za usiku hizo hakuna hata usafiri wa dharura, inapotokea jambo pale labda wale wafanyakazi uweze kuwasaidia. Kwa hivyo na hilo Mhe. Waziri pia ninaliomba.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyakazi wanaoingia pale usiku. Wanaingia kuanzia saa tatu usiku mpaka saa mbili za asubuhi. Fikiria muda wote huo wanafanya kazi zaidi ya masaa ya kufanya kazi wale watumishi. Hivyo naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri awaangalie sana na kuwafikiria watu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la *ZBC* ni shirika ambalo linatakiwa lijiendeshe, lakini mpaka leo *scheme of service* ni kama wimbo wa taifa. Kila siku hakuna *scheme of service* wanayotayarishiwa za Kishirika. Zipo tu zinatajwa lakini kila siku zinaharibika hazijatengenezwa mpaka leo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri naomba na hilo pia uwaangalie. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende katika Chuo cha Habari. Chuo cha Habari kwanza nipongeze uongozi wa wizara kwa juhudi zao kwa kuwapa

elimu vijana wetu mafunzo ya uandishi wa habari. Lakini pia niwapongeze kwa kufanya mazungumzo ya awali na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hivyo mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri afanye jitihada za makusudi ili kuweza kuendeleza yale mazungumzo kuweza kupeana uzoefu baina ya Chuo cha Habari cha hapa na Chuo Kikuu Dar es Salaam, ili tuweze kupata waandishi wazuri kwa kuendeleza taifa letu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapo hapo nilikuwa nina masikitiko ni kwamba jengo ambalo Ofisi hii ya Chuo cha Uandishi wa Habari hairidhishi hata kidogo. Haina nafasi, ipo finyu sana. Nimeona katika kipaumbele cha hotuba, kuimarisha jengo la Chuo cha Habari. Naomba Mhe. Waziri ufanye juhudi za makusudi ili wapate jengo lao na wao wawe na hadhi ya chuo na jengo ambalo linafaa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 28, "Maeneo ya Vipaumbele vya Wizara". Moja ikiwa ni uimarishaji ya miundombinu ya *digital* na ununuzi wa ving'amuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara kwa kuweka kipaumbele hichi cha miundombinu na ununuzi wa ving'amuzi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu king'amuzi hichi cha *AGAPE*. King'amuzi cha *AGAPE* kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hakifai. Kumekuwa na malalamiko mengi na wananchi wengi wameviacha hivi, wanakwenda kununua ving'amuzi vya sehemu nyengine na kuikosesha serikali mapato.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hebu naomba unieleze kwa kina na mimi kuhusu maendeleo ya hichi king'amuzi cha *AGAPE*. Hivyo mumeweka kipaumbele kununua ni hichi hichi cha *AGAPE* muendeleze ama kuna vyengine ambavyo kuna mpango wa kupatikana ving'amuzi vyengine. Hivi ving'amuzi ni vibovu. Ving'amuzi hivi havifai, vimekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi na vinakosa wateja kwa kweli. Tulikuwa navyo, tulikopeshwa sote humu Wawakilishi, lakini tumevikimbia tumeviacha kwa sababu ubora havina.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo Mhe. Waziri naomba utupe maelezo kuhusu ving'amuzi hivi. Kama ni hivi hivi au kuna mpango wa kununua ving'amuzi vyengine. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika uwanja wa Mao Tse Tung. Mhe. Mwenyekiti, nia ya serikali ni nzuri ya kuujenga uwanja wa Mao Tse Tung na hatua zilizofika ni nzuri, lakini Mhe. Mwenyekiti, isiwe kama ni wimbo wa taifa. Kila siku uwanja wa Mao Tse Tung. Mhe. Mwenyekiti, namuomba

Mhe.Waziri ulizingatie, ulisimamie hili suala. Huu uwanja ujengwe, kwa sababu uwanja huu wa michezo utasaidia kukuza michezo.

Na kama walivyosema wenzangu kwamba michezo siyo tu afya, bali michezo pia ni ajira. Kwa hivyo tukiwa na viwanja viwili vikubwa vizuri. Ina maana na michezo yetu itapanuka na vijana wetu watapata ajira. (*Makofi*)

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo. Umesema hapa kwamba hadi Machi, 2016 bado hazijaingizwa fedha za uwanja ule. Je, ni lini hasa utueleze ni lini hasa zitaingizwa hizi fedha ili ule uwanja ujengwe, isiwe tena kama wimbo wa taifa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, labda langu la mwisho na mimi niende kwenye sekta hii ya michezo. Mhe.Mwenyekiti, sekta ya michezo nimeeleza mengi lakini wewe mwenyewe ulilieleza kwamba hukuona ukuzaji wa michezo kwa walemavu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwa Mhe.Waziri watu wenye ulemavu wana vipaji vikubwa sana. Hivyo wanahitaji kuendelezwa Mhe. Mwenyekiti, lakini inasikitisha kuona katika bajeti yako hii pamoja na uzuri wake iliyonayo, inasikitisha...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Sawa. Inasikitisha kuona kwamba vipaji vya walemavu kuwakuza hawa humu kwenye bajeti yako hamna Mhe. Waziri na ninaomba sana na hilo liwemo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Salma kwa mchango wako mzuri. Sasa anafuatia Mhe. Shamata Shaame Khamis na Mhe. Abdalla Ali Kombo ajitayarishe.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi jioni ya leo kupata nikaweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu jioni ya leo kwa kunijaalia kuendelea pia na mimi kuwepo na uhai, na vile vile na Waheshimiwa wengine ikiwa tupo katika neema hiyo ya uhai na ikiwa tunaendelea na jukumu letu kama ambavyo inastahiki.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe jioni hii ya leo na kuweza kuendeleza kazi hii ambayo ipo mbele yetu sasa hivi.

Vile vile niipongeze wizara hii, watendaji wote lakini vile vile niwapongeze zaidi viongozi; yaani Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya, na ambayo imeanza kutoa matumaini kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nichukue fursa hii kuwapongeza wapiga kura wa jimbo langu kwa kazi nzuri na ustahamilivu wao wanaoendelea nao katika kuendeleza majukumu hata nikiwa huku katika maeneo ambayo nawawakilisha wao.

Vile vile naomba moja kwa moja kwa vile wajumbe wenzangu wengi wameshachangia katika maeneo mbali mbali, na mimi nitagusia kwa muda mchache ili niweze kuokoa muda.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikiri kabisa naungana na Mhe. Balozi Ali Karume, kuelezea jinsi ambavyo sekta hii au wizara hii ina umuhimu wa pekee. Ni jambo ambalo halifichiki na ni jambo ambalo lina ukweli kutokana na uhalisia wake na jinsi mambo tunavyoyaona.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukumbuka kidogo kwamba katika chaguzi zetu ambazo zimepotoshwa, ni dhahiri kwamba wananchi wengi waliweza kuelewa kama walivyoelewa kwa mujibu ambavyo walieleweshwa ama kwa kupotoshwa kwa makusudi. Lakini niwapongeze sana Shirika la Utangazaji *ZBC* kwa kuweza kuchambua na kuandaa kipindi maalum ambacho kilichukua fursa ya kuwafahamisha wananchi juu ya ukweli halisi wa jinsi matukio ya uchaguzi au uchaguzi jinsi ambavyo uliharibiwa.

Ni ushahidi kwamba kila kituo takwimu mbali mbali ziliweza kuoneshwa, na ukweli ni kwamba kama hatukuwa na vyombo kama hivi basi nadhani wengi wetu tungebakia na kuamini kama hivyo ambavyo wengine walitaka tuamini, nawashukuru sana na nawapongeza sana.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kwa kuanza kuunga mkono bajeti ya wizara hii ya shilingi bilioni 16,281,900,000 kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya wenzetu, basi mimi sina shaka nayo na naomba wapewe yote na kwa muda ambao unastahiki ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kanuni zao za kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nichangie katika kuimarisha na kuendeleza sekta ya utalii hapa nchini kwa kukumbuka kidogo katika kipindi kilichopita cha bajeti ya mwaka 2015/2016 Baraza limesema kwamba au katika hotuba imeeleza kwamba kuna sanaa na sensa ya filamu na utamaduni ilifanya vikao 11 na kukutana vile vile na masheha katika wilaya na vikao vitano. Suala hili mimi nilitaka kuomba tu kama wenzangu walivyotangulia tuweze kujua ni wilaya zipi, na ni masheha wa shehia zipi ambao waliweza kufikiwa na mpango huu.

Mhe. Mwenyekiti, kama itakuwa imegusa kama vile ambavyo nimeona katika ukurasa wa 15, ambayo imesema kwamba katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2015/2016 kulikuwa na kuadhimisha siku ya makumbusho duniani kwa idara na kushirikiana na Wizara ya Afya, ilifanikisha katika magonjwa yasiyopewa kipaumbele kama vile minyoo, matende na kichocho, hayo ni kwamba kulikuwa na maonesho matatu na hayo yote kwa mujibu wa maelezo ni kwamba yalifanyika katika jengo la makumbusho liliopo Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo basi ningeshauri sana wizara kwamba kwa sasa na ninaamini inawezekana sana, kwamba Kisiwani Pemba kama haya mambo mengine hayajafanyika kama haya ambayo nimeyaelezea basi ni vyema tuelekeze nguvu zetu za makusudi, kuona kwamba utalii nako ni sehemu moja ambayo tayari uwekezaji umeshaanza kuja.

Ukweli ni kwamba utalii bado haujafahamika ipasavyo, na tumekuwa tukishuhudia migogoro na sintofahamu kwa wananchi wetu juu ya dhana nzima ya utalii. Sasa mambo kama haya yakifanyika katika maeneo ya kule, basi tunaweza kusaidia sana katika kuwafahamisha na kuwaelewesha wananchi wetu ili kuweza kutambua dhana nzima na umuhimu wake kuweza kuona kwamba nchi yetu pia inaweza kukusanya mapato kwa kupitia shughuli hizi ambazo zinafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kila anayesimama tunaomba utekelezaji uende sawia. Utekelezaji unaweza kwenda sawia lakini ni vyema tuongeze *speed,* kama vile ambavyo Rais wetu mpendwa alivyoweza kutoa muelekeo wa jinsi gani utekelezaji wa Chama cha Mapinduzi utalenga, na vile vile waziri

mwenye dhamana ya fedha ambavyo alionesha vizuri kwa vitendo kwa kuonesha mkakati wa ukusanyaji mapato. Nadhani hii pia inaweza ikatusaidia kuitangaza nchi yetu, lakini vile vile kuongeza wigo mpana zaidi katika suala zima la ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nichukue fursa hii ili kuingia katika sekta ya michezo. Kwa upande wa michezo niombe tu kwamba katika wilaya zile ambazo zimepangwa kutekelezwa na ambazo bado hatujazijua ni wilaya gani, kuna viwanja vitatu ambavyo vimetajwa kuwa vitajengwa, tunategemea na mimi naamini ni vya michezo ya mpira wa miguu. Kama hivyo ndivyo, basi ningeomba sana kwamba wizara iangalie zaidi kumbukumbu au pengine ahadi ambazo zimetolewa na baadhi ya watu ambao wamewatangulia viongozi.

Kwa mfano, kama sijapoteza kumbukumbu vizuri nakumbuka kwamba aliyekuwa Kamishna wa Michezo kipindi kile bwana Mshindo alikuwa anaitwa huyu, nadhani mwaka 2015 aliweza kutoa ahadi kwamba katika viwanja vile vya wilaya vya michezo vitajengwa basi katika Wilaya Micheweni kwa sasa ambayo imekuwa ni Wilaya ya Wete, kwamba Uwanja wa Kinyasini pia nao ulitajwa kuwa unaweza ukajengwa, ili uweze kuleta ufanisi katika suala zima la mchezo huu wa mpira wa miguu. Lakini kwa bahati mbaya sana nadhani tokea kipindi hicho kazi hii bado haijafanyika. Lakini vile vile tunashukuru kwamba katika kipindi cha karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameweza kuzindua kiwanja kimoja cha mchezo wa *volleyball* katika maeneo ya Wete.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchezo wa *volleyball* kwenye maeneo ya Micheweni kuna kiwanja ambacho nadhani pia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo katika kipindi kilichopita pia iliahidi katika utekelezaji kwamba kiwanja kile itakifanyia marekebisho na hatimaye kukijenga ili kiweze kuchezeka na hususan katika kipindi kile cha mvua. Nadhani kiwanja hiki kipo ndani ya Jimbo la Micheweni, hivyo namkumbusha Mhe. Waziri kwamba atakapokuja atoe ufafanuzi ili na wanamichezo wa jimbo langu waweze kusikia kwamba hiyo ahadi ambayo ilikuwa imezungumzwa basi waweze kusikia ni hatua gani ambazo wizara itaanza kuzichukua.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo napenda nizungumzie suala zima la ukusanyaji wa mapato. Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba katika lengo moja la ukusanyaji wa mapato, kuna jengo la sinema katika mji wa Wete, jengo hili nadhani kama sikosei ni kwamba jengo hili lilikuwa ni jengo la serikali, lakini kwa kipindi cha miaka mingi tumepata kusikia, sina uhakika sana, kwamba jengo lile tayari limetoka kwenye mikono ya serikali na limekodishwa kwa mtu

binafsi. Sasa nilitaka pia kujua kwamba jengo hili ni nani ambaye amekodishwa na ni kuanzia tarehe ngapi au miaka mingapi ambapo jengo hilo itakuwa huyo mwekezaji au huyo mtu aliyekodishwa atakuwa amekodishwa, na zile fedha ambazo zimekodishwa zinakwenda wapi, zinakwenda kwenye mfuko mkuu wa serikali ama zina matumizi mengine. Nataka kujua zaidi ili na mimi niweze kufahamu, wale ambao walitaka nilisemee hili basi na wao waweze kufaidika na kuona kuwa ukweli ni huu ambao unatarajiwa uutoe wewe Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, katika upande wa habari *ZBC* Pemba. Kwa sasa kule eneo lile la Mkanjuni ambako ndio Makao Makuu pale, ni kwamba jengo letu ukiliangalia kwa wastani sasa hivi limeshavamiwa sana. Kwa kweli sasa hivi majengo ya wananchi au makaazi yamekuwa karibu na jengo na sijajua kuwa wamejenga ni kwenye maeneo yao au ni kwenye maeneo ya hii taasisi wenyewe, nina wasi wasi kidogo kwamba tayari uvamizi umeshaanza.

Vile vile kuna hatua imefanywa, kuna uzio pale au ukuta umeweza kuzungushiwa lakini ukuta ule tokea mwaka 2013 bado haujafikia mahali. Kwa hivyo, pamoja na kama kuzuia uvamizi, lakini pia tunaweza tukalifanya jengo letu liwe salama na zile shughuli zinazofanyika pale, zikaweza kufanyika kwa usalama na utulivu na zenye ufanisi zaidi na zenye tija ili kuona kwamba shughuli za watendaji wetu zinafanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ningemshauri Mhe. Waziri tuweze kuona kwamba hatua madhubuti, na naamini kwa wewe jinsi ambavyo nimeona shughuli imeanza, naamini kwamba kazi ile itafanyika kwa ufanisi na kwa wakati muafaka kabisa.

Pia ningependa kujua kuwa kama litakubalika kuwa hizo hatua zianze kufanyiwa kazi, pia ningetaka kujua ni lini tutaanza hiyo shughuli ili na wananchi waweze kufahamu kwamba lile ambalo wamelitaka lisikike, kwamba limeshaanza kuonesha matumaini mema.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nigusie kidogo hizi redio za jamii. Katika nchi yetu kumekuwa na redio nyingi ambazo sasa hivi zimeanzishwa. Kwa mfano, katika jimbo la Micheweni kuna *community* redio ambayo tunaita Redio Micheweni kule iko, vile vile kuna Mtegani, Makunduchi, kuna Mkoani na kwengineko ambako nitakuwa nimekusahau.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nafuatilia hotuba hii sijaweza kuona kwa bahati mbaya pengine sijasema vizuri kuona kwamba mkakati zaidi wa redio hizi ambazo nazo ni mdau katika kutoa habari.

Ukiangalia ukweli ni kwamba hizi redio wale ambao hawaitakii mema nchi yetu wanaweza wakachukua fursa ya kuzitumia redio hizi na badala yake kuona na wao wanatumia nafasi kuweza kupotosha au kufanya yale ambayo hayawezi kuleta tija zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo redio hizi pia zinasaidia jamii katika kuwaelimisha, kuwaburudisha na mambo kama hayo. Pia redio hizi zingeangaliwa kwa mkakati wa makusudi japo kuwa ni redio za jamii, pamoja na kwamba ni jamii lakini najua kwamba taasisi hii au Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo wanaweza kuwa ndio *responsible* kwa lile ambalo litajitokeza.

Kwa hivyo, ni vyema redio hizi kuziwekea mikakati na kuweza kuzisaidia. Na ukiangalia, kwa mfano redio ya Micheweni, redio ile wananchi wa Micheweni bado hawajawa na uelewa wa kutosha juu ya kukisaidia chombo hiki kiweze kumudu shughuli zake. Kwa hivyo, sio jambo rahisi kwa sasa hivi Micheweni kuweza kuchangia kwa kiwango hicho na redio ile wakaweza kufanya kazi na hatimaye lile lengo la kuelimisha wananchi katika mikakati mizima ya kupunguza umaskini likaweza kufikiwa.

Kwa hivyo, ningeomba sana kwamba redio hizi tuziangalie kwa kina na kwa makusudi, ili kuona kwamba tunazisimamia na kujaribu kuwaelimisha watendaji walioko pale wanaoziendesha, ili na wao waweze kufanya kazi na kuisaidia serikali katika suala zima la kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana watendaji wetu hawa wanafanya kazi kubwa wanatusaidia katika kuelimisha...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Hususan katika kipindi cha magonjwa haya ya kipindupindu, wamekuwa wadau wakubwa sana katika kuona wanaelimisha jamii kwenye juhudi za kupambana na ugonjwa huu ambao umejitokeza katika nchi yetu.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba naomba bajeti hii tuipitishe na mimi naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nakushukuru sana. Kwanza kabla ya kuzungumza napenda kumjulisha Mhe. Waziri kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kutembea kwetu kwenye nchi nyingi za nje ya Zanzibar kuhusiana na utalii, basi kuna mambo tumeyaona wenzetu wanayafanya na ni mazuri.

Umesema utalii kwetu umeongezeka kutoka 132,836/- mwaka 2010 hadi 311,891/-. Katika mchango wangu kwenye hotuba ya Rais nilichangia suala hili lakini wakati ule tulikuwa hatuna waziri, leo waziri naomba akija basi anisaidie haya ambayo nitauliza.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoteli tunaambiwa kuna *grade* ya kwanza mpaka *grade* ya tano, Zanzibar nadhani pia zipo hoteli za namna hiyo. Sasa Mhe. Waziri akija atusaidie je, kuna hoteli za nyota ngapi na ngapi, na hawa watalii waliomo humu ni wangapi labda wamelala nyota tano, nyota nne, nyota tatu. Suala hili litatusaidia wageni wetu wanaokuja je, ni wa aina gani, na je wanaoomba vibali vya hoteli tuwape za hoteli zipi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akija atusaidie takwimu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, kuna vituo ambavyo watalii wetu wanakwenda. Kwa mfano, Kizimbani, Marikiti Soko Kuu. Mhe. Mwenyekiti, ukweli wa mambo hizi sehemu ni chafu sana.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ina mabwana shamba, hivyo ningependekeza hata Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo au idara yake yoyote iwe na watu ambao wanakwenda kwenye sehemu ambazo watalii wetu wanakwenda.

Kwa mfano, Kizimbani hasa siku za masika, ukienda kuna tope nyingi sana wamejenga vibanda. Situkani, lakini havina tofauti na vile vya mbuzi ambavyo viko kwenye maeneo yetu. Lakini mbaya zaidi kwenye meza zao ambazo ni za miti tu, kuna mafenesi, mananasi na kadhalika wanawapasulia wale watalii, kwa kweli ni hali mbaya na ni kitu ambacho hakipendezi, hawa wanakwenda kwa sababu hawana cha kukifanya, lakini naomba tufanye marekebisho.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye Soko la Darajani, hasa huku wanakotayarisha samaki na pweza kuingia ndani, hatuna cha kuficha, hali asilimia mia kwa mia ni mbaya sana. Unamkuta pweza anapigwa chini mchafu, mweusi pamoja na samaki halafu watalii wanapiga picha. Shahidi Mwenyezi

Mungu na Ramadhani hii, kulikuwa na mama mmoja wa Kizungu alipiga kelele mimi nikashtuka, maana wenzetu sio mara nyingi hupanda shetani kama sisi. Sasa nikamuuliza nini kimetokea, kakamata pua na mdomo namna hii (*hapa mjumbe alionesha kwa kushika pua na mdomo wake*), akasema harufu kama hii sijawahi kuisikia maisha yangu.

Kwa hivyo, ningewaomba Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, mkae pamoja, ile hali tuirekebisheni ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mwengine wa tatu, nilielezea kwenye hotuba ya Rais tuna nyumba katika fukwe; kutoka Uroa, Jambiani, Kiwengwa, Paje, Makunduchi hizi nyumba zimejengwa na wageni pamoja na wananchi wetu na wanazitumia siku za misimu zikifika wanaleta wageni. Sasa wasi wasi wangu hawa idadi ya wageni wanaokuja isijekuwa wanafikia nyumba hizi badala ya hoteli, ndio maana yake nikasema Mhe. Waziri mtupe wangapi wanalala wapi na wangapi wanalala wapi, tujue kwamba hawa ni watalii ni wageni wa kienyeji na taifa linapata nini.

Mbaya zaidi nyumba hizi ambazo zinatumiwa Serikali inafahamu, kwa sababu Serikali ya mtaa ni Sheha, ma- *DC* wanafahamu, ma-*RC* wanafahamu, *ZRB* wanafahamu lakini hapa tunakuja tunajisifu tuna utalii ambao uliokamilika, kwa hivyo kama ni mapato hapa tunayapoteza. Nina ushahidi sio kama ninazungumza tu kitu ambacho sina ushahidi sitozungumza. Lakini hatuna kimoja ambacho tunakifanya, kwa hivyo nakuomba Mhe. Waziri tufuatilie kitu hiki si vibaya wananchi wetu wakajiingiza katika hili, lakini lazima Serikali ipate mapato ni kitu ambacho tunakitafuta.

Jengine Mhe. Waziri kwenye kipindi chako cha Zanzibar au Redio yetu ya Zanzibar kuna kipindi hichi cha mawio, si vibaya kupata *information*, wanasema *information is power*, lakini kipindi sasa hivi kinaudhi, hawa watangazaji sasa nadhani wanachokifanya hawakijui unaweza ukachukua dakika mbili nzima wanaleta mafumbo, ngonjera, hujafahamu chochote. Sasa kama hawajasomea habari wafundishwe tunachotaka sisi ni habari sio mafumbo.

La mwisho Mhe. Waziri Makunduchi kulikuwa na nyumba za Serikali na mwisho zikawa nyumba za utalii, kulikuwa na nyumba mbili, nakumbuka moja iliwahi kutumiwa mpaka na *DC* wakati huo na moja ilikuwa inatumiwa na viongozi wa juu mpaka Marais kama nyumba ya kupumzikia, sijui kama

Makunduchi unakujua au hukujui, lakini kuna kijumba kimoja kimebakia ile nyumba moja ambayo ilikuwa kubwa imebomolewa na sasa hivi kumejengwa nyumba nyengine. Sasa suala langu ni hili hii nyumba iliyojengwa, je, ni ya Shirika la Utalii ama ni ya kampuni gani na kwa madhumuni gani, na je, Serikali inategemea kupata nini kwa niaba ya taifa letu ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mwanzo kabla ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wataala* aliyeniwezesha hapa kusimama na kuweza kuvuta pumzi zake na kupumua, na kuzingatia ni mwezi mtukufu wa Ramadhani, ikiwa ni Ramadhani ya mwanzo ya kumi la Rehema. Na nitajaribu kuzungumza kwa sauti nyepesi kidogo tofauti na siku za nyuma kutokana na siku yenyewe ilivyo kuipa heshima yake.

Kwanza kabisa nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake, nitakuwa sijatenda haki kama sijawashukuru Mwenyekiti wangu Mhe. Ali Suleiman maarufu Shihata au Mjomba, anapokuwa hayupo wakati mwengine nafasi hizi anakaimu Mwenyekiti anashika usukani huu Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma naye nimpongeze kwa kutuongoza vyema.

Mhe. Mwenyekiti mimi ni Mjumbe wa kamati hii na sikutaka kuikosoa sana hii kamati kwa vile ni Mjumbe, tumekaa huko tukasawazisha baadhi ya sehemu na nyengine hotuba imezitaja hapa sasa tena sijui kama Mhe. Waziri atazifanyia kazi, na tulimueleza huko tunategemea atakavyokuja mchango wa kamati utapata ufumbuzi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hapo nije kwenye sekta ya utalii. Tegemeo la uchumi wa Zanzibar bado lilikuwa linategemea zao la karafuu, lakini sasa kutokana na zao la Karafuu kupungua, hali hairidhishi, ajira zimekuwa haziridhishi na Serikali kama haikuwa makini katika Chuo chake cha Utalii cha Maruhubi basi patakuwa pana mtihani mkubwa.

Hapa naomba usikilize sana kwa makini isije ikafika mahali nikaambiwa ninabagua watu, huu ni ushauri wangu. Chuo kile zaidi kinanufaisha wageni kutoka nje wakiwemo Wakenya, Waganda na ndugu zetu wa damu Tanzania Bara, lakini la kufanya au kushauri Serikali tupeleke vijana pale angalau waliomaliza kitado cha sita ili waweze kuwa matunda mazuri mfano huo nchini Kenya wanapeleka watu karibu elfu 14 sasa hivi wanafaidika nchini Dubai, na wanachokipata wanapeleka kwao Kenya, nafikiri lugha niliyotumia ni

Kiswahili fasaha kabisa, hiyo isije ikafika nikaambiwa nataka kubagua watu aa, baada ya miaka kumi nafikiri tunaweza tukaona tija yake.

Mhe. Mwenyekiti, nije na kilio cha sekta ya habari. Sekta ya habari inahitaji mageuzi makubwa ikiwemo kurekebisha mazingira magumu ya wafanyakazi katika vyombo vya umma, Wizara au Idara ya *ZBC* au Habari na Utangazaji jamaa wana mitihani mkubwa kutoka vitendea kazi, gari hawana, kamera zenyewe za kubadilishana hazitoshi. Kuna Mheshimiwa mmoja alichangia Habari kuna wakulima vijijini, kuna wavuvi wanataka kupata habari watafikaje bila ya kuwezeshwa hawa ,au hawana haki, nitahitaji maelezo hapa Mhe. Waziri pamoja na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ofisi ya Zanzibar leo tumepiga kelele kwa muda mrefu humu ndani, hawa haijulikani magharibi, haijulikani adhuhuri, haijulikani laasiri, haijulikani kuna mvua haijulikani kuna jua. Vyumba vya kufanyakazi haviridhishi na tunahitaji habari kutoka kwao, jambo la kusikitisha kwa muda mrefu Serikali inaambiwa suala hili lakini utekelezaji haupo, na humu humu Naibu Waziri alisema Serikali haijali hasara kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Kauli ya Serikali hiyo ndani ya chombo hichi hivi juzi juzi tu tunaweka wapi watu hawa.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti nitahitaji maelezo unafanya kazi katika Gazeti hili la Zanzibar Leo miaka kumi na mbili watu hawajaajiriwa mpaka wameshakuwa wazee, wengine washafanya mvi nyeupe, wana kasoro gani wale Mheshimiwa. Watueleze miaka kumi na mbili mtu unamchukua hujamuajiri tegemeo lake nini au wana kasoro zote watueleze.

Nije suala la waandishi wa habari hasa wale watangazaji wa redio. Nataka kuwauliza hili suali nimepiga kelele muda mrefu kuna kitu gani cha kushangaza sijui kama wahusika wako huko juu, naomba msikilize vizuri Kiswahili hichi nilikipigia kelele sana mimi mwaka jana na mwaka juzi, Mheshimiwa rafiki yangu hapa Said Omar wa Wingwi akauliza swali humu ndani hatajwi kauliza swali anaambiwa Naibu Waziri kajibu swali, kwani kakosa nini huyu Mhe. Said wa Wingwi si ubaguzi mnaofanya huu, huu ni mwezi mtukufu wa ramadhani, sitaki nitoe sauti yangu kubwa nikaja nikakera watu lakini ubaguzi huu umekuwa, mwisho Mhe. Waziri anauliza swali hatajwi wananchi wake watajuaje kama kafanya kazi, wakati huku Waziri anajibu swali Naibu Waziri anauliza hatajwi, haifahamiki hii tusifike huko. Nafikiri Mhe. Waziri Kiswahili anakifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa na kilio kirefu na hichi nimeshakiambia mpaka Kamati, na hili sina mswalie Mtume, kwa hili maslahi ya wafanyakazi hawa tumezungumza muda mrefu, hili niko tayari hata kuhamishwa Kamati nyengine nipelekwe kwengine, kwa hili sina mswalie Mtume, huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani, muda gani shilingi elfu tano tano Serikali mnalimbikiza madeni yao hawana haki hawa watu, shilingi elfu tano kuwapa hawa waandishi mimi hili sina mswalie Mtume.

Mhe. Waziri mwalimu wangu nitakuwa sina adabu mimi kuja kuzuia bajeti yako, lakini kwa hili aa. Serikali imeji-*commit* katika chombo hichi hichi kuwa kitawalipa, Waziri wa Fedha ambaye hayupo muda huu yupo mwengine hatuwezi kuendeshwa kama hivi tunavyoendeshwa, hawa wanafanya kazi nzito kuelimisha jamii, leo haki zao ramadhani kama hii tunataka kuwaonea, aa, *innaa lillahi wainna ilayhi raajiun*. (*Makofi*)

Mimi nina kitengo kidogo cha Ikulu cha Waandishi wa habari Mhe. Waziri upo Issa Ussi Haji (Gavu) na huko mbele pengine ndio dalili nzuri hizo pengine utabaki huko huko tunakwenda huko usoni, Mungu akujaalie uwe hivyo, waandishi wa kitengo cha Ikulu wa Tanzania Bara wanajulikana kama wameajiriwa na mikataba wamepewa, hawa kwa nini wa Zanzibar Leo mpaka leo wamekosa sababu gani, wa Bara wanapewa mikataba hawa waliokuweko Ikulu mpaka leo hawajaajiriwa kuna sababu gani, na kasoro gani hatuwezi kufika namna hiyo.

Suala la maslahi Mhe. Waziri nikuombe sana, na kwa vile ni msikivu mwalimu wangu mimi nafikiri utaonesha mfano ule, ukakamavu wako na uwezo wako utaondosha mapema hivi kabla jasho lao halijakauka.

Nije na sekta ya michezo uzuri Katibu wa Wizara hii ni mwanamichezo nilitaka kufahamu kwa nini wadhamini wetu wamekimbia wakiwemo *Zantel, Grand Malt,* sababu gani tueleze.

Hii leo kumekuwa na kichekesho hapa Unguja, Pemba wana ligi yao, Unguja wana ligi yao, tena asubuhi na mchana wakati wa kutafuta rizki ligi inachezwa asubuhi huu mpira utakuwa kweli, asubuhi kunachezwa ligi, mchana ligi baada ya kutafuta maji na kuni watu wakatizame mpira, hatuwezi kufanya kitu kama hivi.

Halafu kinakuja kitabu ramadhani yote hii tunasema tuna viwanja vitatu tunataka kujenga wapi Pemba, Unguja, Wilaya tufike pahali tujiulize jamani tunafanya nini leo tumekwenda kuvunja uwanja wa Mao, kwa sababu gani

mwaka mmoja na ushapita sasa hivi na utapita na mwaka mwengine hapa mtakuja kunambia hapa hapa kama utajengwa huo. Mungu asije akajaalia lakini dalili ziko hivyo.

Mwaka jana nilimuuliza Naibu Waziri ndugu yangu Issa Ussi Haji (Gavu) uwanja wa ndege ramani na michoro kipi kinakuja mwanzo, jasho lilimtoka, kama hatukuwa tayari sasa hivi ule uwanja kwa nini tumeuvunja hatujawa tayari kufanya kitu, *usiache tawi wakati hujakamata tawi*.

Leo mnatwambia umeme pale umeme upo, maji yapo, mnakuja kutwambia kitabu hichi haiwezekani hii na mimi nimewasihi sana Baraza lako la Michezo Mhe.Waziri, imeshafika wakati ulivunje mimi sijaliona tija yake, na humu imeeleza humu kwamba imepeleka watu, lakini sifikirii kama si michango ya wafanyabiashara hii ni kitu cha kushangaza sana, Mpira *ZFA* imekuwa inapoteza matumaini kwa washabiki wake kinyume na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa kumi na nane naomba kunukuu "Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kusaidia vyama na vilabu kushiriki katika mashindano kumi ya kitaifa ikiwemo chama cha *squash*, Chama cha baiskeli, chama cha Mpira wa wavu, chama cha Golf, chama cha Michezo". Haya ni maandishi tu haya, waseme nini kilichosaidia, haya ni maandishi tu kuandika ndio ule msemo wangu niliosema, ukiandika kiarabu huwa unavutia kwako tu hivi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiwa na dakika tatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa nisije nikasahau nilikuwa sina nia ya kuzuia bajeti hii lakini mimi kama alivyo Mhe. Waziri bahati nzuri yeye kapata jimbo kupitia kwa wananchi, na mimi nimepata jimbo kupitia kwa wananchi sikupata kutoka Ikulu, wananchi wa Paje hivi sasa wanafanyiwa vitendo ambavyo haviwaridhishi, na mimi ni mtumishi wao, na ndio ajira yangu ilipo hivi sasa, nilisema kwenye kamati na ilizuiwa na Waziri aliyepita nimshukuru Said Ali Mbarouk niseme ukweli, alifika pale saa tisa usiku na pensi yake tu akaenda akaona hali ilivyo, watu wanatoka mjini wanakwenda kuwaudhi wananchi wa Paje wamekosa nini hili nitahitaji maelezo, nilikuwa sina nia hata kuzuia bajeti.

Mhe. Waziri nilikueleza na mtumishi ili niseme hapa wasikie unga wangu usije ukaingia maji. Kuna Mhe. waziri jana Afisa wake hataki umtoke hapa naamini mtumishi, mimi sijafika wala Mungu asije akanijaalia kupata Uwaziri wala

Naibu Waziri, asije akanijaalia hasa ramadhani kama hii, Mwenyezi Mungu usije ukanijaalia mimi.

Kwa hivyo, nitahitaji maelezo wale watu wanaotoka mjini wakaenda wakapiga ngoma kule na mengine hata hayawezi kusemeka katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani nitahitaji maelezo, hoteli zile karibu mbili mpaka tatu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nisije nikapoteza muda na nikaja nikapoteza swaumu yangu. Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Kabla sijampisha mchangiaji wa mwisho Mhe. Zulfa, naomba wajumbe wote ambao wameleta michango yao wawasilishe michango hiyo kwa maandishi kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Awali ya yote naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na kuona tena mwezi huu wa Ramadhani tukiwa tuko katika hali nzuri.

Mimi niungane na waislamu wenzangu katika kuwatakia watu wote Ramadhani kareem, pia niwatakie waislamu wenzangu tuutumie mwezi huu mtukufu wa Ramadhani kama ni mwezi wa kujivunia, mwezi huu una baraka nyingi sana. Kwa hivyo kama ninavyoihusia nafsi yangu naomba tutumie muda wetu mkubwa sana kurudi kwa Mwenyezi Mungu kwa kuomba na kufanya yale memo yote, kwa sababu mwezi huu una faida nyingi sana ndani yake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sitaki nizungumze sana, nina mambo mawili tu nikianza katika sekta ya michezo. Wajumbe wengi sana waliosimama hapa wamezungumzia masuala ya *football,* lakini nimuombe Mhe. Waziri, sisi vijana tunachukua kwamba hii michezo ni sehemu yetu kuweka afya zetu vizuri, pia ni sehemu ya kukutana kubadilisha mawazo na pia ni ajira.

Mhe. Waziri pale katika Wilaya ya Chake Chake pana kiwanja kimoja kinaitwa kiwanja cha *Tennis,* hiki kiwanja kinatumiwa mara nyingi sana katika michezo yetu. Lakini la kusikitisha Mhe. Waziri kiwanja kile ni kibovu hakifai na michezo yote hususan inamalizikia pale.

Mhe. Waziri mchezo wa *Basketball* sasa hivi kwa vijana ni mchezo mkubwa ambao wanaupenda sana, na tunashukuru Pemba tuna timu ambazo zinacheza vizuri na kufika juu kwenda Tanzania Bara kushindana na ushindi wanaupata,

kwa hivyo Mhe. Waziri ningekuomba katika hivyo viwanja ambavyo umevizungumzia, sifikirii kama kuna viwanja vya *basket* au *netball* ambavyo utavifikiria. Lakini mimi nakuomba Mhe. Waziri katika viwanja hivyo vitatu alau kiwanja chetu hicho kimoja cha *Basket* tunakuomba ututengenezee ili mchezo wetu huu na sisi tuweze kuuendeleza kwa furaha.

Sasa niende katika sekta ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti, sekta ya utalii ni sehemu kubwa ambayo inatupatia pato katika nchi yetu lakini kuna kitu kimoja ambacho kinaniumiza kidogo.

Mhe. Mwenyekiti hawa watalii wetu wanapokuja katika nchi yetu sina uhakika kama wanapewa utaratibu wa mavazi kidogo, tunakuta kwamba tatizo la mavazi la hawa wageni wetu wanaoingia kwa sababu watu wameumbwa kuwa na wigo.

Mhe. Waziri jana nilikwenda *Airport* nikakutana na hawa watalii wetu, mavazi ambayo wameyavaa mimi mwenyewe nilifumba macho, sikwambii hawa vijana watakapoona ni lazima wataiga halafu tutaanza kusema kwamba vijana wameharibika.

Mhe. Waziri mimi kwa ushauri wangu hasa kwa kipindi hichi cha ramadhani, pangewekwa utaratibu pale kwamba wakiingia wageni basi waambiwe kwamba mavazi yanayoruhusiwa ni mavazi haya na haya, naamini kwamba wakija na zile nguo za kwao wataweza kununua, pawekwe japo duka wanunue japo kanga wajitande chini au vitenge basi na sisi tutaendeleza utamaduni wetu, wakivaa vile wakipiga picha wakifika kwao mtu akiwaona zile kanga watakapozipenda basi na sisi biashara yetu tutaitangaza.

Nikuombe sana tangazo hilo liwekwe la mavazi, ili tusije kuharibu hizi Ramadhani zetu au tusiharibu familia zetu, kwa sababu hata Mhe. Karume suala hili aliliona na alilipa mkazo, lakini sasa hivi nahisi halipo linatuharibia kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende Idara ya Habari na Maelezo, waandishi wa Mawio. Mimi naomba hawa waandishi wa Mawio uwatizame kwa jicho la huruma, watu hawa posho lao wanalipata pale wanapopeleka habari, lakini pale wanapokuwa hawana habari ya kupeleka wanakuwa wanabakia tu hawana lolote, na hawa ni muhimu sana kwetu, kwa sababu zile habari za ndani, za siri, za uchochezi, za umbeya zote tunazipata kupitia kwao. Mheshimiwa mimi naomba watu hawa uwaangalie kidogo ili wapate nguvu ya kufanya kazi yao.

Mhe. Mwenyekiti, kule Pemba tuna vikundi vyetu vya taarabu, kuna kikundi cha Kangagani maarufu kama Gogo. Hichi kikundi ni maarufu na kinafanya kazi zake wanapopaweza. Mimi ningekuomba kile kikundi ukisaidie, kwa sababu nyimbo zao tunaziona kwamba wanaenda katika asili yetu, wana nyimbo nzuri tu ambazo sisi wenyewe tutazipenda mkungu wa ndizi sijui Lulu.

Kwa hivyo mimi naamini kwamba Serikali ikiwaunga mkono hichi kikundi kinaweza kufika juu, lakini cha kusikitisha kwamba kile kikundi kimejitokeza zamani na wanafanya kazi zao lakini wako chini zaidi kwa kutokuwa na uwezo wa kujitangaza zaidi. Mimi naamini basi kwa Wizara yako itakapowawezesha watu wale tutapata burdani zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ila nawaomba waislam kwa mara nyengine tutumie mwezi huu mtukufu, ili tujivunie mema ili tutakapokwenda huko kesho akhera tukapate maisha bora hapa tunapita tu.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Zulfa kwa mchango wako mzuri, lakini kabla ya hapo napenda kutoa shukrani kwa Mhe. Waziri wa Habari kwa hotuba yake pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo.

Pia shukurani nyengine ziwaendee wale wachangiaji wote waliochangia katika hotuba hii nawapongeza sana, na wale waliokuwa hawajapata fursa ya kuchangia lakini fursa bado wanayo, michango yao wapeleke kwa Mhe. Waziri kwa maandishi.

Pia niwapongeze wasanii wa filamu wa kizazi kipya ambao tumeungana nao leo hii hapa nawashukuru sana kwa kuja.

Aidha niwatakie Ramadhani njema na Ramadhani yenye manufaa kwetu sisi na kwa vizazi vyetu.

Sasa baada ya kusema hayo machache nakiahirisha kikao mpaka kesho saa 3.00 Asubuhi lakini kabla Waziri kutoa majumuisho watakuja Waheshimiwa Mawaziri Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri na Mhe. Said Soud na baadae atafuatia Mhe. Waziri katika majumuisho. Ahsanteni.

(Saa 8.40 Baraza liliahirishwa mpaka
Tarehe 8/6/2016 Saa 3.00 Asubuhi)